

KISWAHILI



**SANIFU KWA SHULE
ZA SEKONDARI**

**KITABU CHA MWANAFUNZI
KIDATO CHA SITA**



ISHAKIRO

UTANGULIZI	iv
SURA YA KWANZA: FASIHI	1
SURA YA PILI: MNYAMBULIKO WA VITENZI	60
SURA YA TATU: UAMBISHAJI WA VITENZI	81
SURA YA NNE: UUNDAJI WA MANENO KATIKA LUGHA YA KISWAHILI	101
SURA YA TANO: UTUNGAJI	117
SURA YA SITA: UTUNGAJI WA HOTUBA	118
MAREJEO	130

UTANGULIZI

Vitabu ambavyo vilitangulia vilikuwa na lengo la kumsaidia mwanafunzi aweze kuzungumza Kiswahili sanifu na kukiandika kwa urahisi. Kwa hiyo, kitabu hiki kinakuja kuviunga mkono vitabu hivyo ili lugha ya Kiswahili iendelee kupiga hatua.

Kitabu hiki kitatumiwa katika kidato cha sita mkondo wa lugha ambapo lugha ya Kiswahili ni mojawapo wa masomo makuu.

Madhumuni makubwa ya kitabu hiki ni kuwaongoza wanafunzi na walimu wa shule za sekondari mkondo wa lugha kuhusu matumizi ya lugha ya Kiswahili na kuimarisha lugha hii.

Kitabu hiki kinaundwa na sura nne ambazo ni: **FASIHI, MYAMBULIKO WA VITENZI, UAMBISHAJI WA VITENZI NA MANENO YA KISWAHILI, UTUNGAJI (Risala na hotuba)**. Mwishoni mwa kila sura kumeandaliwa mazoezi ambayo yatawasaidia wanafunzi kufungua akili na kujaribu kuzama katika mada zilizojadiliwa kitabuni.

Katika kitabu hiki mkazo ni kueleza maana ya mnyambuliko na uambishaji wa vitenzi kama sehemu moja ya sarufi ambayo haikujadiliwa zaidi katika vitabu vilivyotangulia. Somo hili litamwongezea mwanafunzi ustadi wa lugha hii ya Kiswahili.

Uandishi wenyewe wa kitabu ulifanywa na **NDAYAMBAJE Ladislav** na **NIYIRORA Emmanuel** kutoka Chuo Kikuu cha Elimu cha Kigali (KIE).

Mwishoni, hatuna budi kutoa shukrani zetu za dhati kwa mtu yeyote aliyehusika katika kutoa maoni kuhusu uandishi wa kitabu hiki.

SURA YA KWANZA: FASIHI

1.1. DHANA YA FASIHI

Fasihi ni kioo na mwonzi wa maisha ya mtu na ya jamii. Ni sehemu ya utamaduni wa jamii: hushughulika na maisha ya jamii, huchota taarifa zake toka jamii, na kazi hubaki mali na amali (maana yake mambo yanayothaminiwa na kuhifadhiwa na jamii, dini, mila, ujuzi, siasa, jadi na lugha) ya jamii. Ni somo panuzi la ujuzi kuhusu lugha iliyo fasaha. Kwa upande mwingine, Fasihi ni aina ya sanaa ambayo wasanii wake huonyesha ustadi wao katika kutumia maneno kisanaa ili kuwasilisha ujumbe wao kwa wasomaji/jamii iliyonuiwa. Fasihi hutumia lugha kutufafanulia tabia za watu na athari zake huku ikituzindua ili tuone uzuri au ubaya wa jambo au tabia fulani kama vile wizi, wivu, tamaa na kadhalika.

Fasihi hushughulikia ulimwengu halisi na mambo yale yale yanayotuzunguka. Tunapoyachambua mambo hayo, tunaona kuwa yanatukia katika mazingira yetu pia na yanatupa mafunzo muhimu maishani.

1.2. TANZU ZA FASIHI

Fasihi ni moja lakini kutokana na jinsi taarifa inavyohifadhiwa na kurithiwa katika jamii, Fasihi husemwa kuwa ni ya aina mbili: Fasihi simulizi (mapokeo ya mdomo) na Fasihi andishi, yaani habari za kubuni zilizoandikwa. Baadhi ya habari hizo zikiwa zinatokana na Fasihi simulizi. Vitabu vilivyotangulia tulijadili kwa undani Fasihi simulizi na tanzu zake, ndiyo maana katika kitabu hiki tutajihusisha hasa hasa na tanzu tofauti za fasihi kwa mapana na marefu.

Kama tunavyogusia hapo juu, ni lazima kwanza kuona tanzu hizo na kuzijadili moja baada ya nyingine. Tanzu hizo ni: hadithi (hadithi fupi na riwaya), tamthilia, ushairi (mashairi, tenzi, ngonjera, majigambo).

1.2.1. Hadithi

Hadithi fupi

Hizi huwa ni hadithi za kubuni kutoka katika mazingira ambazo huhusishwa na matukio au mambo mbalimbali katika maisha ya watu ya kila siku.

Hadithi hizi hukusudiwa kuandikwa zaidi kuliko kusimiliwa.

Hadithi fupi, kwa umbo huwa fupi yaani angalau kuwa chini ya maneno 30, 000 hivi.

Fani katika hadithi

Katika kiwango hiki, tutazingatia mambo mbalimbali ya msingi katika kukabili kazi ya fasihi andishi au kazi yoyote ya kifasihi. Japokuwa hapa tutaingia zaidi katika kuitazama fani katika hadithi.

Kimsingi fani na maudhui hukamilishana, kwa sababu ujenzi wa fani huathiri moja kwa moja jinsi maudhui yanavyotolewa. Itokeapo kwamba fani inalegalega, basi hata maudhui itakuwa vigumu kuyafikisha yalivyokusudiwa. Hali kadhalika, upo umuhimu mkubwa kwa maudhui kuwepo katika fani bora. Vile vile tutaangalia jinsi vipengele mbalimbali vya fani vinavyoweza kuleta athari mbalimbali katika hadithi.

Katika utanzu wa hadithi, fani yake huzingatia mambo mbalimbali yakiwemo lugha, mandhari, mtindo, mtiririko wa visa (muundo) na mengineyo ambayo tutayaangalia kiundani zaidi hapa na hasa kuona vipengele hivyo jinsi vinavyotegemeana na kuhusiana katika kuunda na kukamilisha fani ya hadithi za Kiswahili.

Wahusika

Katika kujadili kipengele hiki, ni muhimu kuangalia mambo yafuatayo:

- Jinsi wahusika hao wanavyojengwa na
- Jinsi wanavyojitokeza katika kazi ya sanaa inayohusika.

Wahusika huwa ni watu, wanyama, vitu au viumbe wa kufikirika. Mwandishi wa hadithi, huwajenga wahusika wake kisanaa ili waweze kuwakilisha dhana mbalimbali za uhalisi wa maisha katika jamii.

Kwa hiyo, mwandishi wa hadithi au kazi yoyote ya fasihi hukabiliwa na kazi kubwa ya kuwaonyesha wasomaji wake jinsi wahusika wake walivyo; iwapo ni watu kwa kuwatambulisha na sifa zao; mambo wanayoyapendelea, na yale wasiyoyapenda, jinsi walivyo, wanavyokabili maisha, n.k. Matumizi ya lugha ya wahusika hao pia huwa muhimu. Jinsi wahusika wanavyotumia vipengele mbalimbali vya lugha kama tamathali za usemi, misemo mbalimbali, nahau, methali, n.k.

Baadhi ya wasanii, wameamua kuwapa wahusika wao majina yanayoelezea au kufafanua tabia zao. Msanii maarufu katika kutumia mbinu hii katika uandishi wa Kiswahili ni Shaaban Robert, ambaye hutumia majina ya: Hisidi kwa mtu hasidi, Adili kwa mtu adili, Mwivu kwa mtu mwenye tabia ya wivu, utubusara kwa mtu mwenye busara. Hata mahali ambapo matukio ya hadithi yanatokea, kwa sababu ni pa kufikirika tu, anapaita Ughaibu, kufikirika n.k.

Namna nyingine ni ile ya msanii kuwaelezea yeye mwenyewe jinsi walivyo.

“NYANGEZI alikuwa mtu mwenye roho iliyotakata, roho iliyompenda kila mmoja kikijini pao. Maneno yaliyokuwa yanataka ulimini mwake yaliwapendeza wote, licha ya kuwa na busara yeye hakuchagua hirimu ya watu.....”

Namna nyingine ni ile ya kuwaumba wahusika kutokana na matendo yao katika hadithi. Jinsi wanavyotenda, wanavyosema, wanavyowaza, maumbile yao na kadhalika.

Kutokana na ujengaji wa wahusika wa namna hii, msomaji anaweza kumwona mhusika akionyesha wasifu wake wa ndani na nje au anaweza kuonyesha mabadiliko yake.

Wakati mwingine ikibidi, mwandishi anaweza kumjenga mhusika mmoja kwa njia ambayo ni tofauti na wahusika wengine katika kazi yake kwa makusudi ili aweze kujenga dhamira aliyokusudia.

Msanii anaweza kuwawasilisha wahusika katika udhahiri. Katika mbinu hii sifa na matendo ya mhusika yanaelezwa waziwazi. Msomaji akishasoma hadithi inayohusika anaweza kumwelewa sana mhusika huyo.

Njia hii ya uumbaji wahusika husaidia kumfanya msomaji asipate taabu katika kutambua kiini cha kisa, wazo au dhamira, msanii hapa anamjenga na kumtumia mhusika huyo kutoka mwanzo hadi mwishoni mwa hadithi yake.



Uwasilishaji dhamira kwa upande mwingine huenda pamoja na mbinu nyingine za usimuliaji wa hadithi.

Kwa kawaida uwasilishaji dhamira hutokea wakati hadithi inaposimuliwa na msimulizi wa nafsi ya kwanza. Mfano wa hadithi hizo zinaweza kupatikana katika kitabu cha ***Kichwamaji*** kilichotungwa na Euphrase Kezilahabi. Katika usimulizi wake, mhusika mwenyewe hujieleza na kueleza kila jambo analolitenda.

Udhahiri pia unajitokeza wakati hadithi inaposimuliwa na mhusika mmaizi. Msimulizi huyo ni wa nafsi ya tatu ambaye anazijua siri zote za wahusika wote. Ni msimulizi anayeweza kuweko kila mahali kwa wakati mmoja na anayejua tangu mwanzo mambo yote katika dunia yake ya hadithi. Uumbaji huu unaweza kutumia utangulizi ambao mwandishi msanii anaweza kuuweka mwanzoni.

Msanii anaweza pia kuwaumba wahusika wake kwa kuwawasilisha kimatendo. Katika aina hii ya uwasilishaji, msanii hutumia ufafanuzi na huambatisha maoni yake. Sehemu kubwa aghalabu huachwa kwa msomaji anayetakiwa afasili maana na sifa za mhusika kwa kutoa vitendo kidogo kidogo, nusu nusu, hatoi matendo yote mara moja.

Msanii hutumia mazungumzo ya wahusika kama vile kati ya mhusika na mhusika. Hapa ndipo wazo la mhusika linapofafanuliwa. Kwa kuyaunganisha mazungumzo yote ya wahusika kutoka mwanzo hadi mwisho tunaweza kuijua tabia na pengine maumbile ya wahusika wa kazi ya sanaa inayohusika.

Makundi ya wahusika

Katika hadithi, tunaweza kuwagawa wahusika katika makundi matatu muhimu ambayo kwayo hutumiwa na mwandishi kutolea dhamira zake. Makundi hayo ni ya wahusika wakuu, wahusika wasaidizi na wahusika wajenzi.

a) Wahusika wakuu

Wahusika hao, ambao kwa kawaida ni mmoja au wawili hujitokeza kutoka mwanzo hadi mwisho wa hadithi. Mara kwa mara wahusika hawa hubeba kiini cha dhamira kuu na maana ya hadithi yote katika wahusika wa hadithi za tanzia, wahusika wengi huonyesha mabadiliko mengi kama vile anguko pia mhusika hufikia kilele na mwisho

akaanguka. Pengine mhusika anaweza kuonekana anapanda na kuwa mashuhuri, na halafu akakuwa duni katika hadithi.

Wahusika wakuu wanaweza kuwakilisha vikundi, jamii au mtu binafsi.

b) Wahusika wajenzi

pamoja na kuwepo kwa wahusika wakuu, wapo pia wahusika wajenzi. Wahusika hao ni muhimu sana kama walivyo wahusika wakuu katika kazi ya sanaa. Wakati mwingine wahusika wa aina hii hujengwa sambamba na wahusika wakuu katika juhudi ya kuwajenga na kuwafafanua vizuri zaidi wahusika wakuu. Kuweko kwa wahusika hao kunasaidia sana kuipa hadithi ama kazi nyingine ya sanaa mwelekeo muhimu wa kisanaa na maudhui. Wahusika hao wana tabia ya kujitokeza mara moja moja. Kwa jumla wahusika wote hawa wana tabia ya kuhusiana na kutegemeana. Wanasaidia kukuza, kudumaza ama kufanya maamuzi muhimu ya hadithini.

Tabia za wahusika

Katika makundi mawili ya wahusika tuliowaona hapa juu, tunaweza kupata tabia za wahusika za aina tatu. Tabia hizo ni za **ubapa, uduara** na **ufoili**.

i) Ubapa: ubapa huwakilisha aina moja tu ya tabia kutoka mwanzo hadi mwisho wa hadithi. Toka mwanzo hadi mwisho tabia hii inajidhihirisha katika mhusika anayeishi katika wazo na sifa za aina moja bila kubadilishwa na wakati, mazingira, uhusiano wao na wengine, n.k. Tabia hiyo haibadiliki kufuatana na hali za kawaida za maisha ya binadamu zinazobadilika kihistoria. Tabia hii inaelezwa kwa kutumia wahusika bapa-sugu na wahusika bapa-vielelezo.

Wahusika bapa-sugu ni wale ambao wanaonyesha msimamo wao kutokana na maelezo ya msanii. Wanakuwa sugu katika maana kwamba hawabadiliki, kila wanapoonekana hali zao huwa ni zile zile, hawahukumiwi bali huhukumu tu, hawashauriwi bali hushauri tu, hawaongozwi bali huongoza tu.

Wahusika bapa-vielelezo kwa upande mwingine ni wale ambao pamoja na kutobadilika kwao, wanapewa majina ambayo humfanya msomaji aielewe tabia na matendo ya mhusika huyo.

Katika hali hii ya wahusika, msanii anatilia mkazo wake katika aina moja ya tabia inayotawala, na ambao iwafikie wasomaji kiasi ambacho sehemu zote za sifa za mhusika huyo hazitokezi. Aidha, wahusika bapa hawawakilishi hali halisi ya tabia za watu wanaoishi, kwa kawaida huonyesha kipengele kimoja tu cha tabia hata kama wanakutana na mazingira mbalimbali.

ii) Uduara: uduara ni tabia ambayo mhusika mmoja hujenga akionyesha tabia tofauti. Wahusika wa aina hii wanaonyesha aina mbalimbali za tabia katika hadithi ama kazi nyingine japokuwa nazo haziwi zote zinazomhusu binadamu. Tabia ya uduara humfanya mhusika kubadilikabadilika kihulka, kimawazo na kisaikolojia.

Wahusika wenye tabia hiyo huonyesha kubadilika ambako kunatokana na msukumo wa nguvu zilizomo katika mazingira mapya. Sifa kuu ya wahusika wenye tabia hiyo, hadithini huishi maisha kawaida yanayofanana sana na jamii kiasi ambacho msomaji huwakubali kuwa ni wahusika hai.

iii) Ufoili: ufoili ni tabia inayojidhihirisha kati ya wahusika duara na wahusika bapa. Lakini pia ni tabia inayoonyesha hali zaidi kuliko wahusika bapa. Ili waweze kujengeka vyema, wahusika wenye tabia hii huwategemea sana wahusika duara na wahusika bapa. Kwa hiyo, wahusika wenye tabia ya ufoili wana msukumo wa nafsi ulio tofauti na wahusika wakuu ama wahusika wengine muhimu katika kazi ya sanaa.

MFANO WA HADITHI FUPI: MAMA WA KAMBO

Mama wa kambo:

Mzee Mnene alikuwa na wanawake watatu: Nyirabagenzi, Upendo, na Tunu. Nyirabagenzi alikuwa na mototo aitwaye Kagabo na Gasunzu. Baada ya miaka Fulani Nyirabagenzi akaachana na mzee Mnene Mnene. Mototo wake Kibaya akalewa na mama yake wa kambo, Upendo. Kibaya alionekana kuwa mototo hodari kwa masomo na kwa kazi. Walimu wake walikuwa walimpenda kwa sababu ya uelevu wake. Lakini badala ya kutumia mda wake kwa kusoma mara nyingi aliutumia kwa kufanya kazi za nyumbani kwa kupika chakula, kuchota maji, kuuza andazi, kufua nguo na kadhalika. Vile vile siku nyingi hakuenda shuleni kwa sababu ya kukopa karo za shule iwapo baba yake alikuwa mfanyabiashara huko Nyabugogo. Wakati ndugu zake walikuwa

wanafishwa vizuri na kuwepo ruhusa ya kutembelea, Kibaya yeye alikuwa anaambulia makombo, anavaa kufa Ulaya na kufanya kazi kama punda.

Mzee Mnene hakujali yaliyofanyiwa mtotowe kwa kuwa alikuwa anafanya zamu ya siku tatu kwa kila mwanamke na kuzamia katika shughuli nyingine. Hivyo kibaya hakuwahi kuendelea na masomo katika sekondari. Wakati mmoja, Kibaya aliugua Malaria akakosa mtu wa kumpeleka hospitalini. Mpangaji wa hapo anampeleka hospitalini kila asubuhi kwa kiutumia baiskeli yake alipopata nafuu alikataa kufanyia Upendo kazi zile zote bila malipo. Wakati huo alikuwa na miaka 18. Upendo alimshitaki kwa Mzee Mnene kuwa Kibaya anamtaka anamwambia kumtandikia. Kutoka siku ile, Mnene akachukua uamuzi wa kumpiga marufuku. Kijana huyo alisaidiwa na mzee Sembabazi kwa kumtafutia kazi katika Kumekucha Hoteli. Kwa uhodari wake wa kupenda kazi alipendwa mwajiri wake hata na hoteli ikawa na wateja wengi. Lakini siku moja KUMEKUCHA HOTELI ilipata ajali ya kuungua na moto na hoteli hiyo ikateketezwa yote. Kibaya mwenyewe aliugua vibaya.

Kibaya alikaa hospitalini kwa muda wa miezi minane na baadaye akarudi kwa mzee Sembabazi akiwa mlemavu. Alitafuta nyia ya kujifunza kwa kushona viatu. Kwa bahati nzuri, kampuni ya Bima ilimbalikia faranga milioni nne kwa ulemavu wake. Fedha hizo ndizo zilikuwa chanzo cha kazi yake ya ubiashara. Kibaya aligeuka mtu tajiri sana na akapatiwa jina la Kizuri badala ya Kibaya.

Wakati alipokuwa katika shughuli za kufunga ndoa na msichana aitwaye Amina, alivamiwa na majambazi. Majambazi hao walikuwa wanaongozwa na ndugu zake (watoto wa Upendo, Gasunzu na Kagabo). Lakini hawakufanikiwa bali ujambazi huo uliwageukia wakaaga dunia wote wawili. Upendo aliposikia habari hiyo naye aliamua kujiuwa. Mazishi yao yakafanyika siku moja.

UCHAMBUZI WA HADITHI FUPI: *MAMA WA KAMBO*

1. MAUDHUI

a) Dhamira kuu

Dhamira kuu katika hadithi ya *Mama wa kambo* ni:

- **Kutoswa kwa mama wa kambo:** Kibaya alipata mateso yaliyotokana na Upendo, mama yake wa kambo (kuachishwa shule, kufanya kazi kama punda, kushambuliwa, kufukuzwa)

b) Dhamira ndogo

- **Ushirika wa ndoa:** Mnene alioa wanawake watatu
- **Kuachika kwa ndoa:** ndoa ya Mnene na Nyirabagenzi iliachika.
- **Huduma mbaya za wazazi (malezi mabaya):** mnene kwa kutokuwa mwangalifu hakufuata malezi ya Kibaya na mwishoni alimfukuza.
- **Kutakia wengine misaada:** Mzee Sembabazi alimtakia Kibaya msaada kwa kumtafutia kazi. Mpangaji wa nyumba naye alimsaidia Kibaya.
- **Mapenzi:** mapenzi yanadhihirishwa na Kibaya na Amina.
- **Hudhuma za serikali ya kampuni ya bima:** serikali na Kampuni ya bima ilifanya kazi zao ipasavyo (bila rushwa au kuchelewesha kazi).
- **Dini:** dini ni taasisi muhimu katika kukuza utu na ubinadamu. Misaada ya waamini wa Kiislamu wa Kibaya.
- **Uwivu:** Upendo alionea kijicho mafanikio yote ya Kibaya akaamua kumtesa na kumkera kwa fitina na wengine.
- **Ujambazi:** ndugu zake Kibaya yaani Kagabo na Gasunzu walishambulia Kibaya kwa ajili ya kumnyanganya mali yake na kumuondoa duniani.
- **Kujuta:** kujutia kosa baada ya kutofanikiwa katika maovu na kuangamizwa na miradhi uliotengenezwa.

Maadili:

1. Mwavu huangamizwa na matendoye: Upendo, Gasunzu na Kagabo walipata shida kwa sababu ya wivu na matendo mengine ya uovu.
2. Majuto ni mjukuu: Upendo alijutia na kosa lake.

3. Mwenyezi Mungu ndiye mwongozi wa matendo yetu: Upendo alipanga mara nyingi kumuangusha hata kumuondoa duniani Kibaya lakini hakufanikiwa.
4. Mtaka makaa ya migomba haoni kitu ila majivu tu.
5. Tamaa mbele mauti nyuma: Gasunzu na Kagabo walikuwa na nia ya kujitayarisha kwa kumshambulia Kibaya lakini walijipatia mauti ya kifo.
6. Rafiki humuoni katika dhiki: Sembabazi aliyemsaidia Kibaya, Amina:
 - Kujitegemea kwa kutumia ubima,
 - Bora kuzaa watoto wa kutunza na kuletewa malezi mema.
 - Mama wa kambo si mama

FANI

Wahusika

Aina za wahusika:

- **Wahusika wakuu:** wahusika wakuu ni wawili: Kibaya na Upendo. Kibaya ni mhusika mkuu wa kweli na Upendo ni mhusika mpinzani wa Kibaya.
- **Wahusika wasaidizi:**
 - Mzee Mnene, Gasunzu na Kagabo ni wahusika wasaidizi wa upendo.
 - Nyirabagenzi, Sembabazi, Mpangaji wa nyumba, Amina ni wahusika wasaidizi wa kibaya.
 - Askari, afisa wa kampuni ya bima, ni wahusika wajenzi waliogeuka wasaidizi kwa Kibaya.

Methali zilizotumiwa:

1. Siku njema huonekana asubuhi
2. Kuzaliwa mwanamke ni balaa.
3. Kazi ndiyo msingi wa uhai

4. Ng'ombe wa maskini hazai
5. Alichokipoteza Mwenyezi Mungu hakuna binadamu wa kukiongoza na alichooongoza Mwenyezi Mungu hakuna binadamu wa kukupoteza.

1.2.2. RIWAYA

Riwaya ni hadithi ndefu kutosha iliyoandikwa. Huwa na mchangamano wa matukio, yaani ndani yake kuna matukio mengi. Riwaya ina dhamira zake, wahusika, muundo wake na mtindo wa aina yake.

Kwa upande mwingine, Riwaya ni hadithi ndefu ya kubuni, ambayo huwa inakusudia kuifikia hadhira kwa kupitia njia ya maandishi. Riwaya aghalabu huwa na maneno yanayozidi 30, 000. Riwaya ina dhamira zake, wahusika, muundo wake na mtindo wa aina yake.

Lugha itumikayo katika riwaya ni aina ya nathari (maandishi ya moja kwa moja, maandishi ya kawaida) na hutumia mchanganyiko wa vipengele vya lugha kama vile tamathali za usemi, methali, nahau, mafumbo, kejeli, ishara, n.k. Kwa sababu ya urefu wake, hifadhi yake huwa katika maandishi. Tusomapo riwaya tunatalii maisha ya binadamu, wanyama, na amali zote za jamii.

Aina za riwaya

Kuna riwaya za aina nyingi. Kuna riwaya za mapenzi, za upelelezi, za kisiasa, za kidini, za kihistoria, n.k.

Kuikabili hadithi

Katika fani ya riwaya inatubidi kuainisha mambo yafuatayo:

i) Dhamira kuu

Dhamira kuu yaweza kupatikana kutokana na kuduma za wahusika yaani mhusika na jumuiya yake; mhusika na jinsi anavyokabili mazingira katika riwaya; mhusika na itikadi. Dhamira ndogo ndogo pia huweza kujitokeza katika riwaya.

ii) Maudhui

Yaani mafunzo, falsafa, n.k. yatokanayo na riwaya nzima.

Maswali ya kujiuliza:

- Je, kichwa cha riwaya kinasadifu maudhui?
- Tumeambiwa nini? Yale tunayoambiwa yana ukweli wa maisha?
- Sehemu gani imetufurahisha au kutusikitisha zaidi?
- Sehemu gani haitufai au inatufaa?

iii) Fani: Jinsi riwaya ilivyojengeka. Lugha ya mjazo ndicho chombo cha kuibushia maudhui. Riwaya huwa na mtiririko wa vituko. Jinsi tukio moja linavyoathiri jingine ndivyo riwaya inavyosukumwa mbele. Riwaya vilevile huwa na upeo wake. Hapa ndipo hisia za msomaji zinapovutwa na tunapata mchomo kiasi cha haja yetu kukidhiwa. Mandhari ya riwaya ni ya aina nyingi. Matukio hutendeka katika sehemu mbalimbali za nchi na mwandishi huranda sehemu zote hizo akitupeleka wasomaji katika riwaya yake. Mwisho wa riwaya ndipo msomaji hutazamia ufumbuzi wa maswala yaliyoibushwa. Kuna riwaya ambazo huwaacha wasomaji wakielea na kuwafanya wafikiri katika kutafuta suluhisho. Riwaya huweza kuchukua mitindo mbalimbali. Kwa mfano, kuna ambazo mwisho huwa mwanzo na mwanzo huwa mwisho.

a) Wahusika: Wahusika katika kazi ya sanaa itumiayo lugha huweza kuwa watu, wanyama au viumbe vinginevyo. Wahusika katika riwaya si watu au viumbe halisi, bali ni mkusanyiko wa tabia kutoka kwa watu au viumbe halisi wanaoishi au walioishi. Madhumuni ya kuwaumba watu hao ni kuwakilisha dhana mbalimbali na kutoa ujumbe kwa jamii kama msanii anavyotaka. Mwandishi huonyesha sifa zao, hali yao, na maisha yao kwa ujumla katika ulimwengu waishimo. Watazungumza wakitumia vipengee mbalimbali vya lugha kama methali, nahau, misemo, tamathali za usemi, n.k.

Mwandishi anaweza kuwaeleza sifa za wahusika wake kwa kuwapa majina yenye sifa anazotaka kuwapa au anaweza kuwaelezea yeye mwenyewe walivyo kutokana na matendo yao, mawazo yao na maumbile yao. Ufuatao ni mfano wa uumbaji wa mhusika unaoangukia katika mtindo huo wa pili.

“.... Rosa alikuwa mzuri, mrefu kiasi, mnyenyekevu na mnyamavu. Kama akienda kuoga kisimani utamwona kabla ya kuvua nguo anaanza kuangalia huku na huko, huvua, huoga upesi, huvaa, huchukua maji na kurudi nyumbani. Akifika nyumbani anajikuta bado ana mapovu ya sabuni sikioni. Alikuwa hapendi kuangaliwa kwa muda mrefu. Ukimwangalia machoni huinamisha kichwa.....”

Kuhusu wahusika, ni lazima kuzingatia maswali haya:

- Je, wahusika wanakubalika kwa jamii? Kwa nini? Yupi hakubaliki? Kwa nini? Mhusika gani amependelewa zaidi? n.k

Aina za wahusika:

- **Wahusika wakuu:** Hawa hujitokeza tangu mwanzo hadi mwisho wa riwaya. Aghalabu hubeba kiini cha dhamira na maana ya hadithi yote. Matukio katika riwaya hujengwa yakiwazunguka wao. Wahusika hawa huweza kuwakilisha vikundi, jamii au mtu binafsi.
- **Wahusika wadogo:** Huwasaidia wahusika wakuu katika kusukuma migogoro ya hadithi mbele na kutoa maudhui. Wahusika wadogo huibuka wakati fulani fulani tu.

Aina hizo mbili za wahusika huweza kuwa wahusika bapa au la. Wakati wahusika ni bapa, huwakilisha aina moja tu ya tabia kutoka mwanzo hadi mwisho wa riwaya. Hawaathiriki na wakati, mazingira na mahusiano yao na wengine katika tabia zao. Wahusika bapa huwa ni kiwakilisho thabiti cha msanii katika kutimiza lengo fulani licha ya hali za kawaida za maisha ya binadamu ambao hubadilika kadiri wakati unavyopita.

Wahusika bapa hutambulika kwa tabia yao ya kuhukumu tu, kutoshairika, kupenda kuongoza tu, n.k. Pamoja na hali hizo za hapo juu, hupewa majina ambayo husadifu tabia zao. Hasa tabia ile inayomtawala mhusika, ambayo mwandishi angependa waione wasomaji. Hivyo, kama mhusika anatawaliwa na tabia ya kujivuna ataitwa Majivuno, kama ni mbinafsi ataitwa Boramini, n.k.

Kundi jingine, licha ya wahusika bapa, ni lile la wahusika huria au wahusika duara. Hawa huwa na aina mbalimbali za tabia katika riwaya. Hubadilika kitabia, kimawazo, kinafsia, n.k. Tabia zao hufuatana na mazingira mapya yanayotia nguvu na msukumo

mpya, nao hupitia ngazi za kawaida za maisha. Hukua, huumwa na hata kufa panapopasa. Hivyo, huwakilisha uhalisi wa maisha.

Mtindo:

- Msanii ametumia lugha namna gani? Je, kuna tamathali za usemi, mafumbo, methali, kejeli, n.k.

Picha alizochora msanii zimeeleweka na zimemsaidia kumrahisishia maelezo yake?

- Msanii ametumia mbinu zipi: mazungumzo, mijadala au hadithi ndani ya hadithi?

Muundo:

- Muundo wa riwaya umeanzaje?
- Msanii anatupelekaje kwenye upeo na tamati?
- Je, msanii anafaulu kujenga kiini kimoja kutokana na mchangamano wa matukio mbalimbali?
- Mandhari yanawiana ama hayawiani na mazingira ya kweli?

Kufaulu kwa msanii:

Kufaulu au kutofaulu kwa riwaya ya msanii kutategemea jinsi alivyoweza kuonisha maudhui na fani katika kazi yake.

MFANO WA UCHAMBUZI WA RIWA YA “ADILI NA NDUGUZE”

UCHAMBUZI WA RIWAYA “ADILI NA NDUGUZE”, Shaaban Robert.

SURA YA I: Mfalme Rai

Mfalme Rai alikuwa mtawala wan chi ya ughaibu. Mfalme huyo alikuwa na tabia kuu tatu, alikuwa:

- Msuluhifu,
- Mtunzaji wa wanyama (aliwajali na kuwahurumia) na
- Mtii kwa majini.



Ughaibu ilikuwa nchi ya ufugaji. Uchumi wa nchi hii ulitegemea mifugo. Mfalme Rai alikuwa mwenye bidii ya kazi mfuatili wa utendaji wa kazi. Nchi ya Ughaibu ikawa haina mwivu, goigoi na mwoga kwa sababu ya kiongozi wake, mfalme Rai aliamini kuwa “*tendo hukidhi kaja maridhawa*” Rai alikuwa mpenda haki na asiye kubali rushwa.

SURA YA II: Siri inafichuka

Ikibali mshauri wa halmashauri ya Ughaibu na mshauri wa Mfalme Rai, alikuwa mcheshi mwenye kuchukuana na watu sana. Ikibali alitumwa Janibu kwenda kuangalia malipo ya kodi. Malipo hayo baada ya uchunguzi hayakuwa na hitilafu bali yalikuwa na ziada. Akiwa Janibu, Ikibali alimwona Adili akawaadhibu kikatili manyani wawili. Ikibali alishindwa kuvumilia na kuficha siri hii akalazimika kumweleza Mfalme Rai ambaye alialika Adili aletwe mbele yake ajieleze na manyani wale wawili.

SURA YA III. Adili mbele ya Rai

Adili alikuwa mtu mwenye huruma. Ukatili alioufanya dhidi ya manyani alilazimishwa tu, hakuhiari yeye mwenyewe. Alikuwa na upendo, wakati wa kuadhibu wanyama ambao walikuwa zamani ndugu zake, alikuwa anasema

«Nala sumu ndugu zangu, msambe naona tamu,
Takalifu kubwa kwangu, kuadhibu yangu damu,
Sina raha ndugu zangu, neno hili kwangu gumu.»

Kugunduliwa kwa siri yake, kulimfurahisha Adili kwani naye alipenda ijulikane. Adili alimweleza Mfalme Rai kisa kilichomfanya manyani wake kuadhibiwa vile.

SURA YA IV. Ndugu zake

Adili alikieleza kisa cha kuzaliwa watoto watatu; yeye mwenyewe, nduguze wawili Hasidi na Mwivu. Baba yao Faraja ambaye alipewa jina hilo kwa kuwa amewafariji wazazi wake baada ya kufiwa na ndugu yake pacha. Aliwasomesha watoto wake. Ndugu hao watatu walikuwa watu wazima «wenye vichwa vilivyofunzwa lakini mioyo yao ilisahuliwa».

Baada ya kifo cha Faraja, watoto waligawana urithi sawa. Adili aliendesha biashara vyema, akitunza hesabu zote kwani alielewa kuwa “**mali bila daftari hupotea bila habari**”. Ndugu zake walifanya biashara nchi za nje, wakapata faida kubwa na mali yao yote ikapotea. “Mtu kushindwa kujua pato lake mwenyewe kwaonyesha uchache wa uangalifu”.

SURA YA V. Mgawo mwingine

Kwa huruma yake Adili aliamua kugawa mali yake katika sehemu tatu. Aliwaonya ndugu zake juu ya madhara ya mtu kuendeleza ulevi na kuwa mwivu. Adili alikubali kwenda nchi za nje pamoja na ndugu zake kufanya biashara. Adili alikubali akielewa kwa dhati faida za safari kama vile hizi zifuatazo:

1. Kufajirika katika hamu,
2. Kujua namna ya kuendesha maisha,
3. Kupata elimu mpya,
4. Kuelewa tabia za watu mbalimbali,
5. Kukutana na marafiki wa kweli (mara nyingine kushinda ndugu),
6. Kupata bahati njema ugenini.

SURA YA VI. Tandu na nyoka

Adili na nduguze walitembelea miji kadhaa ya awali na walipata faida kubwa katika biashara.

Wakati wakienda miji mingine waliishiwa na maji ya kunywa baharini. Walitia nanga jabalini ili kutafuta maji. Jabalini Adili alimsaidia tandu ambaye alikuwa anashambuliwa na nyoka. Tandu aligeuka msichana alimwomba dua njema Adili imfae maishani na ahera. Alimuahidi kumsaidia naye wakati ujao apatapo matatizo.

Nyoka aliyuawa aliwaka moto, akawa majivu na majivu yakageuka chemchemu ya maji safi. Walipata shida ya maji tena, Adili alipowaomba ndugu zake wamsindikize kutafuta maji walikataa.

SURA YA VII. Mji wa mawe

Adili alipofika mji wa mawe, alishangaa kuona watu na wanyama wote wanageuka mawe. Aliuona utajiri mkubwa alioshindwa kuuchukua. Kama alivyosema mwandishi “Fikra ya mali isiyo kadiri ni mzigo usiochukuliwa”.

Pia aliona halmashauri mbili, ya wanaume na wanawake, zote mbili zilikuwa na watu waliogeuka mawe.

SURA YA VIII. Mrithi wa mji wa mawe

Adili katika upelelezi wake alifanikiwa kuingia katika chumba kimoja ambamo alimkuta msichana aliye hai. “Msichana huyu uso wake ulikuwa umetukuka kwa uzuri uliokuwa haumithiliki”. Kama uzuri ulio peponi wamajaliwa malaika karibu uzuri wote ulio duniani alijaliwa msichana huyo matambo yake yalikuwa kama mfutano wa mziki.

Mshale wa mapenzi ulipenya katika moyo wa Adili na haukuacha nafasi ya mapenzi ya mwanamke mwingine.

Sifa za Mwelekevu katika shairi ni hizi zifuatazo:

1. Miguu ya msichana,
Na mwendo aliokwenda,
Adili alipoona,
Moyowe ulimshinda.
2. Alikuwa na miguu,
Mfano wa cherahani,
Wala ulimwengu huu,
Hajatokea kifani.
3. Alipendeza hatua
Wakati alipokwenda,

Chini viatu vyalia,

Mithili kama kinanda.

4. Alikwenda kwa madaha,

Mwanamke mwenye enzi,

Yaliyompa furaha,

Kila mwenye kubalizi.

SURA YA IX. Mji ulivyogeuka mawe

Adili alipewa maelezo na Mwelekevu jinsi mji ulivyogeuka mawe. Mfalme Tukufu na Malkia Enzi walikuwa watawala wa nchi hii. Ufalme wao ulikuwa na utukufu na enzi. Nchi ilikuwa tajiri sana, shujaa na yenye mawaziri wenye busara. Wote waliabudu mizimu.

Mrefu, Malaika-mtume wa Mola alionya Mfalme Tukufu lazima awe mwadilifu katika matendo yake, awe mfano mzuri kwa raia wake. Alionya kuwa ibada ya mizimu matokeo yake ni maangamizi. Mfalme Tukufu hakukubali onyo la Mrefu, akaamuru Mrefu ashikwe. Mrefu kwa uwezo aliopewa na Mungu, aliizamisha miji yote ndani ya bahari na kilichokuwa na maisha chote katika fahali kiligeuka jiwe. **“Walakini mapendeleo yakiachwa mbali, nuru ya fikra humulika mno siku zote juu ya kweli kuliko uongo na juu ya haki kuliko dhuluma”**.

Nuru hii ndiyo ilimwoko Mwelekevu mpaka alipookolewa na Adili. Adili alichukua mali aliyoweza na maji.

SURA YA X. Kutoswa kwa Adili

Adili alipofika jahazini aliigawa mali yake kwa ndugu zake, nahodha na mabaharia. Nduguze hawakuridhika kwa sababu ya choyo chao kikubwa. Walitaka pia msichana yule wamuo wote watatu. Adili aliwaonya kuwa «ndoa haitaki ushirika, ushirika katika ndoa ulipasa wanyama na ndege. Dunia yapaswa kuwa mahali pa kiasi siyo ulafi na uchafu. Mwanaume hakukusudiwa kuwa fahali wa kila mtamba mwanamke



kuwa mtembe wa kila jogoo». Kwa chuki na wivu, nduguze walimtosa Adili baharini kama kitu kilichokuwa hakifai.

SURA YA XI. Wokovu wa Adili

Akiwa baharini Adili aliokolewa na ndege. Ndege huyu alikuwa ni tandu aliyemwoko asiuaawe na nyoka pale jabalini. Tandu alijigeuza msichana aliyetitwa Huria binti kisasi. Kisasi, Mfalme wa majini na Mjeledi, mke wake. Nyoka aliyekuwa akikimbiza tandu alikuwa Hunde, waziri wa Ngazi. Hunde alikuwa kiumbe wa mwisho katika wanaume waliokuwa na sura mbaya. Alitaka kumwoa Huria kwa nguvu.

Wanawake:

- i) Mioyo yao hulemewa na haja zilizokubalika
- ii) Masikio yao hutwa uziwi kwa maombi ya haraka
- iii) Na miili yao ni mawindo ya jeuri daima.

«Wanaume wana inda mbaya ufidadi unapowapofusha». Wema wa Adili ulilipwa kwa fadhili Ujijini. Alipewa kitabu cha hawala za hazina ya majini.

SURA YA XII. Nduguze kuwa manyani

Marejeo ya Adili jahazini yaliwafanya Mwivu na Hasidi waone haya. Waliangua kilio cha kusingizia ingawa «kilio cha kujisingizia hakina machozi wala matanga» kama wasemavyo Waswahili. Adili aliwatuliza nduguze akisema, «bahari haiweki amana kitu kieleacho».

Huria alitamani uovu wa nduguze Adili ulipwe kwa kifo. Adili aliwaombea msamaha alikumbuka kuwa «Damu nzito kuliko maji». Huria aliamua kuwageuza na kuwafanya manyani.

SURA YA XIII. Adhabu ya kwanza

Adili alifika salama Ughaibu ila alisahau maagizo ya Huria. Adhabu ya kwanza akaipata yeye mwenyewe. Tokea hapo aliendelea kuyaadhibu manyani yale. Huria aliamini



kuwa **”adhabu kali kwa waovu, ilikuwa ndiyo ulinzi bora peke yake wa wema”**.

Baada ya kuyapiga manyani, Adili aliyanasihi akisema:

“Nala sumu ndugu zangu,
 Msambe naona tamu,
 Takalifu kubwa kwangu,
 Kuadhibu yangu damu,
 Sina raha ndugu zangu,
 Neon hili kwangu gumu”.

SURA YA XIV. Kula na manyani

Adili aliyahadithia yale yote yaliyotokea kwa sababu naye alitaka siri yake ijulikane kwa Mfalme Rai ili aweze kuwaombea nduguze msamaha. Jitihada za kuyaokoa manyaniyale zilifanywa na Rai. Alimwandikia Huria barua ya kumtaka awasamehe akiahidi kuwa tendo hilo lilifanya Ufalme wake kuwa rafiki ya Ufalme wa majini.

Siku hii, baadala ya kuyapiga manyani, Adili alikula pamoja nayo mezani, akayapa uhuru na kulala nayo chumbani.

SURA YA XV. Arusi

Alipoulizwa sababu yake ya kuvunja amri alipewa na Huria, Adili alimtolea barua ya Rai. Ombi la Mfalme Rai lilikubaliwa na Mfalme wa majini Kisasi. Huria aliamuru:”Tokeni katika uhawayani mrudi katika utu!” Hapo hapo Hasidi na Mwivu, nduguze Adili wakawa watu tena.

Ndugu hao wawili walishukuru sana na kahidi kuwa walikoma kutenda dhala lolote kwa ndugu yao na mtu yeyote mwingine au kitu chochote kingine kilichokuwa na maisha. Watu wote hapo walifurahi na kumwomba dua Adili azidishwe cheo.

Adili aliwavisha nduguze nguo nzuri na kwenda tena Ughaibu. Walipofika pale walikuwa na furaha kubwa sana. Waliporudi kwao Janibu njiani Adili alikutana na



Mwelekevu aliyekuwa na wasichana wawili. Adili alibusiana na Mwelekevu na nduguze wakaamkiana na wasichana wenzake Mwelekevu.

Walifunga safari kuelekea Janibu. Walipofika pale Janibu walifanya arusi tatu siku moja. Adili alimwoa Mwelekevu na nduguze kila mmoja akamwoa kila mwingine mwa wasichana wale nduguze Mwelekevu. Siku hiyo ilikuwa kubwa sana kuliko zozote zingine zilizopita Janibu.

Uchambuzi wa jumla wa “ADILI NA NDUGUZE”

Utangulizi

Adili na nduguze ni riwaya iliyotungwa na SHAABAN Robert; mwandishi mashuhuri (maarufu) kutoka Tanzania. Riwaya hii ilitungwa mnamo 1952. Katika riwaya yake anashughulika na mambo mengi kuhusu tabia mbalimbali za watu. Mtunzi anatueleza kuwa tushinde uovu kwa kutenda mema yaani “Wema hauozi”. Adili alimwokoza Huria wakati alipokaribia kuuwawa na Hunde. Kutokana na wema huo, Huria naye alimwokoza Adili wakati alipotoswa baharini na ndugu zake. Haya yanazingatiwa na msembo wa Kiswahili “kinifaa huangua, nitakufaa kwa mvua” au methali isemayo “Mwosha huoshwa”.

1. Mandhari

Mandhari ya riwaya hii ni ya nchi ya Ughaibu, yaani nchi ya mbali. Nchi hiyo ni ya kufikirika kwa kuwa haipo katika mazingira ya kawaida. Kuna vituko vichache vilivyotokea katika nchi za kigeni zisizotajwa kwa majina na vingine vilitukia katika nchi ya majini.

2. Wahusika

Wahusika wa SHAABAN Robert katika riwaya ya *Adili na Nduguze*, aliwapa majina yanayowiana na tabia zao. Wale ambao hawakubadilika kitabia kama Adili, Mfalme Rai ni **wahusika bapa vielezo**. Wahusika Huria, Hasidi na Mwivu ambao walibadilika kitabia ni **wahusika duara**.

3. Wahusikana tabia zao

- **Adili:** shauri; onyo.
- **Hasidi:** mtu mwenye tabia ya kutofurahia mafanikio ya mwingine (husada)
- **Mwivu:** mtu menye kijicho; asiyependa mafanikio ya mwingine
- **Mfalme Rai:** wazo au maoni ya mtu juu ya jambo fulani
- **Kurai:** kusema na mtu kwa maneno mazuri kwa madhumuni ya kumtaka akubali kutimiza linalotarajiwa.
- **(I) kibali:** ruhusa, idhini
- **Mwelekevu:** mtiifu; mwenye urahisi wa kukubali maelezo (mwongozo)
- **Huria:** mwenye uhuru wa kutenda kila jambo analotaka
- **Mrefu:** mwenye kimo (kipimo) kilichozi kingine (cha kawaida)
- **Mfalme Tukufu:** mheshimiwa, mtu mwenye madaraka au cheo cha juu
- **Malkia Enzi:** utawala, utukufu
- **Hunde:** kiumbe cha ajabu kinachitisha
- **Mfalme Kisasi:** malipo kwz ajili ya tendo bayaalilofanyiwa mtu#fadhila (au fadhili).
 - **Adili:** ni mhusika mkuu wa riwaya hii. Alikuwa mwema, mwenye huruma, msamehevu, mvumilivu, jasiri na mfanyabiashara hodari. Tabia yake ile haikubadilika toka mwanzo hadi mwisho wa hadithi. Kwa hiyo, tabia yake ni mhusika bapa kielelezo.
 - **Hasidi na Mwivu:** ni ndugu zake Adili. Walikuwa watu wakatili, wenye tamaa, choyo kikubwa na wabadilifu kitabia, kwa hiyo ni wahusika duara.
 - **Mfalme Rai:** alikuwa mtawala wa nchi ya Ughaibu ambaye aliiletea nchi yake ustawi wa kiuchumi kutokana na uongozi mzuri, ufuatilizaji bora wa kazi na ushauri wa kuwahimiza raia kuwa wachapakazi.



- **Ikibali:** ni mshauri wa Mfalme Rain a Halmashauri yake. Alikuwa mcheshi na mtu aliyechukuana na watu kutokana na kuwatunzia haki zao.
- **Mwelekevu:** ni msichana mwenye upendo wa kweli, mrembo na mwaminifu kidini na kindoa.
- **Huria:** ni jini lililokuwa na uwezo mkubwa wa kutenda kila jambo lililotaka na kujigeuza sura kwa utashi wake (mhusika duara)
- **Mfalme Tukufu na Malkia Enzi:** ni watawala ambao walipuuza/walidharau ujumbe wa Mola, wakaadhibiwa kugeuzwa mawe, mji wao na raia wao.
- **Mfalme Kisasi:** ni mfalme wa majini aliyewaelekeza raia wake majini kutii uongozi wa binadamu.

3. Dhamira kuu

“Mapendeleo yakiachwa mbali nuru ya fikra humulika siku zote juu ya kweli kuliko uongo, juu ya haki kuliko dhuluma na juu ya wema kuliko uovu”.

4. Dhamira ndogo ndogo

- a. Uongozi mzuri na ufuatiliwa bora wa kazi wa Mfalme Rai uliomwezesha kuistawisha nchi ya Ughaibu katika mifugo,
- b. Uchunguzi mzuri wa Ikibali uliomfanya agundue hila za Adili kuwaadhibu vikali manyani,
- c. Ukalili uliochanganywa na huruma dhidi ya manyani ambao zamani walikuwa nduguze Adili,
- d. Utetezi wa Adili mbele ya Mfalme Rai na kukieleza kisa cha baba yao Faraja kuwazaa ndugu watatu, Adili, Hasidi na Mwivu,
- e. Mvuto wa faida za biashara safarini baada ya mgawo wa urithi wa Adili na nduguze waliofilisika,
- f. Wokovu wa Tandu aliyeshambuliwa na nyoka na bahati ya Adili kupata maji safi,
- g. Mji wa mawe uliokuwa na mali isiyo kadiri

- h. Mapenzi ya Adili na Mwelekevu, msichana aliyekutwa hai katika mji wa mawe,
- i. Habari ya mji na watu wake kugeuzwa mawekutokana na ibada ya mizimu,
- j. Wivu wa nduguze Adili kumwona na mchumba na kumtosa baharini,
- k. Wokovu wa Adili aliyeokotwa na Huria,
- l. Marejeo ya Adili jahazini na nduguze kugeuzwa manyani,
- m. Adhabu kali kwa manyani baada ya Adili kuadhibuwa mwenyewe kwa kutotii amri ya Huria.
- n. Jitihada za Mfalme Rai kuokoa manyani waliokuwa nduguze Adili,
- o. Ombi la Mfalme Rai lililokubaliwa na Mfalme wa majini Kisasi na bintiye Huria la kugeuza manyani kuwa watu tena na ndoa ya ndugu wote watatu.

5. MHUTASARI: *Adili na Nduguze*

Uongozi mzuri na ufuatiliwa bora wa kazi ulimfanya Mfalme Rai kuistawisha nchi yake ya Ughaibu katika mifugo. Mshauri wake Ikibali alikuwa bingwa wa uchunguzi wa kodi za wanyama ila alielemea na siri ya kiongozi wa Janibu, Adili kuwaadhibu vikali manyani waliokuwa kwake. Alishangaa kuona jinsi ukatili huo ulivyohitilafiana sana na tabia ya wema na huruma ya Adili akaamua siri hiyo ifichuliwe mbele ya Mfalme Rai.

Alipoletwa mbele ya Mfalme Rai, Adili alijitetea akieleza kuwa wanyama hao walikuwa zamani nduguze kwani walizaliwa na baba mmoja, Faraja. Alijulisha kuwa alilazimika kuwagawia urithi wake wakati walipofilisika ugenini na kurejea nyumbani kwao Janibu. Alisimulia jinsi ndugu wote watatu walivutwa na faida za biashara na kusafiri mpaka walipoufikia mji wa mawe, Adili alipokutana na mchumba wa kuusiwa, Mwelekevu.

Hapo hapo, Adili alieleza kuwa uovu waliomfanyia nduguze ndio uliwafanya wageuzwe kuwa manyani. Kwanza kutokana na mali aliyoleta jahazini na mwanamke huyo mrembo kutoka mji wa mawe, nduguze walimwonea wivu na kumlia njama za kumtosa baharini.

Wakati huo huo, aliokolewa na jinni, Huria binti Kisasi, ambalo aliwahi kusaidia lililoshambuliwa na nyoka, ama jinni jingine Hunde.

Adili aliporejea katika chombo akiwa na Huria, jinni hilo ndipo liliamua kuwafanya manyani ikiwa ni adhabu na kutoa amri ya kuwa watapigwa kila siku kutokana na maovu yao.

Adili aliporudi nchini mwake, Ughaibu, ndiye aliadhibiwa wa kwanza kwa kusahau kuwapiga manyani. Tokea hapo ilikuwa mazoea yake kuwapa chakula na kuwapiga vikali hadi siku, Ikibali aligundua siri hiyo.

Baada ya kisa hicho, Mfalme Rai almsihi Adili asiwapige tena manyani ila awatunze vizuri na kula nao. Alijitahidi kuwaombea msamaha kwa Mfalme wa majini Kisasi na bintiye Huria. Ombi lake lilisikilizwa na nduguze Adili waligeuzwa kutoka uhawayani na kuwa watu tena. Siku hiyo ilikuwa ya furaha, na nduguze wote watatu walifunga ndoa pamoja.

6. Mtindo

Mtindo wa riwaya hii ni mtindo wa rejea. Mwandishi huanza kuisimulia riwaya yake wakati Adili alifanya ukatili wa kuwaadhibu manyani (ambao walikuwa nduguze).

Kugundulika kwa uovu huu ndiko kulifuatiliwa na maelezo ya kisa na sababu ya nduguze kuwa manyanina hatimaye kuwa watu tena baada ya ombi la Mfalme Rai kukubaliwa na majini.

Lugha ya Shaaban Robert katika riwaya ya **Adili na nduguze** ni nzito. Ni lugha yenye msamiati mgumu, misemo isiyo ya kawaida, nahau na methali nyingi. Pia ametumia lugha ya ushairi, lugha ya picha na tamathali za usemi za kipekee. Kuna wakati mwandishi huyu alipotumia lugha ya kisheru katika barua, na hayo yote ni kuonyesha jinsi ana ustadiwa kuimudu lugha ya Kiswahili katika nyanja zake zote.

Matumizi ya lugha

a) Tamthali za usemi

- Tashbiha:

Uk. 1: Tabia yake ijigawa katika theluthi tatu mbalimbali **kama** rangi ya ngozi ya pundamiliya.

Uk. 27: Aliwapenda **kama** penzi ya maisha yake mwenyewe.

Uk. 33: Aliwapenda **kama** punzi ya maisha yake.

Alikuwa na miguu **mfano wa** charahani.

- Sitiari:

Tamaa kwake ni gurudumu la maisha

Lugha ni pandamizi kubwa kwa watu duniani.

Adili alitamka kuwa maisha ni safari na duniani ni matembezi.

- Kipanafsi: "Moyowe ulimshinda"

Msanii amechukua moyo kama mtu.

Moyo ulimshinda ni kusema hakuweza kuzivumilia hisia za moyo wake. Kwani bila kujitambua alinaswa na uzuri wa Mwelekevu, binti Mfalme Tukufu.

b) Matumizi ya methali na nahau

i) Methali

- Mali bila daftari hupotea bila habari,
- Wema hauozi,
- Asiyefurahia heri ya mwenzake shauri yake hunghadhabika,
- Mkulima alikuwa mmoja siku zote lakini walaji wengi,
- Damu nzito kuliko maji,
- Ng'ombe wa masikini hazai picha,
- Busara kubwa kichwani haina faida kama moyoni.

ii) Nahau

- Kukata tama: kupoteza matumaini
- Macho yao yalii.

c) Matumizi ya mashairi

1. Miguu ya msichana,
Na mwendo aliokwenda,
Adili alipoona,
Moyowe ulimshinda.
2. Alikuwa na miguu,
Mfano wa cherahani,
Wala ulimwengu huu,
Hajatokea kifani.

Msanii alitumia ushairi kueleza kwa usanii uzuri wa Mwelekevu.

7. Muundo

Muundo wa riwaya hii unaambatana na kisa kinachomhusu Adili na nduguze, Hasidi na Mwivu. Mwandishi alieleza jinsi vituko vilivyotiririka tokea mwanzo, ndugu hawa watatu waliokuwa wakitoka familia moja, uovu ndugu wawili, Hasidi na Mwivu, waliomfanyia Adili na malipo ya uovu huo (kama upeo wa kugeuzwa manyani na kupata adhabu ya kupigwa kila siku). Mwishoni kabisa anaujadili msamaha waliopewa ndugu hao. Kutokana na majuto na ahadi ya kutorudia tena uovu huo.

8. Maadili

- Wema hauozi (mt),
- Kazi ni msingi wa maendeleo (ms),
- Tendo hukidhi haja maridhawa (ms),

- Hulka njema sawa na mali (ms),
- Damu nzito kuliko maji (mt),
- Mali bila daftari hupotea bila habari (ms),
- Mbwa wa msasi mkali ni wakali pia (mt),
- Mapendeleo yakiachwa mbali nuru ya fikra humulika siku zote juu ya kweli kuliko uongo, juu ya haki kuliko dhuluma na juu ya wema kuliko uovu (ms),
- Turufu huenda siku zote kwa mchezaji (mt),
- Chama chema huvikwa pete (mt),
- Wema utashinda na ubaya utashindwa.

9. Uhakiki

Mwandishi Shaaban Robert amefaulu kuieleza hadithi yake kwa mpangilio bora wa visa vyake akianzia kuwaletea wasomaji shauku ya kujiuliza “Manyani yanapigwa kwa sababu gani? Na yahusiaje na watu?” Amewachora vizuri wahusika wake akiwapa majina yanayowiana na tabia zao. Wale wenye tabia nzuri ni mfano mzuri katika jamii yaani wanafaa kuigwa. Na wahusika wenye tabia mbaya ni mfano wa kupigwa marufuku, usiofaa kuigwa katika jamii.

MAZOEZI

1. Riwaya ni nini?
2. Riwaya huhifadhiwa kwa njia gani ili isisahaulike?
3. Eleza sifa na tabia mbalimbali za wahusika
4. Fafanua dhana zifuatazo:
 - a) Mandhari katika riwaya
 - b) Upeo wa riwaya
 - c) Mwisho wa riwaya
5. Lugha inayotumika katika riwaya ni aina gani?

6. a) Riwaya hujengwa na mambo gani?
- b) Eleza sifa za wahusika bapa.

1.2.3. TAMTHILIA

a) Utangulizi

Ni uwanja mpana unaochukua dhana ya sanaa za maonyesho na michezo ya kuigiza. Katika kiwango hiki tutashughulikia michezo ya kuigiza.

Sanaa za maonyesho ni uwanja mpana sana. Kwa mfano mchezo wa mazingaombwe unaonyesha maajabu jukwaani, hiyo ndiyo sanaa ya maonyesho bendi (maarufu).

Michezo ya kuigiza hujengwa na wahusika na migogoro iliyomo mchezoni hali ya fujo, kutoafikiana baina ya pande mbili. Hiyo migogoro ndiyo inayokuza mwendo wa igizo katika tanzu hii. Migogoro huendeshwa na wahusika katika mazungumzo.

b) Dhana ya michezo ya kuigiza

Michezo ya kuigiza hutungwa kwa madhumuni ya kuigizwa mbele ya watu. Ni mfululizo wa visa vinavyoweza kumhusu mtu yeyote. Visa mara nyingi huonyesha mambo ya ajabu na ya kawaida, ya ujasiri na ya woga na uzembe, yaliyompata mtu au watu katika hali na nyakati mbalimbali. Michezo inapoigizwa jukwaani mambo yafuatayo lazima yazingatiwe:

- i) Uangarifu wa kuchagua waigizaji wenye vipaji vya kuigiza mambo barabara na wanaofaa kuchukua nafasi za wahusika wa mchezo, watakaofaulu barabara, kuonyesha na kuhusisha wazo la mtunzi. Wahusika watakaoweka bayana wahusika wanaochorwa mchezoni hadi kufikisha mchezo kwenye kilele cha kuvutia watazamaji;
- ii) Uandalizi wa mandhari au jukwaa kulingana na tukio la mchezo ambao unadhihirisha wakati na mahali pa matukio na namna hali ya mambo ilivyo, kwa jumla matumizi bora ya jukwaa au uwanja wa maonyesho, ni lazima kuwa na matumizi ya taa, picha na pazia kama vinavyohitajika;
- iii) Uchaguzi wa mavazi na vyombo vya michezo;

- iv) Ufundi wa kuzungumza unajifanya tu, pia kutumia vyema ishara zitakiwazo;
- v) Ufundi wa kushirikisha na kuitazama hadhira wakati wote ingawa imetengwa na jukwaa.

c) Tofauti baina ya michezo ya fasihi simulizi na fasihi andishi

Michezo ya kuigiza ya kisasa au fasihi andishi ni yenye asili ya kigeni kwa mswahili ingawa ina athari za masimulizi ya ngoma ya kiasili. Miundo inaonekana kuwa ya tamthilia za mataifa ya kimagharibi.

- Utunzi wa maonyesho: mtunzi wa mchezo na muigizaji mara kwa mara ni watu tofauti. Maneno ya mtunzi sharti yakaririwe na waigizaji jinsi yalivyo au kama madokezo ya lazima hali kadhalika vitendo vyake. Katika maigizo ya fasihi simulizi, watunzi wa michezo ni hao wachezaji wenyewe. Maneno na vitendo ni vyao wenyewe tena vyabunuwa papo kwa papo.
- Maandalio: panatakiwa mazoezi mengi kabla ya kuonyesha michezo ya kuigiza hadharani. Jukwaa na vyombo maalum sharti viandaliwe. Baadhi na hivyo vyombo, ni lazima vikusanywe kutoka porini na vingine vinunuliwe madukani au viletwe kutoka majumbani. Kwenye maigizo ya fasihi simulizi kila mahali pafaa kuwe jukwaa, ardhi, vichakaa, n.k. yote yanafaa kuwa vyombo vya mchezo.
- Ushirikiano baina ya wachezaji na watazamaji ya michezo ya kuigiza. Kuna ushirikiano mdogo sana. Waigizaji au wachezaji ni wataalam pengine watu wa mshahara, wanajua yote kuhusu mchezo. Watazamaji ni watazamaji tu, wanatengwa mbali na jukwaa hata kwa pazia katika maigizo ya fasihi simulizi aghalabu wachezaji ndio watazamaji na watunzaji.
- Dhamira: mchezo wa kuigiza unaweza kutungwa na kundi kuhusu jumla lolote hata geni lisilohusiana na maisha ya hadhira na utamaduni wake, kumbe katika fasihi simulizi mambo yanayotendwa hutokana na maisha na hali halisi ya wachezaji wenyewe. Ni sehemu ya maisha yao halisi.
- Shabaha: shabaha kuu ya michezo ya kuigiza ni:
 - Kuwafundisha watazamaji mambo kwa kuona na kusikia bila ya kutenda wao wenyewe;

- Kufurahisha, kustarehesha na kuburudisha hadhira;
- Biashara, mara nyingi uigizaji hasa katika nchi za kibepari ni kazi ya mshahara. Kwa hiyo maonyesho ya michezo hutoza kuingilia.

Katika maigizo ya fasihi simulizi licha ya kuburudisha ni njia moja ya kulea motto na kujenga uzoefu wa kutenda mambo. Si kazi ya ujira.

- Mhusika mkuu: katika michezo ya kuigiza ya kizungu ya kale, mhusika mkuu kwa kawaida alikuwa ni mtu wa kutoka tabaka la juu, mwenyewe hushangaliwa au kusikitiwa na walio chini yake. Kumbe katika sanaa za maonyesho na michezo ya kuigiza ya Mswahili, mhusika mkuu anaweza kuwa mtu yeyote (katika fasihi simulizi ya Kiafrika, mhusika mkuu alikuwa mtu wa cheo, heshima, mwenye umri, mwenye ujuzi fulani wa kufundisha mambo walio chini yake).

d) Aina za michezo ya kuigiza

Kuna aina nyingi za tamthilia. Kuna tamthilia za mapenzi, za kihistoria, za kisiasa, za kidini, za kikabla, n.k.

Hizi zote huangukia katika moja ya makundi manne yafuatayo:

- i) Futahi:** futahi maana yake bahati njema na kufuatahi, kuondoa katika hatari shida, n.k.

Katika fasihi, michezo ya futahi ni ile ambayo visa, vituko na migogoro vinavyoelezwa humalizikia katika ushindi na furaha kwa mhusika mkuu na jamii anayowakilisha, pia na watazamaji wote. Pengine huitwa **tanzia-ramsa**.

- ii) Tanzia:** Tanzia maana yake tangazo la kifo, habari ya kifo. Michezo ya tanzia ni ile ambayo visa, vituko na migogoro yake huishia na masikitiko, maanguko na hasara au kifo cha mhusika mkuu na jamii. Watazamaji huachwa wanamuomboleza mhusika wao.

- iii) Yuga:** kuyugayuga maana yake ni kusitasita, kupepesuka. Michezo ya yuga ni ile ambayo ni wastani ya furaha na masikitiko kwa watazamaji wake. Shabaha ya michezo ya yuga hasa ni kutoa mafunzo bila ya mishtuko mikali pamoja na kutumbuiza kwa vichekesho.

iv) Ramsa: maana yake sherehe kama katika sikukuu. Katika fasihi michezo ya ramsa ni ile ambayo ina utani wa masahihisho au mraha na kejeli ya ukweli fulani wa maisha.

- **Ramsa za utani wa masahihisho**

Ili kumsahihisha mtu mkubwa kwa mfano mtawala, kiutani mwandishi hutumia mhusika huyu anayejiyonyesha kuwa mtu asiyejua mambo mengi na mwenye kutojali chochote, humzungumzia na kutenda mambo kiutani tu. Lakini kwa kweli katika matendo yake na vitendo vyake vya kiutani kuna mizaha yenye ukweli, majuto na maonyo mazito kwa mkubwa huyo anayehusika na aliyekusudiwa kukosolewa.

Mwenye kusemwa pengine huweza kuudhika sana. Lakini hathubuti kuonyesha hasara zake wazi, kwa hiyo anajikaza na kunyamaza. Na sababu yake ni kwamba watazamaji wote humchukulia huyo mchezaji kama bwegemtu. Na kwa mtu mkubwa aliye timamu kumkasirikia bwenge ni kujifedhehesha hadharani. Hivyo “bwengekiongo” huyo halaumiwi, bali hushangiliwa kila atokeapo kwa mizaha yake.

- **Ramsa za mzaha na kejeli**

Katika ramsa za mzaha na kejeli au dihaka mwandishi hueleza vipengele Fulani vya iimani au itikadi ya jamii kwa kutumia mifano inavyodhihirisha mambo na kwa jinsi ambayo inawafanya watazamaji waone mashaka juu ya ukweli na ujahilifu na dhima na imani na itikadi hizo. Mwisho wake watu hucheka na kuona kwamba jambo zima linalosaidiwa kuwa la msingi upuuzi. Mfano mzuri wa michezo ya aina hii ni “Aliyeonja pepo”.

UCHAMBUZI NA UHAKIKI WA MICHEZO YA KUIGIZA

Mambo muhimu ya kuangalia katika kuhakiki na kuchambua michezo ya kuigiza ni haya yafuatayo:

a) Maudhui: ujumbe wa dhamira za mwandishi wa tamthilia yaani yaliyomo, maadili, maonyo, mafunzo.

- Uhakika wa maudhui unataka kusoma na kuelewa habari nzima na kueleza kwa muhtasari.

- Kutambulisha dhamira au wazo kuu na michezo
- Kuonyesha msimamo wake na mtazamo wake.
- Kuchunguza falsafa ya maisha ambayo mwandishi anaieleza (hali halisi ya maisha).
- Kuainisha matatizo na migogoro iliyomo
- Kutambulisha mhusika mkuu kwa kuonyesha njia zilizotumika ili kumwima au kumwangusha huyo mhusika.
- Kuonyesha majibu ya juhudi zote za kukabili swala au tatizo linalozungumziwa.
- Kupima ikiwa mwandishi amefikia lengo lake.

b) Fani

Mambo yanayochunguzwa katika fani ni wahusika, muundo, mtindo, mandhari, lugha, kichwa na matukio ya mgogoro.

i) Wahusika: watu, wanyama, wadudu na viumbe wa kufikirika (majina, mazimwi) ambao wamechukua nafasi ya kuwakilisha jumua katika mchezo. Kuna wahusika wakuu na wahusika wadogo. Ni lazima kueleza jinsi wahusika walivyoundwa na wanavyojitokeza katika mchezo, uhusiano wao na namna wanavyoendelezana au kugongana kitabaka, kifikra, kiundani, kielimu, n.k. jinsi wanavyopokelewa na jamii yao au hadhira.

ii) Muundo: kipengele hiki kinachunguza jinsi mchezo ulivyotengenezwa.

- Mwanzo wa mchezo unasukumwa vipi na unakomea wapi? Kilele au upeo wa mchezo upo wapi na mwisho wake ni upi?

Kilele (upeo)hudhihirika mahali ambapo matukio yote yanapata suruhisho yake au hisia kunuliwa kabisa. Kilele cha tamthilia humfanya mtazamaji apate huruma na hofu na mwisho huwa na usuruhisho ambao hutuambia hali mpya ilivyo;

- Ni mchezo mmoja, miwili au zaidi inayoendelezwa katika mchezo ule ule. Muundo wa tamthilia unaweza kuwa mtiririko rahisi yaani mtiririko wa moja kwa moja usiokuwa na mchangamano wa visa. Unaweza kuwa mtiririko mgumu yaani

mtiririko wenye uchangamano wa vitushi. Upeo wake hutokana na maingiliano ya vitushi mbalimbali;

- Sehemu zake ni zipi, yaani mchezo una vitendo au sehemu ngapi na maonyesho mangapi?
- Ni maandhari gani yanasawiriwa katika mchezo.

iii) Mtindo: yaani “sanaa ya mtunzi”.

Tamthilia inaweza kuchukua mtindo wa ishara yaani huweza kuzungumzia kitu ambacho kinawakilisha kitu kingine.

Kwa mfano; Shetani kuwa mkoloni, inaweza kuwa katika hali halisi ya mambo. Tamthilia pia inaweza kutumia nyimbo kwa kuisisitiza ujumbe.

Ili kuchunguza sanaa na kufaulu kwa msanii katika utunzi wake sharti kuchunguza mambo yafuatayo:

- Lugha yake ikiwa ni fasaha, sahihi, kisarufi na kirahisi hueleweka na watu wengi;
- Viashiria au ishara na mifano iliyotumika kujenga wazo kuu, visa, mazingira ya wakati na mahali vinafungamana;
- Ukubwa wa hadhira au jamii inayoweza kufikiwa na ujumbe ikakolewa na kuvutiwa nao na kuathiriwa nao.

Je, semi na tamathali za usemi, nahau na metahali zinawiana na migogoro ya wahusika?
Je, migogoro yenyewe inasababishana?

iv) Kichwa cha mchezo

Kuhusu kichwa cha mchezo yafaa kujiuliza:

- Kichwa kinachowekwa ni wazo kuu au kiini cha habari?
- Ni wazo mojawapo linalojitokeza mchezoni?
- Ni neno tu la kuamsha udadisi wa msomaji na labda kuwavutia wanunuzi wa kitabu.

Mfano wa uchambuzi wa Tamthilia “HAWALA YA FEDHA”

Mwandishi: Amandina Lihamba

Hawala ya fedha ni tafsiri ya kitabu cha Sembene OUSMANE kinachoitwa “*Le Mandat*” (The money order katika lugha ya Kiingereza).

1. Mhutasari wa tamthilia “Hawala ya fedha”

Familia ya mzee Ibrahim CHANDE imetumiwa hawala ya fedha na mpwawe Abdul.

Huyu anasomea mjini Landani. Thamani ya hawala hiyo ni shilingi elfu mbili. Ibrahim CHANDE anapaswa kuchukua kiasi cha shilingi mia tatu, kumpatia mama yake Abdul mia tano na zinazobaki amwekee mpwa wake.

Hawala hii inaleta matumaini katika familia ya Ibrahim CHANDE, wanafikiri kwamba umasikini na njaa vimemalizika. Kwa kuwa wake zake CHANDE wamesomesha barua inayohusu hawala ya fedha, majirani wote wanajua habari hiyo.

Watu kadha wa kadha wanakuja kukopesha fedha na chakula kwenye familia hiyo. Wengine wanafuata Ibrahim CHANDE kila anapokwenda ili awasaidie kutokana na fedha hizo.

Inambidi Ibrahim CHANDE aende kubadilisha hawala yake kwenye posta. Anapofika anaombwa kuwa na kitambulisho lakini anakikosa. Hana kitambulisho chochote kila ila kadi ya chama isiyo na picha. Lazima aende kwenye kituo cha polisi.

Anapofika, anaelezwa kuwa hawezi kuwa na kitambulisho kama hana picha. Ibrahim CHANDE anamwendea AMBROZI ambaye anampiga picha. Anamwambia kurudi kesho yake baada ya kulipa shilingi thelathini. Lakini anaporudi huyu AMBROZI anamnyanganya picha pamoja na faranga zake.

Siyo hayo tu, bali anampiga vibaya pia. MBAYE anajitolea kumsaidia CHANDE kutoa fedha kwenye posta. Kwa upande mwingine, dada yake CHANDE, yaani Mama Abdul anakuja kudai faranga zake zilizoelzwa kwenye barua iliyokuja pamoja na hawala hiyo. Mzee huyo lazima auzishe herein za dhahabu za mkewe ili dada yake asiende mikono mitupu.

Ibrahim CHANDE hapumziki hata kidogo. Mwishowe, MBAYE aliyejidai kumsaidia anamwambia kuwa fedha alizichukua kutoka posta lakini akazinyanganywa na wizi akiwa njiani.

Matumaini yote ya Ibrahim CHANDE pamoja na wake zake yakafifia. Amne mke wake wa pili akaamua kwenda zake na Mama Dogo, mke wake wa kwanza akaenda kijijini kulima shamba.

2. Wahusika

a) Wahusika wakuu

Ibrahim CHANDE ndiye anakuwa mhusika mkuu katika tamthilia "*Hawala ya fedha*". Ana wake wawili: MAMA DOGO na AMNE. Habadiliki kitabia tangu mwanzo hadi mwisho wa mchezo, yeye ni mhusika bapa.

Ubapa wake unadhihirishwa na ujinga wake anaokumbana nao katika habari yote. Mhusika huyu hajui kusoma wala kuandika. Isitoshe, hataki pia wake zake wawe na kisomo (uk.4). kama inaruhusiwa katika dini ya Islam, Ibrahim CHANDE ana wake wawili. Katika usemi wake wote kuna rejesta ya dini. Pengine anaonekana akitoa sadaka kwa maskini, wengine anakataa kuwapa.

Isipokuwa ujinga wake wa kutojua kusoma na kuandika, mzee huyu anaonyesha moyo wa kusikiliza shida za watu wengine hasa hasa wale wanaotaka msaada kutoka kwake.

b) Wahusika wasaidizi

i) Mama Dogo: Huyu ni mke wake wa kwanza wa Ibrahim CHANDE. Yeye na Amne wake wenza. Hali yao ya uke wenza haiwatenganishi wala kuwafanya wachukuiane. Wanaonyesha ushirikiano tangu mwanzo hadi mwisho wa mchezo.

Mama Dogo anaonyesha busara katika maneno yake. Mfano bayana ni usemi wake unaokuwa kwenye ukurasa 41 (uk.41), pale ambapo anasema: "**Afugaye punda lazima ampendelee mlimaji nyasi.**"



Katika usemi huu alitaka kuonyesha namna ambavyo hakuna mtu pekee anayeweza kujitoshereza. Kama mtu ana duka, anategemea wale ambao wanakuja kununua vitu katika duka hilo. Kwa sababu hiyo, mtu yeyote anapaswa kutodharau mwenzake.

Kila wakati, Mama Dogo anaonekana akimtetea mumewe. Anaonekana akihangaishwa na usalama wa mumewe. Ili watu wasiendeleo kumfuata Ibrahim CHANDE kwa ajili ya fedha, yeye alibuni kisingizio na kuwaambia watu kuwa mume amenyanganywa fedha hizo (uk.36-38). “Alipopata pesa watu wakamvamia (uk.36)”. “Majangili ndugu yakamvamia. Hata senti moja si yake. Mungu na Mtume, sasa pesa zimekwenda na heshima yetu pia imekwenda.”

Pengine Mama Dogo anaonyesha imani katika Mungu. Anaamini kuwa Mwenyezi Mungu hasahau waamini wake (uk.1). yeye ndiye anaweza kunusuru maisha ya mtu aliye hatarini (uk.37).

ii) AMNE: Huyu ni mke wa pili wa Ibrahim CHANDE, yaani mke mwenza wa Mama Dogo. Tabia yake inaonyeshwa na ushirikiano anaokuwa nao kati yake na Mama Dogo mbele ya mume wao.

Amne ana tamaa ya kuwa na kisomo. Anamwona mumewe kama mjinga wakati wowote anapomzuia kwenda kusoma. Mwishoni mwa mchezo, anaonyesha tabia ya kutoweza kuvumilia hali ya umaskini na njaa inayojitokeza katika familia yake. Alipokata tamaa ya kupata fedha zilizokuwa kwenye hawala iliyotumwa na Abdul, yeye aliamua kumtoroka mumewe.

iii) Mbarka: Ni menye duka. Kutokana na mazingira au hali mbalimbali, yeye anabadilika kitabia. Wakati alipojua kuwa Ibrahim alikuwa na hawala ya fedha, alifurahi sana na kumkopa mchele bila wasiwasi.

Lakini alipopata habari kuwa pesa za Ibrahim zimeibiwa, alikasirika na kuanza kumdai kwa fadhaa. Mbarka anaonyesha tabia za uduara.

iv) Issa: Huyu ni rafiki Ibrahim CHANDE. Urafiki wao unatokana na kuwa Issa anataka sehemu ya fedha alizonazo Ibrahim. Yeye anaonyesha tabia ya unyonyaji.

Kila alipoongozana na Ibrahim wakienda mjini, alitaka Ibrahim amlipie basi. Unyonyaji wake unaonyeshwa pia na kunyang'anya watu akitumia ujanja (uk.16). yeye alikuwa anaganda kwenye Ibrahim kama rubu ama kupe wagandavyo kwenye ng'ombe.

v) Ambrozi: Ni mwenye studio. Yeye anaonyesha tabia ya kunyanyasa watu duni. Yeye ni mjangili: anachukua pesa za watu kwa bure na kuwadhulumu ili wasije wakamdai fedha zao. Lugha anayoitumia ni ya matusi.

Amandina Lihamba alitumia katika mchezo wake wahusika wengine wa aina mbalimbali ili kuonyesha hali halisi ya maisha. Mojawapo wa wahusika hao ni **bapa vielelezo**.

Majina yao yanaonyesha shughuli au tabia zao. Hao ni kama **mchuuzi, polisi, karani, maskini** na kadhalika. Mhusika **Abdul** ansimamia kundi la watu waliopata kisomo. Yeye anajua umuhimu wa kusoma, ndio sababu alienda Landani.

Vilevile anajua wazazi wanahitaji msaada kutoka kwa watoto wao wakati wakiwa na uwezo. Kwa sababu hiyo, alitumia mjomba wake pamoja na mama yake hawala ya fedha.

3. Mtindo

Mtindo ni kiwango cha lugha alichotumia mwandishi katika **Hawala ya fedha**.

Lugha inayotumiwa ni ya mazungumzo kwani kitabu hiki ni cha mchezo wa kuigiza, yaani tamthilia.

Vipengele vya lugha vilivyotumiwa na msanii ni tamathali za usemi, nahau, methali, misemo na rejesta. Pengine alitumia lugha ya kawaida, lugha inayoeleweka kwa wazungumzaji wengi wa lugha hiyo.

i) Tamathali za usemi

a) Sitiari: mifano,

- Umaskini bila nyumba ni kifo
- Madeni yatushika mpaka pwani
- Ndiye shetani mkubwa.

b) Tashibiha

- Kukusanyika kama sisimizi, (uk.3)
- Asiponilipa haraka nitamganda kama rubu, (uk.16)

ii) Methali

- Kutoa ni moyo si utajiri, (uk.13)
- Ulimi hauna mfupa: ulimi husema yote, yaani mazuri na mabaya.
- Dawa ya moto ni moto: kwa tatizo nzito lazima kauli nzito.

iii) Nahau

- Kutia chumvi,
- Chungu nzima,
- Kukata kauli,
- Kuwa na mkono mrefu (kuwa na huruma kwa kila mtu),
- Kuwa na mkono wa birika (kinyume na kuwa na mkono mrefu),
- Kukata tama,
- Kufariki dunia/kuaga dunia.

4. Muundo

Msanii alitumia muundo wa moja kwa moja, yaani hakufanya mazungumzo anayeweza kujitoshleza msomaji. Visa na matukio muhimu vya kuzingatia katika **Hawala ya fedha** ni hivi vifuatavyo:

- Taarifa inayomfikia Ibrahim CHANDE yenye ujumbe wa kupelekewa hawala ya fedha na kuwa postani.
- Tumaini la kuwa hawala ya fedha ingemwokoia toka hali yake ya umaskini,
- Kupanda kwa madeni,
- Harakati za kubadilisha hawala hiyo,
- Kupanda kwa tumaini la Ibrahim,
- Matumaini ya kupata vitambulisho,

- Kupatikana kwa fedha na kuibiwa kwake (**Upeo wa habari**),
- Kushuka chini kwa tumaini.

Msanii amefaulu kujenga kiini kimoja kutokana na mchanganyiko wa matukio mbalimbali.

5. Mandhari

Mandhari nayozungumziwa mchezoni ni halisi. Kama tulivyoielezwa na mwandishi, habari hii inatokea katika mji mdogo pwani mwa Afrika Mashariki.

6. Maudhui

Katika uchunguzi wa maudhui ya mchezo wa **Hawala ya fedha** tunachambua dhamira kuu pamoja na dhamira ndogo.

i) Dhamira kuu

a) Unyonyaji na kuharibika kwa urasimu

unyonyaji ni hali ya kutegemea wengine bila ya kufanya kazi; ni hali ya kuishi kwa jasho la mwingine.

Katika tamthilia **Hawala ya fedha**, unyonyaji unadhihirishwa na hasa hasa na majirani wa Ibrahim CHANDE wanaotaka awasaidie kwa kila hali baada ya kupata habari kuwa ametumiwa hawala ya fedha.

Kuna wanaotaka awakopeshe mchele na wengine fedha kiasi kwamba angetimiza hoja zao angebaki mikono mitupu. Mhusika anayeonekana kuwa mnyonyaji kuliko wengine ni ISSA. Huyu anamsindikiza Ibrahim CHANDE katika harakati za kubadilisha hawala ya ili apate fedha. Kila wanapoenda, ISSA anataka Ibrahim amlipie basi.

Si hayo tu, anataka ampatie fedha za kutumia katika shughuli mbalimbali. Watu wengine wanadhihirisha unyonyaji ni msichana aliyekutana na Ibrahim CHANDE akimuomba msaada kwa mara nyingi.

Pengine ni Ambrozi, aliyemnyanganya pesa zake alipoenda kujipigisha picha. Mhusika mwingine ni MBAYE aliyefaidi hawala isiyokuwa yake.



Kwa upande mwingine kuna katika mchezo huu, hali ya kuharibika kwa **urasimu**. Ijulikane kuwa urasimu ni utaratibu wa kuendesha kazi za kiofisi kulingana na kanuni za kiutawala.

Katika mchezo (tamthilia) **Hawala ya fedha** kuharibika kwa urasimu kunatambulika kutokana na viongozi (makarani).

Hawa hawafanyi kazi yao kama ilivyo. Hawakutaka kuendesha haraka mambo ya hawala ya fedha ya Ibrahim ili yeye awapatie rushwa.

b) Ujinga

Katika kitabu cha Amandina LIHAMBA, ujinga unatokana na tabia ya Ibrahim: kutojua kusoma, kukosa vitambulisho ambavyo ni mambo muhimu ya raia.

Kwa ajili ya kutojua, ilimbidhi Ibrahim kusomesha barua yake iliyohusu Hawala ya fedha. Habari hiyo ilipaswa kuwa siri lakini ilisambaa katika kijiji kizima kutokana na kuwa barua imesomeshwa.

ii) Dhamira ndogo

- Mvutano baina ya vizazi (vijana mbele ya wazazi)

Mvutano baina ya vizazi unaelezwa na msichana mmoja aliyetukana Ibrahim baada ya kujionyesha mbele yake akitaka msaada na kunyimwa. Matusi yake yalienda pamoja na kumsingizia kuwa alitaka kumtongoza.

Mvutano unaonekana pia kutokana na tabia ya Ambrozi aliyempiga Ibrahim badala ya kumpa picha zake. Alionyesha dharau kubwa mbele yake mzee.

- Nafasi ya mwanamke katika jamii

Katika nchi nyingi za Afrika, mwanamke huonekana kama kiumbe duni. Mambo yanayokuwa vilevile katika **Hawala ya fedha**. Ibrahim anaonyesha dharau lakini wanawake hawa wanaonekana kuwa washauri wa nafasi ya kwanza wa mume wao.

AMNE anaonekana kujikomboa kutoka dharau hiyo. Katika kitabu hiki, wanawake wengine huonekana wakitaka kusitisha mambo ya rushwa.

- Nafasi ya fedha katika maisha ya kila siku

Dhamira hii inajidhirisha katika matukio mengi ya habari hii. Kusomesha barua lazima fedha, kutafuta vitambulisho ni fedha, picha, chakula, safari katika basi ni mambo hayo hayo. Inadhirika kuwa watu wote wametekwa na tamaa ya fedha ili waweze kufanya shughuli zao mbalimbali.

Mfano wa watu wanaotamani fedha kuliko wengine ni ISSA. Huyu anatumia hila ili aweze kuzipata.

MAZOEZI

1. Tamthilia huandikwa kwa madhumuni gani?
2. Taja aina za tamthilia unazozifahamu. Kwa kila aina, tolea mifano kutoka tamthilia za Kinyarwanda.
3. Tanzania ni tamthilia ya aina gani?
4. Nini tofauti ya ramsa na Tanzania ramsa?
5. Migogoro ina umuhimu gani katika tamthilia?
6. Tamthilia inatofautianaje na Riwaya?

1.2.4. USHAIRI

1.2.4.1. Maana ya ushairi

Ushairi ni sanaa ya lugha inayoeleza jambo au wazo kwa njia ya mkato, kwa namna inayoteka (kuchukua hisia za msomaji au msikilizaji).

Maneno ya mashairi huundwa kimaksudi ili yaletе picha maalumu akilini mwa msomaji au msikilizaji. Maneno hayo hupangwa pia ili yatoe mdundo fulani shairi linapoimbwa, linaposemwa, linapoghamiwa au linaposomwa. Ushairi unaweza kumfanya mtu ahisi uchungu au furaha, hasira au ridhaa; waweza kumburudisha mtu hadi moyo wake utulie ama kumhamasisha hali, kama yafanyayo mashairi mengi ya ukombozi.

Ushairi ni chombo cha kueleza maisha ya kila siku kuzidi kazi za mashairi na tamthilia. Hueleza maisha kwa sanaa ya juu ya lugha. Ni usemi wenye utamu sana kwa sababu ya mapingo na midundo yake ya kuisisimua. Licha ya kustarehesha na kukosoa, ushairi huadili, hujadili mazingira, hutoa fikra na busara, hujigamba na msiba, mapenzi, machukivu, maoneva, na hisia zote alizo nazo binadamu.

1.2.4.2. Asili ya ushairi

Ushairi ndio utanzu wa fasihi ulio mkongwe zaidi katika jamii za kilimwengu. Ulianza wakati binadamu alipobuni lugha. Kubuniwa kwa lugha kulipanua uwezekano wa binadamu kujielewa, kuelewa mazingira yake, na kujihani (kujilinda, kujitunza) kutokana na maadui wake. Njia mojawapo iliyotumika kuyamiliki mazingira na kuyatumia kwa manufaa ya binadamu. Ni kufanya kazi na hivyo kuzalisha mali. Ushairi kama ulivyojibainisha katika nyimbo zilimpa nguvu na kumhimiza mfanyakazi ajitahidi, hata kama kazi ni ngumu namna gani.

1.2.4.3. Umbo la ushairi

Umbo la ushairi unaweza kujitokeza kwa njia tofauti. Kwa mujibu wa wanamapokezi ambao wanakili kuwa lazima ushairi ufuate urari fulani (au sheria fulani). Umbo la shairi sharti lionyeshe beti, mishororo, mizani, vituo na hata ujitoshereze. Kwa upande wa wanamabadiliko (wa mapinduzi) ambao wanatetea kuwa na uhuru katika usanifu wa mashairi, kanuni hizo sizo za lazima kwani badala ya kurutubisha uwanja wa ushairi unauponza.

- a) **Ubeti (beti):** mgawanyo wa shairi au utunzi katika idadi ya mistari (mishororo) inayolingana.
- b) **Mishororo (mistari):** unaweza kuwa wa kipande kimoja au wa vipande viwili.
- c) **Mizani:** idadi sawa ya silabi katika kila mishororo ubeti hadi ubeti.
- d) **Vina:** hii ni miisho iliyo sawa yaani silabi za sauti zile zile zilizoko mwishoni mwa maneno. Kuna vina vya kati na vina vya mwisho.
- e) **Kituo:** huu ni msitari wa mwisho wa ubeti. Vituo ni vya aina tatu:
 - **Kituo bahari:** huu nimstari unaotokea mwishoni mwa kila ubeti ambao haubadiliki (kibwagizo).

- **Kituo nusu bahari au nusu kimalizio:** ni mstari wa mwisho ambao maneno yake nusu hubadilika na nusu hubaki yale yale ubeti hadi ubeti.
- **Kituo kimalizio:** huu nimstari wa mwisho ambao maneno yake ni tofauti ubeti hadi ubeti.

f) **Kujitoshereza:** katika mashairi kila mstari hupaswa kuwa kamili, aidha kila mstari uwe tungo kamili lakini ni lazima kila ubeti uwe na maana kamili, na usiogope kutimizwa na ubeti mwingine ufuatao.

1.2.4.4. Aina za ushairi

Kwa kawaida kuna aina mbili kubwa za ushairi, yaani ushairi unaofuata **urari wa mizani** ambao unazingatia **shairi, utenzi na ngonjera**. Kuna ushairi unaokireka sheria hizo za usanifu ambao huitwa **zuhari** au **ushairi huru**. Lakini kunaweza kujibainisha aina mbalimbali kufuatana na mishororo iliyopo katika beti.

1.2.4.4.1. Shairi

Shairi ni mojawapo wa tungo za ushairi ambao kwa kawaida si mrefu. Beti hujigawa katika mistari. Kila mstari una vipande viwili. Huwa na vina vya kati na vina vya mwisho. Shairi linaweza kuwa na mizani mingi.

Utungo huu ukiwa na mishororo mine unaitwa **tarbia**, ukuwa na mitano unaitwa **takhmisa**, ukiwa na mistari mitatu unaitwa **tathlitha**.

Mifano 1:

Siku moja itafika, katika hii dunia,

Itapozuka fanaka, kupotea kwa balia,

Hakiitakaposhika, batili kuangamia.

. **ka, ka, ka** ni vina vya kati, wakati **ia, ia, ia** ni vina vya mwisho.

. Mizani ni sawa na kumi na sita (16).

Mfano 2:

Uhuru utapodumu, sio ule wa bandia,

Tasitawi mwanadamu, kila atajifanyia,

Utakwenda udhalimu, kata hautarejea.

(Kutoka Sikate Tamaa na Said A. Mohamed. Nairobi, Longman, 1960: uk. 25).

Kina cha kati katika ubeti huu ni **-mu** na kina cha mwisho ni **-ia**.

Mfano 3:

Niwapo mestakimu, kwa unyonge wa mashaka,

Naishini madhulumu, kwa janila ukoka,

Apatapo mwanadamu, atimba akitimbika,

Madamu sitakimu, huona sina hisia.

(Kutoka Sikate Tamaa, uk. 45).

Kina cha kati ni kimoja, cha mwisho kinabadilika kwenye mshororo wa mwisho.

Mfano 4:

Watu walomba, zana za zamani,

Na nyimbo huiмба, za nyingi maani,

Hewe kosa kwamba, jeuri kulani,

Kungawana sambe, ni jadi kubeli.

Mizani ni sita kwa sita. Kina cha kati ni **-мба** na kina cha mwisho ni **-ni** isipokuwa kwenye mshororo wa mwisho.

Mfano wa shairi na uchambuzi wake

Semani Wenye Kusema

Muko wapi wenye ndimi, zenye makali ya wembe?

Mbona leo hamusemi, mu kimya kama mapumbe?

Mwangoja yatimu kumi, halafu ndipo mulumbe?

Musijifanye migombe, semani wenye kusema.
Ni mawi yaliyotuka, “ni ya hi utu” musambe
Ni yupi mwenye kutaka, kama hayo yamkumbe?
Hao yaliwowafika, ni kama mefumwa chembe
Musijifanye migombe, semani wenye kusema.
Uwovu kiwa kwa watu, ijapokuwa u tembe
Utaona kila mtu, yu mbiyoni akaimbe
Mbona leo u kwetu, twaambizana tusambe?
Msijifanye migombe, semani wenye kusema.
La damu kutanganyana, za tafauti viumbe
Ni hatua njema sana, watakayo wenye pembe
Pasi kukubaliana, haifuzu hata pembe
Msijifanye migombe, semani wenye kusema.
Engani yatendekayo, mato yenu msifumbe
Kisikizeni kiliyo, waliyao ni viumbe
Yapimeni yasemwayo, musimili moja pembe
Msijifanye migombe, semani wenye kusema.
Lavuja paa la nyumba, wavimbaji nawavimbe
Na klia mlima shamba, natiye mpini jembe
Na wale waliyo samba, leo wangurume jumbe
Msijifanye migombe, semani wenye kusema.



Uchambuzi wa jumla wa Shairi hili

1. Muundo wa shairi hili:

Shairi hili lina beti sita (6). Kila ubeti una mishororo minne. Kama mashairi yanavyotungwa, shairi hili lina vina vya kati na vina vya mwisho.

i) Mizani: Shairi hili lina mizani kumi na sita. Nane upande wa ukwapi na nane upande wa uketo.

Mfano:

Mu|ko| wa|pi| we|nye| ndi|mi|, ze|nye| ma|ka|li| ya| we|mbe|?

1 2 3 4 5 6 7 8 1 2 3 4 5 6 7 8

La |da|mu| ku|ta|nga|nya|na|, za| ta|fa|u|ti| vi|u|mbe|

1 2 3 4 5 6 7 8 1 2 3 4 5 6 7 8

ii) Vina: kuna sauti (silabi) za mstari za kati na za mwisho ambazo zinafanana. Silabi hizo ndizo huitwa vina. Kuna vina vya kati na vina vya mwisho.

Mfano:

Uwovu kiwa kwa watu, ijapokuwa u tembe


Utaona kila mtu, yu mbiyoni akaimbe

Mbona leo u kwetu, twaambizana tusambe?

Msijifanye migombe, semani wenye kusema.

iii) Kituo: mstari wa mwisho wa ubeti ambao ni tofauti na mistari inayotangulia na unaomalizia beti zote za shairi ndio huitwa **kituo**. Kama ni ule ule unaomalizia beti zote, ni **kituo kibwagizo**. Katika shairi hili ni kituo kibwagizo (bahari) kilichotumiwa mwishoni mwa kila beti.

Mfano: “**Msijifanye migombe, semani wenye kusema**”.



2. Tamathali za usemi

Katika shairi hili msanii alitumia tamathali za usemi mbalimbali kama tashbiha, sitiari, tashihisi, takriri.

a) Mshairi alitumia **sitiari** katika mshororo ambamo anasema:

- Muko wapi wenye ndimi, zenye **makali ya wembe?**
- Na wale waliyo **simba, leo wangurume jumbe**
- Msijifanye **migombe**, semani wenye kusema.

b) Mshairi pia alitumia **tashbiha** katikabeti zifuatazo:

Beti la kwanza

- Mbona leo hamsemi, mu kimya **kama** mapumbe

Beti la pili

- Hayo yaliwowafika, ni **kama** mefumwa chembe

c) Mshairi alitumia **takriri silabi "ni"** katika beti la pili, la nne, la tano na **"na"** katika beti la sita.

- **Ni** mawi yaliyotuka, **ni** ya ki utu msambe
- **Ni** yupi mwenye kutaka, kama hayo yamkumbe?
- **Na** kila mlima shamba, **natiye** mpini jembe
- **Na** wale waliyo simba, leo wangurume jumbe

d) **Kejeli** ilitumiwa sana sana katika shairi lote hasa hasa katika kituo bahari ambacho kinasema **"Msijifanye migombe, semani wenye kusema"**.

e) Msanii alitumia pia **chuku** katika shairi lake hasa hasa katika beti la sita anaposema **"Lavuja paa la nyumba, wavimbaji na wavimbe**

Na kila mlima shamba, natiye mpini jembe

Na wale waliyo simba, leo wangurume jumbe"



Katika sentensi zilizoandikwa kwa rangi iliyokoza, msanii anapiga chuku kwa kueleza fikra zake.

3. Mpangilio wa maneno

Hapa msanii alitumia lugha ya mkato, na kupanga maneno katika mpangilio wa kiima, kiarifu na shamrishi. Pia msanii alitumia mpangilio wa kuuliza maswali.

Mfano:

Ni mawi yaliyotuka, ni ya ki utu musambe

Mbona leo u kwetu, twaambizana tusambe?

Muko wapi wenye ndimi, zenye makali ya wembe?

4. Matumizi ya picha

Katika shairi hili, msanii anachora picha kwa uteuzi mzuri wa maneno ambayo yanatoa picha katika mawazo ya msemaji, anauliza maswali na kutumia maneno ambayo yanaonyesha kuwa anakasirika sana kuhusu wanavyosema. Mshairi anaonekana kuwa mwenye hasira kubwa.

Mfano:

Mwangoja yatimu kuni, halafu ndipo mulumbe

Kisikizeni kiliyo, waliyao ni viumbe.

5. Takriri na ridhimu

Kama vilivyosemwa hapo juu, msanii alitumia takriri na ridhimu kwa kuisitiza ujumbe uliotajwa.

Anatumia hasa hasa “**ni**” na ridhimu ambayo inaathiri mawazo na hisia za msomaji.

Katika kuchora hisia, msanii alitumia tamthali za usemi **takriri** na **ridhimu** kwa kuchora picha au taswira ya masikitiko yake katika fikra za wasomaji.

6. Maudhui na dhamira

Shairi hili linasimulia kuhusu upinzani wa msanii na watu wengine. Linaonyesha ujasiri wa msanii, imani yake na matumaini yake makubwa juu ya haki.

Msanii huyu anapigania ukweli. Shairi hili linaonyesha unyanyaswaji wa wanyonge na ukali wa msanii katika harakati za kuwakomboa.

i) Dhamira kuu

- **Matumaini ya kushinda:** msanii anawaita wapinzani wake waje waseme yanayomhusu. Anawahimiza kutokuwa na woga anaposema

“Muko wapi wenye ndimi zenye makali ya wembe?”

Mbona leo hamsemi, mu kimya kama mapumbe?”

Dhamira kuu nyingine ambayo inaweza kuonekana hasa ni **vita baina ya ukweli na uongo**. Mwandishi anaonekana kuwa anataka kuonyesha ukweli wake kwa waliomsema vibaya. Kuna pia vita baina ya haki na dhuluma.

Mfano:

- Engani yatendekayo, mato yenu musifumbe
- Kisikizeni kiliyo, waliyao ni viumbe.

7. Hisia za kishairi

Hisia hizi zinaonyeshwa katika mpangilio wa maneno, picha, sauti na ridhimu pamoja na tamathali za usemi alizotumia.

Hisi inayozushwa na msanii ni kudharau watu ambao wanamsema mabaya, chuki nyingi kwa waongo.

1.2.4.4.2. Utenzi au utendi

Utenzi ni utungo mrefu wa kishairi unaoeleza kihistoria au kisa fulani ambao hauna vina vya kati katika mistari yake, bali kila ubeti una vina vya namna moja katika kila ubeti. Kina hicho kinachorudiwa rudiwa katika kila ubeti wa utenzi chaitwa **bahari**.



Tenzi nyingi husimulia visa virefu vya kihistoria kama utenzi wa vita Mau Mau, hadithi au mawaidha marefu kama ***Utenzi wa Mwanakupona***.

Kwa sababu ya uzito wa yale ambayo tenzi huelezea, kwa kawaida tenzi nyingi huanza na dua. Mwandishi humuomba Mola amwongoze katika uandishi wake. Tungo za utenzi huwa ndefu yaani huwa na beti nyingi kuliko shairi. Zaweza hata kuzidi mia tatu (300) kufuatana na uzito wa maudhui na ubingwa wa utenzi wakati ambapo beti zake zavuka ishirini. Utenzi una mizani mifupi isiyoziidi kumi na moja, mara nyingi huwa nane katika kila mshororo au mstari ingawa kuna nyingine ambayo huwa na mizani mingi au chache ya hapo. Mstari wa utenzi una kipande kimoja tofauti na mstari wa shairi ambao una vipande viwili. Ubeti wa tenzi huwa na mistari minne.

Mifano:

1. ***“Utenzi wa Hidaya”*** kutoka ***Sheria za kutunga mashairi na Diwani ya Amri***, Kaluta Amri Abedi, Nairobi, Kenya Litoretture Bureau 1991.

- a) Kwa Mola nakimbilia, utuongoze na njia,
Nijilinde na madhia, ilinyooka sawia,
Moyoni mpulizia, iliyopita manabia,
Shaitani rajimia, na walowafuasia.
- b) Bismillahi naanza, kovu umeshitadi,
Rahamani reHEMEZA, umepitiliza hadi,
Rahimini mjaliliza, kuusema sina budi,
Si feza mdajalia, ili yapate elea.
- c) Tunakuabudu wewe, mbinu zote zinalia,
Msaada tupe wewe, imani imepotea,
Maisha tudumu nawe, ardhi yaitikia,
Tuwe tukinyenyekea, yamezidi maasia.

2. *“Utenzi Twamkumbuka Kenyatta”* uliomo katika *Mashairi yetu* kilichohaririwa na Khan.

Natarabuku na dua, twafia tukidadisi,
 Naombea mwenye dua, tukumbukapo jinsi,
 Rais mwenye murua, alivyotenda Rais,
 Peponi kukaribia, siwezi kusimulia.
 Mola umueke pema, ninachukua fursa,
 Akae na kujerema, wasomi niwape kisa,
 Dasi hofu humwangama, alivyoanza siasa,
 Wala taabu na udhia, uhuru kugombania.

1.2.4.4.3. Ngonjera

Ni aina ya ushairi ambapo twakuta mahojiano na malumbano kati ya watu wa pande mbili. Yaweza kuwa baina ya mtu na mtu, au na watu na watu. Jambo kubwa kabisa katika ngonjera ni kwamba zenyewe husemwa haziimbwi. Tofauti na mashairi ya kawaida huwa na wahusika ambao hushika nafasi. Mara nyingi huwa na mhusika mjuaji, mwerevu. Kazi yake ni kumwelimisha mdadasi kukili kwamba amepambanuliwa na kuelewa jambo hilo. Maudhui yake huweza kuwa ya kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni kwa ujumla.

Utoaji wa ngonjera, hutumia vitabia yaani wahusika hutumia mikono, macho, modomo, mabega na viungo vingine vya mwili. Mhusika anakonyeza kufanya ishara kwa kusisitiza ujumbe. Hali kadhalika penye mshangao, mhusika huweza kutumbua macho na kuachama mdomo kama ishara ya kupigwa na bumbuazi, n.k. Uhai wa ngonjera hutokana na sifa hii ya utumiaji wa vitabia.

Mfano:

Kaka: Kusoma nilikosoma, kambiwa sipati kazi

Yapata mwaka mzima, nategemea shangazi

Wasiojua kusema“Sababu sina ujuzi”

Huna uhaba wa kazi, husababishwa na wake.

Dada: Mbona wataingilia, kaka acha ubaguzi

Likulerele twambia, tulijue waziwazi

Au unachochukia, ni wake kufanya kazi

Mambo ya kisiku hizi, watu ni bega kwa bega.

Kaka: Siwangilia kwa nini, nanyi mwatukopa kazi?

Kwani tokea zamani, hazikuwa shida hizi

Mtu kutoka shuleni, kibarua si tatizo

Leo hatupati kazi, kisa nyingi wanawake.

Dada: Hapo hujisema kuwa wake ndio chanzo chanzo cha hii

Na kama wanaume hukosa kazi,

Mtindo wa siku hizi Watu ni bega kwa bega

Kutoka Malenga wa Umba, Boukhest, Amana, Nairobi Oxford University Press, 1982, Uk 42-43.

Tanbihi: Kuna aina nyingine za mashairi lakini yasiyo na vipengele vya nje (fani) kama vina ambavyo huvitofautisha na mengine. Aina hizo ni kama:

- **Zivindo:** ni tungo ambazo kazi zake ni kufunza lugha aghalabu kwa kutoa maana tofauti ya neno moja au maneno yenye matashi yaliyokaribiana. Kwa mfano mshairi anaweza kuchukua neno “**paa**” au akasuka maana zake tofauti katika shairi.

Mfano: Mdudu

Kaa ni kusema kama, na mwaliko ni kaa

Kaa (kukaa) alosimama, wamweleze kukaa

Kaa ni lililozima, na lililo moto ni kaa

Moto uliozima, mwenye ya tano yafaa,

Anene ni kaa gani?

Kutoka Malenga wa Mista: Diwani ya Ustadh Bhalo, Ahmed Nasir.

- **Tumbuizo:** ni shairi ambalo haligawanyiki kwa ubeti lakini ni mistari mingi iliyowekwa pamoja na yenye vina na mizani linganifu. Ni tungo ambazo ni za makusudi ya kuimbwa kwani huwezi kutumbuiza bila kuimba. Mahali maarufu ambapo tumbuizo huimbwa huwa hasa katika hadhira za harusi. Tumbuizo huimbwa zikifuatishwa na Vugo(pembe za ng'ombe ambazo zilizotumbuliwa tundu) na kutiwa vibamba(bati au vikengele na hivi hupigwa kwa vigongo vifupi).

Maudhui ya tungo hizi huwa ni ya **kuomboleza, kutumbuiza, kulalanikia au kubembeleza watoto**. Wakati mwingine tumbuizo huimbwa katika ngoma iitwayo **gungu** (ni ngoma inayopigwa katika harusi au wakati wa kufunga au kuanza mwaka). Utumbuizo maarufu uimbwao katika mkusanyiko wowote wa gungu ni ule unaosemekana kuwa umeimbwa na Fumo Liyongo.

Fumo Liyongo ni shujaa maarufu wa Kiswahili aliyeishi baina ya 1160-1204. Aliuimba utumbuizo huu alipokuwa amefungwa gerezani akingojea hukumunyake ya kifo. Aliuimba utumbuizo huu ili kumtuma msichana aliyekuwa amekuja kumpelekea chakula gerezani ili aende akamwambie mama yake Liyongo amletee tupa akelezee minyororo iliyomfunga ili apate kutoloka. Utumbuizo mwenyewe unaitwa "**Kijakazi sada**".

Mwanzo wa utumbuizo huu ni huu ufuatao:

Kijakazi sada nakutuma hujatumika

Kamwambie mama ni mjinga hajalimka

Apike mkate pale tupa kaweka

Nikereze pingu na minyoo ikinemka

Nipande madari na makuta yakibomoka

Niingie shakani ningurume ja samba

Niingie ondoni nitambae ja mwana nyoka

Nipige miremba muimao kuuandika

Niwe kati mwao kiwegema wakinepuka

Niingie mjini wake na mama wake mateka

Nail mti pweke nimeziye katika nyika

Si nduu si mbasi nimeziye kukupuka

Kazi ya utumbuizo pia ni kutoa hisia za ndani zilizombana mtu, na huimbwa kwa sauti maaalumumu laini na yenye kuvutia pumzi, kwa kipimo. Mtoto anaweza kutumbuiza alale. Sauti ya shairi kama hili ni ya kutuliza (Ibihozo).

Kwa mfano:

Silie mama silie

Ukulia waniliza

Wanikumbusha makiwa

Baba na mama watende

Waniozea dume kongwe

Halisafiri hutendi

Kazi kumega matonge (melodie).

Papo tumbuizo zina mahadhi, si lazima ziwe na mizani wala vina.

1.2.4.4.4. Zuhali

Baadhi ya wanafasihi huita fani hii ya ushairi mashairi kisiasa, mashairi huru au mashairi ya kienyeji, na wengine mashairi guni. Zuhali siyo fani mpya.

Zuhali zimetungwa tangu zamani, na zinaweza kusemwa. Ni maendeleo ya nyimbo za makabila zilizomo katika fasihi simulizi. Kwa makundi zuhali hazina urari ule wa kimapokeo unaotawala katika mashairi na tenzi. Na hivi si tungo shairi guni kwa

mfano hazivunji kanuni fulani za ushairi kwa sababu ya kushindwa kuzifuata. Zuhali huunda fani yake pekee. Mawazo yaliyomo katika zuhali hutiririka mstari hadi mstari mwanzo hadi mwisho. Zuhali zina utenzi wa maneno na mpangilio wa maneno kishairi kabisa, ingawa hazidai **vina** na **mizani**.

MAZOEZI

1. Kuna tofauti gani kati ya mashairi na tenzi?
2. Lugha ya ushairi ni lugha ya namna gani?
3. Matumizi ya vitabia katika ngonjera husaidia nini?
4. Je, katika jamii ya Wanyarwanda kuna utungo wa ngonjera?
5. Utungo wa utenzi huwa mrefu kwa sababu gani?

1.2.4.4.5 Majigambo

Majigambo ni utanzu wa fasihi simulizi ambayo yana uhusiano wa karibu na mashairi. Dhana ya kujisifu ndiyo ambayo huwa dhamira kuu ya majigambo. Shairi la majigambo ni shairi la kujikweza na kujisifu. Washairi wa kizamani na hata wa kisasa wamekuwa wakijipa lakabu au majina ya kishairi. Dhana ya kujisifu huwakilishwa kwa vitenzi vingi sana tofauti. Aidha, karibu vitenzi vyote ni vitenzi jirejee, yaani vina kiwakilishi jirejee **-ji-**.

Vitenzi hivyo ni kama vifuatavyo: kujigamba (kujifanya unajua sana); kujinaki (kujitangazia sifa, kujitakasa, kuwa huna makosa); kujinata (kujiona bora kuliko watu wengine); kujitwaza (kujinata); kujiketua (kujifanya kuwa na mambo usiyokuwa nayo); kujivuna (kuhisi kuwa u zaidi kuliko wengine, kuringa); kuringa (kujiona bora kuliko watu wengine; kuwa na kiburi; kujiona); kudesha (kujionyesha kwa watu kwa kitu ulicho nacho; kutia mikogo, kuringa); kujifutua; kujifaragua; kujibodoa; kujikita; kujisifu; kujitapa; kujiona; kujisikia; kujitutumua; kujitukuza; kujikweza, kujinadi; kujipambanua.

Kuhusiana na fasili kutoka Kamusi ya Kiswahili Sanifu (KKS: 1981), *kujigamba ni kujifanya unajua sana; kujifutua; kujisifu; kujifaragua; kujikita; kujinadi; kujibodoa;*



kujivuna; kujinaki. Fasili hii siyo inayojitokeza katika uchambuzi wa mashairi yaitwayo **majigambo**, maelezo yake ni potofu kufuatana na muktadha wa fasihi yenyewe

Kuhusiana na fasili ya Kamusi ya Kiswahili Sanifu, kujigamba huonekana kama tabia mbaya ya kuwaudhi watu wengine na kwa hiyo huhistahili kulaumiwa. Majigambo ni kinyume cha majisifu au majivuno. Nayo ni sanaa muhimu katika fasihi simulizi ya Kiafrika ambayo pamoja na kutungwa kwa ufundi mkubwa, humsaidia mtu binafsi au kundi la watu kujipa moyo na kujipatia nguvu.

Mjigambi halisi si mtu wa kawaida anayejifanya anajua sana, bali ni mwanasanaa ambaye bila shaka, kwanza ni mshairi na pili anajua kwa undani jambo analoliongelea.

Imebainika kwamba majigambo huwa yamehimiliwa ya kijamii na kitamaduni ambayo yalirutubisha na kuzalisha majigambo. Imebainika pia kwamba majigambo huwa yamehimiliwa na utamaduni fulani, amali fulani, mfumo fulani wa kiuchumi, na mazingira fulani. Sura hii imeonyesha kuwa majigambo ni zao la mazingira pamoja na mikakati ya binadamu ya kuhimili maisha. Majigambo huwa na utendaji na hutokea palipo mziki.

Kwa kawaida majigambo hutungwa na kuimbwa na mhusika mwenyewe. Majimbo hutungwa kwa ufundi mkubwa, kwa kutumia mbinu kama takriri, sitiari, ishara, vidokezi, na wakati mwingine vina. Mjigambaji ambaye kwa kawaida ni mme hujitungia shairi lake kufuatia au kufungamana na tukio maalumu katika maisha yake, kwa mfano kuoa, kushinda jambo gumu (kama vile myama mkali, mchezo, kesi mahakamani, masomo, n.k), kuingia jandoni, kurejea kutoka vitani.

Baadhi ya majigambo huwa ni marefu sana na yenye masimulizi ndani yake lakini mengi ni mafupi. Majigambo mengi hueleweka kwa urahisi kwa hadhira iliyokusudiwa, kwa vile huzungumzia mambo wanayoyafahamu au waliyoyashuhudia. Wale wasiohusika hupata taabu kuyaelewa, hasa kama hawaifahamu vizuri historia ya mtunzi.

Majigambo kwa asili hayaandikwi, hutungwa papo kwa papo, lakini siku hizi baadhi ya watu wameanza kuyatunga kwa kuandika, na harafu huyasoma au kusomwa wakati wa sherehe inayohusika kama vile harusi.



Muundo wa majigambo

Muundo wa majigambo hutegemea shabaha za mtunzi na jadi ya mtunzi anayoiwakilisha. Kwa mfano, kivugo aghalabu hupaswa kuwa na mambo yafuatayo:

- ✓ Jina halisi na/au jina la sifa la mhusika;
- ✓ Sifa za nasaba yake ya kuumeni;
- ✓ Sifa za nasaba yake ya kuukeni;
- ✓ Maelezo ya matendo matukufu aliyoyafanya;
- ✓ Ahadi za kutenda makubwa zaidi kwa ajili ya mkubwa wake(mzazi, mtawala, n.k);
- ✓ Tamati: “kujikabidhi “rasmi kwa mkubwa.

Washiriki katika Majigambo

Siku hizi majigambo hufanywa mara nyingi sehemu za vijijini wakati wa sherehe za harusi au hufanywa na wanafunzi wa shule za msingi wakati wa sherehe za kiserikali. Mengine hufanywa na waimbaji kama wapiga zeze, nanga, wacheza ngoma za kienyeji, au na watu binafsi bila ya kuzingatia sababu maalumu, k.m. wakati wa vinywaji, michezo, n.k.

Kuna pia majigambo ya wakati wa sherehe ya harusi ambayo hufanyika baada ya Bwana harusi kufunga ndoa na kujamiana na mkewe, ambapo huwa amethibitisha uume wake.

Wakati wa sherehe hiyo msimamizi au shahidi wa bwana harusi au mtu yeyote Yule aliyeteuliwa na kamati ya wazee kutoka upande wa bwana harusi ndiye anayeweza kujigamba kwa niaba ya bwana harusi. Wakati mwingine bwana harusi mwenyewe anaweza kujigamba kama ilivyokuwa zamani, ingawa inakuwa sio rahisi kwani shughuli yenyewe inahitaji mtu ambaye ni mkakavu na msemji sana, kitu ambacho kinaweza kumshushia hadhi bwana harusi.

Katika sherehe hiyo mtu aliyepewa kazi ya kujigamba hupewa silaha na baba mzaa bwana harusi, ambayo hukabidhiwa kwa bwana harusi. Silaha hiyo inaweza kuwa mkuki, upinde na mshale, upanga, fimbo, kisu au bunduki. Inawakilisha ushujaa wa mtu aliyeoa. Maneno ya majigambo hutayarishwa mapema ili mtu anayejigamba aweze kuyapangilia vizuri. Wakati anapojigamba bwana harusi husimama akiwa ameshikilia silaha hiyo. Baada ya kujigamba, huwazungukia watu wote waliohudhuria sherehe hiyo na kuwashukuru. Maneno yaongelewayo huelezea hasa jina la bwana harusi, ndugu zake, uwezo wa familia, jinsi alivyompata bibi harusi, maisha yake toka azaliwe na jinsi gani atakavyoishi na mke wake.

Mfano wa majigambo

Naingia

Katuku Karuhango

Mpini uwekwao shoka

Nilikwenda msituni

Kuwinda wanyama

Nikaitwa jina la Mtafuta-vita

Mimi ni nyoka mwenye sumu kali

Hurukia mtini lakini sina mikono na kucha

Nikiteremka chini huteremka

Nikiwa mtambaji

Ni mimi

Mwezi ulioandama Karagwe

Kyamutwara la mgambo likalia

Mtemi hunizungumzia wakati amelala

Kwenye mwamba akijifunika ungo



Huja kwa nguvu! Kwanyamukazi Bugabo

Niliua familia ya Kagoro na Kailali

Nilipogeuka niliua familia

Ya akina Rukora

Heshima ni yako Mtemi

Mfano huu wa majigambo hautoi fundisho zuri sanasana, bali inakuwa kama tishio tu, na yanapotosha. Maana yake kwa ufupi ni kwamba mjigambi ametaja majina ya wazazi wake ambayo ni kweli. Lakini maneno mengine sio ukweli: kuwa nyoka mwenye sumu kali, kurukia mtini bila mikono na kucha, kuwa mwezi ulioandama Karagwe

SURA YA PILI: MNYAMBULIKO WA VITENZI

2.1. Dhana na aina za vitenzi

2.1.1. Dhana

Kitenzi ni neno linaloarifu jambo ambalo hufanywa na jina pia na kiwakilishi na kivumishi kisimamapo peke yake kama jina.

Kwa upande mwingine kitenzi ni aina ya neno linalotoa taarifa juu ya tendo linalofanyika au linalotendwa na kiumbe au kitu.

Mifano:

- Munezero *anakula* viazi mviringo.
- Kamanzi *anapika* wali.
- Mukamana *anampiga* motto
- Sisi *tunakunywa* chai.

i) Tabia ya vitenzi

Kitenzi huarifu vitu muhimu vifuatavyo:

a) Tendo lenyewe litendekalo. Kwa mfano:

- Cheza
- Anakata

b) Wakati tendo linapotendeka. Kwa mfano:

- Anakula (wakati uliopo)
- Alicheza (wakati ukliopita)
- Atafika (wakati ujao)

c) Hali ya tendo. Kwa mfano:

- Ameondoka (tendo limetimilika)
- Anasoma (tendo linaendelea)
- Kalisa huchelewa (tendo la kuzoea)

d) Masharti. Kwa mfano:

- Akija atapewa
- Ungalifika ungaliona

e) Kauli ya tendo. Kwa mfano:

- Kauli ya kutenda: Anapiga
- Kauli ya kutendwa: Anapigwa
- Kauli ya kutendewa: Anapigiwa
- Kauli ya kutendeka: Anapigika
- Kauli ya kutendana: Wanapigana

f) Kama tendo lenyewe ni la kuyakinisha au kukanusha, yaani kutenda au kutotenda. Yaani kitendo kinafanyika au haifanyiki. Kwa mfano:

- Anakula (yakinishi)
- Hakuli (kanushi)
- Unasoma (yakinishi)
- Husomi (kanushi)
- Nimefika (yakinishi)
- Sijafika (kanushi)

2.1.2. Aina za vitenzi

Katika Kiswahili, kuna aina mbili kuu za vitenzi. Aina zenyewe ni hizi:



a) Vitenzi halisi (kweli)

b) Vitenzi vishirikishi

Kitenzi halisi ni neno linaloarifu kwamba jambo linafanywa na mtu, mnyama, mdudu au kitu kingine chochote. Kwa mfano, katika neno **walitutesa** tunaona kwamba neno lenyewe lina sehemu mbalimbali. Kwanza kuna **wa-** kama ilivyoelezwa mwanzoni, hiki ni kiambishi awali cha nafsi. Pili, kuna **-li-** inaonyesha wakati wa mateso yaani katika wakati uliopita. Tatu, kuna **-tu-** inaonyesha watu waliotendwa. Sehemu ya mwisho, **tesa** ni shina la kitenzi halisi. Kwa hivyo, sehemu zote zinzunda neno ambalo linaitwa **kitenzi halisi**.

Kitenzi halisi chaweza kuundwa na:

- Neno moja moja lililo kitenzi. Kwa mfano:

Alimwona rafiki yake

- Kitenzi zaidi ya kimoja vilivyotumika sambamba kwa njia ya kuarifu jambo lile lile moja analotenda. Kwa mfano:

Juma **alikuwa anafundisha**.

Maneno mawili haya katika rangi iliyokoza ni vitenzi viwili sambamba ambavyo pamoja vinaunda kitenzi halisi kimoja.

Kitenzi halisi kimeundwa na vitenzi sambamba; vitenzi sambamba hivyo navyo huwa na ngazi mbili.

- a) Kitenzi kikuuu (T)
- b) Kitenzi kisaidizi (TS)

Kwa mfano:

- Mwezi umeandama
- Shangazi aliwahi kukueleza shida yangu
- Mukamusoni alikuwa amekwisha ondoa vyombo vyote

VITENZI VIKUU NA VITENZI VISAIIDIZI

Kitenzi kikuu

Kitenzi kikuu hubeba mambo matatu:

- i) Hutoa taarifa kamili kuhusu tendo lenyewe linalofanyika,
- ii) Hali ya tendo; tendo lenyewe linaweza kuwa limekamilika au linaendelea kutendeka,
- iii) Kauli, yaani hapa tunapata kujua kama nomino au jina ni mtenda, mtendwa, mtendewa na kadhalika.

Kwa mfano:

Ndugu Nsengiyumva alikuwa *anafundisha*.

- Anafundisha: kitenzi kikuu
- Taarifa: anaelimisha, anampiga vita adui ujinga
- Hali ya kuendelea, yaani anaendelea kufundisha,
- Kauli ya kutenda.

Kitenzi kisaidizi

Kuhusu kitenzi kisaidizi, tunaweza tukasema kwamba kazi zake kubwa ni mbili:

- i) Kwanza ni kusaidia kitenzi kikuu ili sentensi fulani ilete maana kamili na kwa wakati unaotakiwa.

Kwa mfano:

- a) *Alikuwa* anakunywa urwagwa,
- b) Gatete *anaweza* kufunga goli,
- c) Wewe *umekwenda* kuchota maji kisiwani.



Katika mifano hii mitatu, vitenzi saidizi vinasaidia vitenzi vikuu kutoa maana kamili na kwa wakati maalumu. Vitenzi saidizi vyenyewe ni **kuwa**, **weza** na **kwenda**. Kama maneno haya hayatumika, sentensi zetu wakati mwingine zinaweza zikatatanisha kisarufi. Kwa mfano, hatuwezi kusema:

* Gatete kufunga goli

Au

* Wewe kuchota maji kisiwani

Lakini tunaweza kusema: Anakunywa Urwagwa.

Vile vile kwa kutumia hivyo vitenzi visaidizi katika sentensi tatu, tunaona tofauti ya wakati wa matendo yanapofanyika.

Pili, kazi nyingine ya kitenzi kisaidizi ni kueleza kama tendo limefanyika au halikufanyika.

Kwa mfano:

- Mukashema *alikuwa* analala.
- Ngabonziza *hakuwa* amelala.

Katika Kiswahili, vitenzi saidizi vilivyokuwepo ni **kuwa**, **kuja**, **kwisha**, **kwenda**, **weza**, **pata**, **wahi**, **taka** na **kubidi**. Vile vile, katika mazingira mengine, baadhi ya vitenzi saidizi hivi vinawza vikatumika peke yao na kuleta maana kamili katika tungo.

Kwa mfano:

- i) Kayitesi *amekuja* shuleni.
- ii) Nyanya *amepata* pesa zote.
- iii) Yeye *ataka* pombe.

Vitenzi saidizi vinaweza pia kujulikana kwa jina la **VISHIRIKISHI VIKAMILIFU**. Vishirikishi ni maneno ya aina ya vitenzi vinavyoonyesha umoja wa vitu yaani vitu kadha vipo katika hali au tabia au katika mazingira fulani. Vishirikishi ni vya aina mbili: **Vishirikishi vikamilifu** na **vishirikishi vipungufu**.

A) VISHIRIKISHI VIKAMILIFU

Vishirikishi vikamilifu ni vile vinavyochukua viwakilishi nafsi au viambishi ngeli na pia vinaweza vikachukua alama za wakati wowote kama vile **-na-**, **-me-**, **-li-**, **-ta-** na kadhalika. Vishirikishi vikamilifu ni kama kuwa, kwenda, kwisha, kuja, kuweza, kutaka, kupasa, kubidi, kupata, ngali.

- Maneno haya yote hufanya kazi ya vishirikishi vikamilifu, wakati yametumika kama vitenzi saidizi katika vifungu tendo sambamba.

Mifano:

- Kalamu imekwenda kuletwa: N+Ts+T
- Matunda yamekwenda kuchumwa: N+Ts+T
- Angalikuwa amelala: Ts+T
- Majangiri yangali yanakula nyama za karamu
- Amekwisha kucheza
- Amekuja kutambua ubaya wake
- Maneno hayo hayo yakitumika peke yake, au baadhi yake yakitumika na mtendwa (N) au na vielezi vinavyohusika. Hapo hufanya kazi ya **vitenzi halisi**.

Mfano:

- Kazi imekwisha vyema: N+T+E
- Hatutaki mchezo: T+N
- Amepata mbatata (viazi mviringo) nzuri: T+N+V

Maelezo zaidi kuhusu “**kuwa**” na “**ngali**”

1. Kama ilivyotajwa hapo juu **kuwa** na **ngali** ni vishirikishi vikamilifu.

Mfano 1:

- *Alikuwa* anacheza: Ts+T
- *Angalikuwa* anajifunza haungalishindwa: Ts+T+T

- *Hakuwa* anakimbia: Ts+T
- *Akawa* naruka juu juu: Ts+T

Maneno yaliyochapwa kwa italiki ni **vishirikishi vikamilifu**. Vyote vimejengwa juu ya shina moja “**kuwa**”.

Mfano 2:

- Mtoto *angali* anacheza: N+Ts+T
- Wanakijiji *wangali* wanahama: N+Ts+T
- *Hatungali* tumekaa: Ts+T

Maneno yaliyoandikwa kwa italiki ni vishirikishi vikamilifu. Vyote vimejengwa juu ya shina “**ngali**”

2. Vishirikishi vikamilifu hivi **kuwa** na **ngali** huweza kutumika namna mbili:

- a) Kama vitenzi saidizi katika vifungu tenzi sambamba. Hapo alama yake ni Ts (rejea mifano ya hapo juu).
- b) Pamoja na nomino au vivumishi lakini nomino hizo haziwi mtendwa anayepokea pato la kitendo. Bali hizo nomino na vivumishi huwa ni mjalizo tu vinavyoonyesha hali au tabia ya kitu. Na hapo alama yake ni T.

Kwa mfano:

- Mukamana alikuwa mdogo siku hizo: N+T+V
- Habyarimana angali motto: N+T+N

3. Vishirikishi vikamilifu viwili au zaidi vinaweza kutumika pamoja, vyote vikifanya kazi ya vitenzi saidizi (Ts) katika vifungu tenzi sambamba, ili kuunda kitenzi halisi kimoja pamoja na kitenzi kikuu, au peke yake pamoja na kijalizo.

Kwa mfano:

- Alikuwa angali njiani: T+T+N
- Nilikuwa nawahi kuamka: Ts+Ts+T

- Mngalikuwa mngali watoto: T+T+N
- Atakapokuwa anataka jkukimbia, usimwache: Ts+Ts+T+T

B) VISHIRIKISHI VIPUNGUFU

Dhana ya KUWA huwakilishwa na vishirikishi vipungufu. Vishirikishi hivihavina viambishi vya nyakati zote yaani havichukui alama za wakati **-na-**, **-me-**, **-li-** na **-ta-**. Hata hivyo, huweza kuchukua viwakilishi nafsi na viambishi ngeli. Vishirikishi vipungufu vinavyotumika mara nyingi ni **NI**, **SI**, **NDI-**, **-LI-**, **-PO-**, **-KO-**, **-MO-** na kadhalika.

B.1. Matumizi ya vishirikishi vipungufu

i) NI

Hiki ni kishirikishi kinachotumika kwa mtindo wa kukubali ili kuonyesha ukweli wa jambo, ainisho la vitu na pia maelezo ya jambo fulani.

Kwa mfano:

- Kamana **ni** mtoto anayependa kucheza mpira wa kikapu.
- Dalili ya mvua **ni** mawingu.
- Mapenzi **ni** kikohozi, hayawezi kufichika.

Matumizi ya ni yanaonekana kutia mkazo au msisitizo hasa pamoja na viwakilishivya nafsi, vya kuonyesha, vya kumiliki na kadhalika.

- **Ni** mimi nitakayefika.
- **Ni** huyo atakayekuja.
- **Ni** vyetu vilivyopotea.
- **Ni** vipi vilivyokosekana?

ii) SI

Kishirikishi hiki kinaonyesha hali ya kukanusha. Kinaonyesha kwamba mambo fulani hayana ukweli ndani yake au usemi fulani ni kinyume na usemiunaokubaliwa.

Kwa mfano:

- Wawili **si** mmoja.
- Majyambere **si** mjinga.
- Kulenga **si** kufuma.

iii) NDI-

Hiki ni kishirikishi kipungufu kinachotumika kwa mtindo wa kukubali na tena husisitiza maneno. Kishirikishi hiki hakisimami peke yake. Kinapotumika huwa kinaunganishwa na viwakilishi nafsi huru au pamoja na viambishi ngeli vilivyopachikiwa katika **-o-** rejeshi ili kusisitiza kitu fulani.

Si nayo ina tabia hiyo hiyo ya kuweza kuchukua au kuunganishwa na viwakilishi nafsi huru au rejeshi.

Viwakilishi nafsi huru vinavyoweza kuungana na **NDI-** ni hivi vifuatavyo:

Yakinishi**Kanushi**

Ndi-mi (ni mimi)

Si-mimi

Ndi-we (ni wewe)

Si-wewe

Ndi-ye (ni yeye)

Si-yeye

Ndi-si (ni sisi)

Si-sisi

Ndi-ny (ni nyinyi)

Si-nyinyi

Ndi-o (ni wao)

Si-wao

Kwa mfano:

- (Mimi) ndimi mchapakazi: (W)+T+N

- (Yeye) ndiye anayefutwa: (W)+T+T
- Mimi niye anayefutwa: (W)+T+T
- Wewe siwe Yohana?: (W)+T+N

Tanbihi: Viwakilishi nafsi rejeshi vinavyoweza kuungana na **ndi-** au **si** ni vyote isipokuwa **-ji-**.

Mfano:

- Ndio (sio) ukuta wenyewe.
- Ndilo (silo) sanduku lenyewe.
- Ndipo (sipo) mahali nitakapotulia.
- Ndipo au ndio (sio) wakati nitakapolala.

iv) -LI-

Kishirikishi hiki kinatumika mara nyingi katika semi za kurejesha. Kwa kawaida, kishirikishi chenyewe kinaambatana pamoja na kiwakilishi nafsi na kiambishi cha **-o-** rejeshi.

Kwa mfano:

- Aliye hodari, asijivune.
- a-:** kiwakilishi nafsi kiambata (W)
- li-:** kiwakilishi (T)
- ye-:** kiwakilishi nafsi rejeshi (W)
- Walio wagongwa wasifike.
- Tulio wakubwa tumsaidie yule mzee.

Wakati mwingine, **-li-** inaweza ikatumika pamoja na kiwakilishi nafsi katika usemi wa kusisitiza.

Kwa mfano:

- Ngozi ivute **ili** maji.
- Samaki mkunje **ali** mbichi.

-PO-, -KO-, -MO-

Vishirikishi hivi vinaonyesha sehemu ya kitu au mtu alipo. Huweza kutumika kwa njia ya kukubali au kukanusha.

Kwa mfano:

- Kiti *kipo* hapa.
- Watoto *wako* nyumbani.
- Mwizi *yumo* ndani.
- Kijiko *hakipo* darini.
- Mgeni *hayuko* chumbani.
- Kitana *hakimo* kabatini.

B.2. Vishirikishi viwakilishi nafsi na viambishi ngeli

Viwakilishi nafsi na viambishi ngeli hutumika kama vishirikishi pindi vikiwepo katika sentensi na kuweza kuunganisha mawazo mawili au zaidi.

Vishirikishi vyenyewe hufanya kazi sawasawa na NI na huonyesha upatanisho wa kisarufi baina yao na maneno mengine. Matumizi ya vishirikishi hivi yanaweza kuonekana kama ifuatavyo:

- Mimi **ni** maji ya kunywa pombe.
- Mlango **u** wazi.
- Alphonse **yu** daifu siku hizi.
- Sisi **tu** wengi.
- Wao **wa** tayari sana.

- Kijiko **ki** mezani.
- Kabati **li** dogo.

Kuwa inaweza vile vile ikawakilishwa na mofimu **-awa** iliyoambatishwa na kiambishi maalumu. Katika tungo yakinishi, mofimu hii inaweza ikaelezwa na kama hivi:

- *Twawa* wagonjwa siku hizi.
- *Nawa* mpumbavu sana.
- Embe zote *zawa* mbovu.

Katika kutumia tungo kanushi, viambishi mbalimbali vya kukanusha vilivyoambatishwa na mofimu **-awa** vinatumika.

Kwa mfano:

- Sisi *hatuwi* wagonjwa.
- *Siwi* mpumbavu sana.
- Embe zote *haziwi* mbovu.

KUWA NA

Kuwa na huonyesha ushirikisho wa vitu ambapo kitu au mtu humiliki kitu chochote. Kwa wakati wa sasa, **kuwa na** inaweza ikatumika kama hivi:

- Juma *ana* pesa.
- Wao *wana* vitabu vizuri.

Kuwa na inatumika vile vile katika nyakati nyinginezo. Kwa mfano:

- Amina *alikuwa na* mali.
- *Atakuwa na* kalamu.

Katika tungo kanushi, matumizi ya **KUWA** yanaweza pia kutumika katika nyakati mbalimbali. Mifano ifuatayo inathibitisha usemi huu:

- Nyinyi *hamna* pesa.

- *Sitakuwa na chochote kesho.*
- Haji *hakuwa na habari.*

Matumizi ya **KUWA NA** katika wakati uliopo yanaonekana hata katika kuonyesha kuwepo kwa sifa fulani katika kitu au mtu.

Kwa mfano:

- Mzee *ana wasiwasi tu.*
- Nyumba yangu *ina ufa.*

Katika tungo kanushi, matumizi yake yanaonekana kama hivi:

- Mama hana homa.
- Nyumba yangu haina mlango.

Mwishoni, **KUWA NA** katika nyakati nyinginzo huonyesha kwamba vitu viwili vinaandamana, kusindikizana au vinakwenda pamoja au kimoja kiko tayari kwa kutumiwa na chenzake.

Kwa mfano:

- Mvuvu atakuwa na mshipi wake.
- Mkulima atakuwa na jembe lake.

MAZOEZI

1. Eleza kikamilifu maana ya:

- Kitenzi kikuu
- Kitenzi saidizi

Toa mifano ya kutosha kwa kila moja.

2. Kitenzi ni nini? Eleza pia tabia zake katika sentensi. Maelezo yako yaambatane na mifano madhubuti.

3. Tambulisha kitenzi kikuu na kitenzi saidizi katika sentensi zifuatazo:

- a) Mvua kubwa imenyeshwa Kigali.
- b) Msichana alikuwa anapika maji.
- c) Kamali amewahi kufukuzwa na Nizeyimana.
- d) Matofali mengi yameporomoka hapa majuzi.
- e) Nunua mayai sokoni kwa haraka.
- f) Mbona ulikuwa unakwenda kumtazama kaka yako usiku?
- g) Pengine atakuja kuwasili leo.
- h) Kitabu changu kimenunuliwa sana.
- i) Anaweza kutumia anwani yetu ya posta.
- j) Walikwenda kuangalia ajali ya ndege.
- k) Tunaweza kukutana naye wakati wowote.
- l) Mkalimani ameifasiri vizuri hotuba ya mgeni wa heshima.
- m) Eti anataka kunikutana bure.
- n) Faraji alikuwa anataka kumwoa Chausiku.
- o) Chama cha mpira kitafanya mkutano katika Uwanja wa Taifa.
- p) Pesa zangu zote zimenipotea hivi leo.
- r) Huyu mvuvi amewahi kuvua nguru.
- s) Murekatete ametuondoka duniani ghafla.
- r) Toa hoja zako mbele ya hakimu.

4. Nini maana ya vishirikishi? Dhihirisha jibu lako kwa kutoa mifano ya kutosha.

5. Tafuta neno linalofaa katika kila mabano ya sentensi zifuatazo na kisha lijaze katika nafasi tupu ulizopewa:

- i) Wewe.....unayefanya kelele mtaani (ndiye, ni).
- ii) Mimi.....mwerevu kama nitawatukaneni (nawa, siwi).
- iii) Kwa kweli, nyumba yangu ufa hata kidogo (ina, haina).
- iv) Sisi mbioni tu kila mara (tumo, tupo).
- v) Nazi hizi mbovu kwa kukaa sana (zawa, yawa).
- vi) Vijana hawa adabu za kutosha (hamna, hawana).
- vii) Hivi inavyotakiwa na mwalimu mkuu (ndivyo, ndicho).
- viii) Kikombe kabatini kama hujui (kiko, kimo).
- ix) Hiki kitabu bali ni gazeti (sicho, si).
- x) Fadhili mkaidi wa ajabu (u, yu).
- xi) Mbona siku hizi Mugabo haonekani wapi? (yumo, yuko).
- xii) Nyinyi wasiwasi wa bure (mna, wana).
- xiii) Ugomvi huu utakaotutenganisha mimi na mke wangu baadaye (ndio, ndiyo).
- xiv) Baba yako nyumbani mle (yupo, yumo).

2.1.3. VIAMBISHI

Kiambishi ni mofimu iliyopachikwa kwenye kiini au shina la neno ili kulitambulisha neno lenyewe.

Kwa mfano:

- mtu
- kikapu
- makasha
- mishale

Katika kujadili dhana ya kiambishi, ndipo tunapopata pia dhana nyingine inayoitwa upatanisho wa kisarufi ambao ni utawala halisi wa maneno ya fungu moja. Aghalabu maneno yanayoingia katika upatanisho wa kisarufi ni majina, vitenzi, vivumishi na viwakilishi.

2.1.3.1. AINA ZA VIAMBISHI

Baadhi ya wanasarufi huvigawa viambishi katika mafungu matatu kama ifuatavyo:

1. Viambishi awali

Hivi ni viambishi vinavyosimama kabla ya kiini au shina la neno hasa kwenye majina, vivumishi, vitenzi na vielezi. Pia, kuna viambishi vya ngeli ambavyo ni viambishi awali.

Viambishi hivi hupatikana mwanzoni mwa majina ili kuonyesha umoja au wingi wa vitu. Mifano ya viambishi awali katika aina hizo nne za maneno ni kama hii:

- *mkulima mrefu ameanguka.*
- *mtumbwi mkubwa umezama.*
- kisu *kibutu kimeniumiza vibaya.*
- *anakula kizungu.*

Viambishi awali hujitokeza pia katika mtindo wa kukanusha unaonekana katika vitenzi.

Kwa mfano :

- *Sitapika*
- *Hukunieleza*
- *Hakupenda*

Kuna aina mbili za vikanushi: **si-** na **ha-**

a) **Si** : mimi sitakula: **si**-ta-ku-li-a

Mimi sisomi : **si**-som-i

b) **Ha-** : wewe husomi : **ha-u-som-i**

Yeye hasomi: **ha-a-som-i**

Sisi hatusomi: **ha-tu-som-i**

Wao hawataimba: **ha-wa-ta-imb-a**

2. Viambishi kati

Viambishi kati hupatikana mara nyingi katika vitenzi. Viambishi hivi viko namna tatu: viko **viambishi wakati**, **viambishi rejeshi** na **viambishi viwakilishi vya kitendwa**.

Viambishi wakati ni kama **-na-**, **-li-**, **-ta-**, **-ka-**, **-ku-**, **-ki-**, **-takapo-** na **-ji-**. Tuangalie baadhi ya mifano yao katika sentensi hizi:

- Ali **an**acheza mpira.
- **Alin**ipiga mwizi.
- Tuta**ond**oka leo.
- Birasa **ame**fariki.
- Ni**ka**pigwa vibaya.
- Hawa**ku**fika mapema.

Viambishi wakati hujitokeza namna hii katika vitenzi:

a) Wakati uliopo

Huwakilishwa na kiambishi **-na-**

Mifano :

- Ninasoma : ni-na-som-a
- Sisomi : si- ϕ -som-i
- Tunalima : tu-na-lim-a
- Hatulimi : ha-tu- ϕ -lim-i

b) Wakati ujao

Wakati huu huwakilishwa na kiambishi wakati **-ta-**

Mifano:

- Tutasoma: tu-ta-som-a
- Nitalima: ni-ta-lim-a
- Hatutasoma: ha-tu-ta-som-a
- Sitalima : si-ta-lim-a

c) Wakati timilifu (wakati uliopita wa karibuni)

Wakati huu huwakilishwa na kiambishi **-me-** katika hali yakinishi na kiambishi **-ja-** katika hali kanushi.

Mifano:

- Nimesoma kitabu: ni-me-som-a
- Sijasoma kitabu : si-ja-som-a
- Nimekula : ni-me-ku-li-a
- Sijakula : si-ja-ku-li-a

d) Wakati uliopita (wa zamani)

Huwakilishwa na kiambishi **-li-** katika hali yakinishi na kiambishi **-ku-** katika hali kanushi.

Mifano:

- Nilisoma kitabu : ni-li-som-a
- Sikusoma kitabu : si-ku-som-a
- Tulikunywa : tu-li-ku-nyo-a
- Hatukukunywa : ha-tu-ku-nyo-a

e) Wakati uliopita wa masimulizi

Mifano:

- Akaja : a-**ka**-ji-a
- Akaingia : a-**ka**-ingil-a
- Aliniuliza wakakataa : wa-**ka**-katal-a
- **Nika**mwendea, **nika**muuliza, **aka**nijibu

f) Viambishi vingine vinavyoonyesha wakati:

-nge-, -ngeli-, -ngali-, -ki-, -hu-

Mifano:

- Angekosa kazi, angeiba : a-**nge**-kos-a
- Asingekosa kazi, asingeiba : a-si-**nge**-kos-a kazi, a-si-**nge**-iba
- Alinikuta nikitembea : ni-**ki**-temb-il-a
- Walimuita akicheza : a-**ki**-chez-a
- Wanafunzi hupenda kunywa maji : ϕ -**hu**-pend-a

Viambishi rejeshi husimama baada ya viambishi vya wakati. Viambishi vyeneyewe vyabadilika kadiri ya upatanisho wa kisarufi baina ya viambishi hivyo na majina ya ngeli yanayohusika.

Kwa mfano:

- Tun**aji**umiza.
- Anay**eni**sumbuwa ni Mujawayezu.
- Kil**icho**kuvutia ni hiki.

Viambishi viwakilishi vya kitendwa husimama kabla ya shina au baada ya viambishi rejeshi kama vitakuwepo.

Kwa mfano:

- Wanatusema.
- Aliyenipiga ndiye mbaya wangu.
- Tunawapenda.

3. Viambishi tamati

Viko aina nyingi ya viambishi tamati. Kwa mfano:

- Twende, Twendeni.
- Mnasemaje?
- Funga, fungia, fungiana, fungwa, fungwa, fungisha, fungika,

Matumizi ya viambishi

Kwa ujumla, kama inavyoonekana viambishi vinatumika katika njia mbalimbali.

Kwanza, viambishi kama vile vya awali vinatumika katika kubadilisha umoja na wingi wa vitu tofauti.

Kwa mfano:

- Mtu – watu
- Kiti – viti
- Machungwa – chungwa
- Viatu – kiatu
- Wakulima – mkulima

Pili, viambishi awali vinatumika katika kuunganisha maneno mawili yenye maana mbalimbali kuwa na maana moja.

Kwa mfano:

- Mwana+hewa – mwanahewa
- Mchapa +kazi – mchapakazi

Tatu, viambishi awali vya majina kama vile vya **ki**, **ji** na **ma** hutumiwa katika mazingira kadha wa kadha.

Kwa mfano:

- Mtoto – kitoto (kuonyesha hali ya udogo).
- Mti – jiti (kuonyesha hali ya ukubwa katika umoja).
- Joka – majoka (kuonyesha hali ya ukubwa katika wingi).

Nne, viambishi awali kama vile vya **ku-** n a **hu-** katika vitenzi pia huwa na matumizi yao maalumu.

Kwa mfano:

- Kuiba kunakatazwa (kutoa maelezo).
- Hula nyama kila siku (kuonyesha mazoea).

Kuhusu viambishi tamati, baadhi ya matumizi yao yanaonekana kama ifuatavyo:

- Jirekebishe – jirekebisheni (kutoa amri).
- Ameibi**wa** (kuonyesha kutendwa).
- Aliniimb**ia** (kuonyesha kutenda kwa ajili ya mtu au kitu fulani au kwa maneno mengine kuonyesha kutendewa).
- Tulikupig**isha** (kuonyesha dhana ya kusababisha).
- Anasem**aje?** (kuonyesha maulizo ya kutaka kujua kitu fulani).
- Tulikwenda duk**ani** (kuonyesha mahali kwa njia ya maelezo).
- Waend**api?** (kuonyesha mahali kwa njia ya maulizo).

ZOEZI

Kiambishi ni kitu gani? Eleza matumizi mbalimbali ya kiambishi.

SURA YA TATU: UAMBISHAJI WA VITENZI

Katika lugha ya Kiswahili vitenzi ndicho kipengele cha kisarufi ambacho hubeba viambishi vingi kuliko vipengele vingine. Viambishi hivyo huwa na huwa na uamilifu mbalimbali. Viambishi hivyo vimefafanuliwa kwa makini katika sehemu ndogo zifuatazo:

3.1. Viambishi vya unyambulishaji katika vitenzi

Unyambulishaji ni ni upachikaji wa viambishi kwenye mzizi ili kuunda maneno mapya. Katika lugha ya Kiswahili kuna viambishi nyambulishi ambavyo vinatumika katika uundaji wa vitenzi vipya kama inavyoonekana katika mifano hapa chini:

- Pend-a
- Pend-*il*-a (pendea)
- Pend-*il-il*-a (pendelea)
- Pend-*il-il-an*-a (pendeleana)
- Pend-*il-y*-a (pendeza)
- Pend-*il-y-ish*-a (pendezesha)
- Pend-*il-y-ish-an*-a (pendezeshana).

Hapa kutokana na mzizi wa kitenzi pend-, tunaweza kupata maneno kama yale yaliyoorodheshwa katika mfano ambapo viambishi tamati -il-, -an-, -il-il-, -ish- ni nyambulishi kutokana na kufanya maumbo yanayohusika kuwa vitenzi vyenye maana tofauti.

Kiswahili kina viambishi tamati nyambulishi vinane ambavyo huambikwa kwenye mizizi ya vitenzi kama ilivyoonyeshwa katika mifano iliyotangulia. Vinyambulishi hivyo ni kama vifuatavyo:

- a) -w-

- b) -ik-
- c) -ish-/-il-y-
- d) -il-/-il-il-
- e) -ul-
- f) -am-
- g) -at-
- h) -an-

Hapa tunaona orodha kamili ya viambishi nyambulishi vinavyoambikwa kwenye mizizi ya vitenzi na baadhi ya alomofu (umbo jingine la mofimu hiyo hiyo moja) zake.

Viambishi vya nafsi

Viambishi vingine ambavyo, kwa kawaida, huandamana tu na vitenzi ni vile vya nafsi. Hivi ni pamoja na viambishi ni-, u-, tu-, m-, wa-, -ku-, n.k. ambavyo hujitokeza katika mifano ifuatavyo:

- ni -merudi	tu -merudi
- u -takuja	m -takuja
- a -nalala	wa -nalala
- ni -me- ku -ona	ni -me- wa -ona
- u - ta - ni -penda	m - ta - tu -penda

Katika mifano hii viambishi vinavyojitokeza mwanzo kabisa vinawakilisha nafsi katika nafasi ya kiima kama ifuatavyo:

ni: nafsi ya kwanza umoja

u: nafsi ya pili umoja

a: nafsi ya tatu umoja

tu: nafsi ya kwanza wingi

m: nafsi ya pili wingi

wa: nafsi ya tatu wingi

Katika mifano hapo juu, vile viambishi vyenye rangi iliyokoza, ambavyo ni **-ku-na -n-**, vinavyokabiliana na mashina ya vitenzi **ona** na **penda**, navyo ni viambishivya nafsi ya yambwa. Nafsi katika nafasi ya kiima ni nafsi ya nomino mtenda (yaani, ile inayotenda tendo) na nafsi katika nafasi ya yambwa, ni ya nafsi mtendwa (yaani, ile inayopokea tendo). Viambishi hivyo vya nafsi vinaweza kueleweka vizuri zaidi kwa kukichunguza kielelezo kitakachoonyeshwa hapo chini.

Aidha kiambishi kingine cha nafsi ambacho huambikwa mwishoni mwa vitenzi ni **-ni**. Kiambishi tamati hiki kinapoambikwa kwenye vitenzi vya Kiswahili huwa kinabeba dhana ya idadi hasa ya nafsi ya pili wingi. Kwa mfano, **ondoke-ni, some-ni, simame-ni, lale-ni**, n.k. Aidha kiambishi hiki hujitokeza kwenye maumbo mengine kwa maana hiyo hiyo ya kubeba dhana ya idadi au wingi. Kwa mfano: **karibu-ni, kwaheri-ni, ahsante-ni**, n.k.

Viambishi nafsi: kielelezo

Nafsi	Katika nafasi ya kiima	Katika nafasi ya yambwa
1. Umoja	ni- : ni -limuona	-ni- : wali- ni -ona
2. Umoja	u- : u -likuja	-ku- : tuta- ku -fundisha
3. Umoja	a: a -tarudi	-m- : tuta- m -sema
1. Wingi	tu- : tu -tafika	-tu- : ata- tu -shitaki
2. Wingi	m- : m -nasoma	-wa- : nina- wa -penda
3. Wingi	wa- : wa -nalala	-wa- : tuli- wa -ona

Viambishi vya njeo

Tungependa tutoe pia maelezo mafupi kuhusu viambishi awali vya njeo ambavyo vinajitokeza katika maumbo ya vitenzi vya Kiswahili> orodha nzima ya viambishi hivi ni kama inavyonyeshwa katika kielelezo kifuatacho:



Kiambishi	Njeo (wakati)	Mtindo wa kitenzi
-li- : a- li -kula	Wakati uliopita	Kukubali
-me- : a- me -rudi	Wakati uliopita hali timilifu	Kukubali
-na- : u-na-lala	Wakati uliopo	Kukubali
-ta- : m- ta -lewa	Wakati ujao	Kukubali
-ku- : ha- ku -lia	Wakati uliopita	Kukanusha
-ja- : ha-tu- ja -li-a	Wakati uliopita hali timilifu	Kukanusha
-hu- : hu -wa	Hali ya mazoea	Kukubali
-i : ha-tu-l- i	Wakati uliopo	kukanusha

Mifano zaidi ya matumizi ya viambishi hivi ni kama hii ifuatavyo:

a) Wakati uliopita (kukubali)

ni-**li**-kula

tu-**li**-kula

wa-**li**-tu-tafuta

vi-**li**-haribika

b) Wakati uliopita hali timilifu (kukubali)

tu-**me**-soma vizuri

wa-**me**-tembea kwa mguu

vi-**me**-letwa muda si mrefu

ni-**me**-itwa na mama

c) Wakati uliopo (kukubali)

u-**na**-zungumza Kiswahili

m-**na**-m-taka nani?

ya-**na**-li-a-wa

d) Wakati ujao (kukubali)

vi-**ta**-rudishwa vyote

wa-**ta**-vi-penda

a-**ta**-ni-kop-ish-a fedha

e) Wakati uliopita (kukanusha)

ha-**ku**-ni-ona

si-**ku**-wa-pelek-il-a barua zao

ha-vi-**ku**-nun-ul-il-w-a

f) Wakati uliopita hali timilifu (kukanusha)

ha-**ja**-rudi

si-**ja**-wa-ona

ha-ki-**ja**-iva

g) Hali ya mazoea (kukubali)

Yeye hu-tu-temb-il-il-a mara kwa mara

Wanafunzi hu-wa-heshimu watu wazima

Watoto hu-m-said-il-a mwalimu wao kazi

Mifano yote isipokuwa ule uliotolewa katika “g” (ambapo njeo hutangulia) inawonyesha wazi kwamba viambishi vya njeo hufuatana na viambishi vinavyowakilisha kiima moja kwa moja.



Viambishi vya hali

Viambishi vya hali, kwa upande mwingine, ni vile vinavyoonyesha dhamira ya maelezo. Viambishi hivi na dhana zake vinaonyeshwa ifuatavyo pamoja na mifano yake ya matumizi.

- a) **-a:** kiambishi cha dhamira dhahiri
- b) **-e:** kiambishi cha dhamira ya matilaba, yaani ya kuonyesha nia ya kutenda jambo
- c) **-po-:** kiambishi (cha sharti) cha kuonyesha mahala, au muda
- d) **-ka-:** kiambishi cha mfuatano wa matendo
- e) **-ki-:** kiambishi cha sharti
- f) **-ki-:** kiambishi cha tendo kuendelea
- g) **-ki-:** kiambishi cha hali fanani
- h) **-li-:** kiambishi cha hali ya kuwa
- i) **-nge-/-ngali-/-ngeli-:** viambishi vya kudadisi tendo.

i) Kiambishi wakati (hali) “ku-“

Kiambishi hiki “ku-“ kinatumika kunyesha hali ya nyakati mbalimbali.

Tazama mifano hii:

1) Kama tendo limefanyika na kukamilika

- Nimeokota fimbo na **kumpiga** nyoka kichwani.
- Tumefunguwa na **kufunga** sanduku lile.
- Wamemuona samba na **kumkimbia**.
- Amemkuta na **kumsaidia**.

Tungo hii, “Nimeokota fimbo na kumpiga nyoka kichwani” inatuonyesha kuwa tendo la **kuokota** na tendo la **kupiga** tayari yamefanyika.

“Tumefungua na kufunga sanduku lile”. Tungo hii pia inatuonyesha kutimilika kwa matendo ya **kufungua** na **kufunga**.

Kwa mifano hii, kiambishi hiki **ku-** kinatuambia juu ya tendo ambalo limetimilika.

2) Kama tendo litakamilika

- Atamkamata na **kumfunga** kamba
- Utakula chakula na **kulipa** gharama
- Watacheza na **kushinda** bila wasiwasi
- Nitakwenda **kumwita** sasa hivi
- Nitakuja **kumsikiliza** mwimbaji kutoka Tanzania
- Utachima viazi na **kuviuza** vyote.

Kwa kutanguliwa na vitenzi vyenye kuonyesha wakati ujao **-ta-**, **ku-** katika kitenzi cha pili katika tungo, kinaonyesha kuwa tendo linalokusudiwa katika tungo nzima litatimilika.

3) Kama tendo lilikamilika

- Tulimkuta na **kumchukua**
- Nilifua na **kuzianika** nguo zote
- Ulikwenda **kuazima** mwavuli wake
- Aliteleza na **kuanguka** vibaya
- Alifunika vibaya na **kuvunja** chupa
- Walifurahi na **kumpa** kila mtu zawadi.

Katika mifano hii, **ku-** inaonyesha kutimilika kwa tendo katika wakati uliopita. Kwa maneno machache, kiambishi **ku-** ili kionyeshe dhana hii ya kutimilika na kutendeka kwa tendo hutumika iwapo vitenzi viwili vinafuatana. Kwa mfano:

Alikwenda na kumpa pole.

Nitakuja kumsikiliza mwimbaji.



ii) Kiambishi “-ka-“

Tunapozungumza juu ya masimulizi au maelezo ya matukio ya matendo yanayofuatana na ndipo kiambishi hiki **-ka-** hutumika.

Tazama mifano hii:

- Mamba mdogo **akafikiri** namna ya kupata moyo wa tumbili **akashindwa**.
- Mamba **akamkumbuka** rafiki yake tumbili **akasema**, “Nimegundua hila”
- Baada ya muda, tumbili **akafika** pale kwenye mti.
- Mamba **akamwambia** tumbili, “Twende **ukapaone** ninapoishi”.
- Alipofika kule juu ya mti, tumbili **akamcheka** sana mamba.

Wakati uliopita

Tunaposimulia juu ya matukio yaliyotendeka, ama kwa wakati uliopita wa **-li-** au wakati uliotimilika wa **-me-**, tunatumia **-ka-**.

Yohana alikuwa akitembea njiani, mara akamwona nyoka mkubwa sana, **akashtuka**, **akaruka**, **akatafuta** fimbo haraka **akaiona** **akaanza** kumpiga nyoka. **Akampiga** kichwani, **akampiga** mgongoni, **akampiga** mkiani, **akamkata** kichwa, kisha **akachimba** shimona kumfukia!

Wakati ujao

Tunapozungumza juu ya matendo yatakayofanyika, kwa kutumia wakati unaoendelea (-na-) au katika wakati ujao wa (-ta-), tunaweza kutumia **-ka-** katika maelezo yetu, tunapoamrisha au kuonyesha hali ya kutazamia, tunatumia **-ka-** kama hivi:

- Nenda **ukalime** bustani
- Nenda **ukanunue** sigara
- Tutakwenda bwaloni **tukatazame** filamu
- Twendeni **tukacheze** mziki

- Kesho asubuhi nitaamka **nika**oge, nivae nguo zangu, niende kunywa chai kisha niende darasani kusoma hadithi ya kulisimua.

iii) Kiambishi “-ki-“

Kiambishi -ki-hutumika kwa kuonyesha wakati na hali. Kiambishi hiki kinapotumika huonyesha nyakati katika hali;

1. Huonyesha kuwa kitendo kimoja kilipokuwa kinatendeka wakati huo kitendo kingine kilikuwa kinatendeka pia.

Mfano: **Wakati uliopo**

- Mvua ilikuwa **iki**nyesha wakati tulipokuwa **tuki**safiri.
- Gasana alikuwa **aki**nywa pombe wakati **aki**endesha basi.
- Shemsa alikuwa **aki**pika, mama yake alipokuwa **aki**mnonyesha mtoto.
- Walikuwa **waki**piga kelele, walipokuwa **waki**tufukuza.
- Mukamwiza alikuwa **aki**lia, alipokuwa **aki**nyolewa.

2. Kiambishi hiki huonyesha pia iwapo kitendo kitakuw kikiendelea wakati kingine kitafanyika.

Mfano: **Wakati ujao**

- Mtakapofika mtawakuta **waki**wangoja
- Uwimana atakuwa akila nitapokuwa **niki**andika barua.
- **Waki**chelewa watatukuta **tuki**cheza.
- Utakapokwenda, utamkuta **aki**oga.
- Wakulima wa mpunga watakuwa **waki**vuna huku **waki**panda miche mingine.

3. Kiambishi **-ki-** hutumika kuonyesha kuwa tendo limekuwa likitendeka kwa mda mrefu.

Mfano: **Wakati wa mazoea**

- Timu yetu imekuwa **iki**shinda kwa muda mrefu.

- Mpira wa kikapu umekuwa **ukipendwa** kwa miaka mingi.
- Gahizi amekuwa **akicheza** michezo mingi bila kushindwa.
- Tumekuwa **tukila** wali na maharage kila siku.
- Kabendera alikuwa **akitangaza** vizuri redioni.

4. Katika wakati ujao au wakati uliopita kiambishi hiki hutumika katika tungo zenye masharti.

Mfano:

- **Tukisikia** mlio wa risasi sote tutakimbia ovyo.
- **Mkicheza** vizuri mtashinda bila wasiwasi.
- **Ukiomba** utapewa.
- **Akiumwa**, tutampeleka zahanatini.
- **Mkikimbia** mtaliwahi basi.

iv) Kiambishi “-po-”

Kiambishi hiki kinapotumika katika kitenzi huonyesha kuwa:

1. Tendo linafanyika na kufuatwa na jingine.

Mifano:

- Nilip**osikia** habari wakitakanyara, nilihofia sana kupanda ndege.
- Mukanyandwi alip**ofika** Kigali, alishangaa kuona magari mengi sana.
- Walikwenda kumpokea Rais alip**ofika** uwanja wa ndege.
- Watu wote walimtaazama Mukamwiza alip**oanza** kucheza.
- Alip**oshindwa** kufunga breki ya baiskeli, alianza kupiga kelele kuomba msaada.

2. Kiambishi hiki hutumika pia kuonyesha kuwa tendo litafanyika na kufuatiwa na jingine.

**Mifano:**

- Watakapovuna njegere watazitaryarisha na kwenda kuziua sokoni.
- Atakapouliza atajibiwa.
- Tutakapowasili Musanze tutakuwa tumechoka sana.
- Utamsubiri hapa mpaka atakapofika.
- Watakapofika kiwanjani watawababaisha wachezaji wengine wote.

3. Kiambishi hiki vilevile huweza kutumika kwa kuonyesha kuwa tendo hufanyika na kufuatwa na jingine.

Mfano:

- Nisikiapo wimbo wa Malaika machozi hunilengalenga.
- Murekeraho atembeapo barabarani, hutufurahisha sote.
- Apatapo pesa, huwaita rafiki zake wote kunywa pombe.
- Umuonapo, moyo wake hutulia.
- Ufuapo nguo zake, husuburi chini ya mti.

v) Viambishi “-nge-, -ngali-, -ngeli-“

-nge-, -ngali-, -ngeli-, viambishi hivi ni viambishi ambavyo hutuarifu juu ya hali ya masharti. Matumizi ya viambishi hivi hutegemea utashi wa mzungumzaji, kwa maana kwamba anaweza kutumia kimoja badala ya kingine. Viambishi hivi hutuarifu juu ya sharti kwamba tendo moja ni lazima lifanyike ndipo tendo jingine nalo lifanyike. Ni viambishi vya masharti katika wakati uliopo na uliopita.

Mifano: Wakati uliopo

1. a) Ningekuwa na koti safi sasa, ningekwenda harusini.
- b) Ningalikuwa na koti safi sasa, ningalikwenda harusini.
- c) Ningelikuwa na koti safi sasa, ningelikwenda harusini.

2. a) Kama **ningekuwa** na pesa sasa, **ningenunua** shati hili.
- b) Kama **ningalikuwa** na pesa sasa, **ningelinunua** shati hili.
- c) Kama **ningelikuwa** na pesa sasa, **ningelinunua** shati hili.
3. a) **Ningejua** kuwa mvua itanyesha leo, **ningenunua** mwavuli jana.
- b) **Ningalijua** kuwa mvua itanyesha leo, **ningalinunua** mwavuli jana.
- c) **Ningelijua** kuwa mvua itanyesha leo, **ningelinunua** mwavuli jana.

Wakati uliopita

1. a) Kama **wangewahi** kuondoka siku ile, mvua **ingewanyeshea**.
- b) Kama **wangaliwahi** kuondoka siku ile, mvua **ingaliwanyeshea**.
- c) Kama **wangeliwahi** kuondoka siku ile, mvua **ingeliwanyeshea**.
2. a) **Wangewahi** kuamka, **wangeweza** kuwahi shuleni.
- b) **Wangaliwahi** kuamka, **wangaliweza** kuwahi shuleni.
- c) **Wangeliwahi** kuamka, **wangeliweza** kuwahi shuleni.
3. a) Kama wasi**ng**ekamatwa pale mlangoni, wangi**e**iba faranga.
- b) Kama wasi**ngal**ikamatwa pale mlangoni, wangi**li**iba faranga.
- c) Kama wasi**ngeli**kamatwa pale mlangoni, wangi**li**iba faranga.

Tanbihi:

Katika matumizi ya viambishi hivi, tunaweza kukanusha kwa kutumia kikanushi “si”.
Kama sehemu ya tatu hapa juu.

“Kama wasi**ng**ekamatwa pale mlangoni, wangi**e**iba faranga zote za benki”.

Mifano:

- Kama asi**ng**elisoma barua ile, asi**ng**elielewa kusudi letu.
- Asi**ng**alituambia shida yake, tusi**ng**alimsaidia.

- Nisingalikunywa dawa ya kuzuia malaria, ningaliumwa leo.
- Nisingalifika mkutanoni, nisingalielewa yote yaliyozungumzwa.

Viambishi virejeshi

Katika Kiswahili pia, viambishi vya kisarufi vilivyojadiliwa hapo awali huweza kuungana na kiambishi cha **-o-** rejeshi kuunda aina nyingine ya viambishi amilifu katika lugha hii. Aina hii hujulikana kama **viambishi rejeshi**. Viambishi hivi ni vile vinavyowakilisha kitajwa katika umbo hasa la vitenzi. Viambishi hivi hujitokeza ifuatavyo:

- a) wa+o = wo = o: k.m. wa-li-**o**-ku-ji-a
- b) u+o = wo =o: k.m. u-li-**o**-anguk-a
- c) li+o = lo: k.m. li-li-**lo**-nun-ul-il-w-a
- d) ch+o= cho: k.m. ki-li-**cho**-pot-il-a
- e) i+o = yo: k.m. i-li-**yo**-simam-a
- f) vy+o = vyo: k.m. vi-li-**vyo**-let-w-a
- g) zi+o = zo: k.m. zi-na-**zo**-fanan-a

Katika mifano ya hapo juu, huonyeshwa viambishi virejeshi na taratibu za uundaji wake katika Kiswahili. Vinavyojitokeza katika maumbo ya vitenzi ilivyoonyeshwa, huwa vinarejerea kitajwa, yaani nomino inayohusika na tendo.

Kwa ajili ya marejeo ya haraka na wepesi, viambishi vilivyomo katika lugha ya Kiswahili vimeorodheshwa katika sehemu ifuatayo hapa chini. Katika orodha hii viambishi vinagawanywa katika makundi kulingana na dhana zake, lakini mifano inayotolewa huonyesha pia nafasi vinamokaa katika maumbo ya maneno, yaani kama ni awali au tamati. Aidha orodha hii inaonyesha wzi kwamba katika lugha hii baadhi ya viambishi hufanana katika maumbo yake. Mfanano huu unajitokeza hata miongoni mwa viambishi vilivyoainishwa katika kundi moja. Kwa mfano, katika kundi A kun viambishi m- mbili, n- mbili na ku- mbili. Vivyo hivyo katika orodha nzima kuna viambishi m- vingine kadhaa, -ji- tatu, li- tatu, n.k. Viambishi vyote hivi vinajitokeza katika miktadha tofauti.

3.2. Orodha ya viambishi katika Kiswahili

Ifuatayo ni orodha ya viambishi mbalimbali vinavyojitokeza katika maneno mbalimbali ya lugha ya Kiswahili:

1. Viambishi vya nomino (au upatanisho wa kisarufi)

Kiambishi	Kiambishi (nomino)	Kiambishi (kivumishi)	Kiambishi (kiwakilishi)
m-	m-tu	m-zuri	a, yu, u, ye a-li-ku-ji-a yu-le, wa-ngu, a-li-ye-ku-ji-a
wa-	Wa-tu	Wa-zuri wa-ta-fika	wa, o wa-li-o-fik-a
m-	m-ti	m-refu	u, o u-li-oz-a u-li-o-oz-a
mi-	mi-ti	mi-refu	i, yo i-li-oz-a i-li-yo-oz-a
ji-	ji-cho	j-eusi	li, lo li-ta-um-a li-li-lo-um-a

Kiambishi	Kiambishi (nomino)	Kiambishi (kivumishi)	Kiambishi (kiwakilishi)
ma-	ma-cho	ma-dogo	ya, yo ya-na-um-a ya-li-yo-um-a
ki-/ch-	ki-ti	ki-dogo	ki/ch, cho ki-li-fung-w-a ki-li-cho-fung-w-a
vi-/vy-	vi-ti	vi-dogo vy-eusi	vi-/vy, vyo vi-li-vunj-ik-a vi-li-vyo-vunj-ik-a
n-	ngoma	n-zuri	i, yo i-li-lal-a i-li-yo-pasuk-a
n-	ngoma	n-zuri	zi, zo zi-li-pasuk-a zi-li-zo-pasuk-a
u-	u-kuta	m-refu	u, o u-li-anguk-a u-li-o-anguk-a
ku-	ku-oga	ku-zuri	ku, ko ku-li-pend-il-y-a ku-li-ko-pend-il-y-a



Kiambishi	Kiambishi (nomino)	Kiambishi (kivumishi)	Kiambishi (kiwakilishi)
ku-	ku-le	ku-baya	ku, ko ku-na-vut-il-a ku-na-ko-vut-il-a
pa-	pa-le	ku-baya	pa, po pa-na-vut-il-a pa-na-po-vut-il-a
mu-	m-le	pa-zuri	mu, mo m-na-vut-il-a m-na-mo-vut-il-a

2. Viambishi vya nafsi

a) Nafsi ya kiima:

Kiambishi Nafasi yake katika neno

ni- ni-li-ku-ji-a

u- u-li-ku-ji-a

a- a-li-ku-ji-a

tu- tu-li-lal-a

m- m-ta-fik-a

wa- wa-ta-lil-a

b) Nafsi kiima ya yambwa

Kiambishi Nafasi yake katika neno

-ni- a-me-ni-on-a

-ku- tu-me-**ku**-on-a
-m- ni-ta-**m**-pig-a
-tu- a-ta-**tu**-sem-a
-wa- m-ta-**wa**-on-a
-wa- tu-ta-**wa**-on-a
-ji- a-me-**ji**-kat-a
-ni some-**ni**

3. Viambishi nyambulishi:

a) Viambishi vya vitenzi:

Kiambishi Nafasi yake katika neno

-w- pig-**w**-a
-ik- vunj-**ik**-a
-ish- chek-**ish**-a
-il-il- pig-**il-il**-a
-ul- vul-a
-am- kw-**am**-a
-an- on-**an**-a
-at- fumb-**at**-a

b) Viambishi vya nomino

Kiambishi Nafasi yake katika neno

-ji m-sema-**ji**
-u u-ok-ul-**u** (wokovu)
-o ki-zib-**o**

- e m-tum-e
- i m-som-i
- ni jiko-ni

4. Viambishi vya njeo

a) Viambishi viyakinishi

Kiambishi Nafasi yake katika neno

- li- a-li-ku-ji-a
- me- a-me-ku-ji-a
- na- a-na-lal-a
- ta- a-ta-lal-a

b) Viambishi vikanushi

Kiambishi Nafasi yake katika neno

- ku- ha-ku-ji-a
- ja- ha-ja-ji-a
- i ha-lal-i
- ta- ha-ta-lal-a

5. Viambishi kanushi

Kiambishi Nafasi yake katika neno

- ha i ha-wa-tak-i
- si i si-wez-i



6. Viambishi vya hali

Kiambishi Nafasi yake katika neno

-po-	a-li- po -fik-a
-ki-	a- ki -li-a (kula)
-nge-	wa- nge -on-an-a
-ngali-	a- ngali -fik-a
-ki-	a- ki -som-a
-li-	a- li -ye
-ka-	a- ka -ji-a (kuja)
-a	val- a (kuvaa)
-e	w-end- e
ki-	ki -jinga

MAZOEZI

1. Toa maelezo kuhusu viambishi awali **ni-** na viambishi tamati **-ni** katika Kiswahili. Je, vinatokea katika maumbo gani ya maneno na vinabeba dhana zipi?
2. Nini maana ya “Viambishi awali”, “viambishi kati” na “viambishi tamati”.
3. Tenganisha viambishi katika maumbo yafuatayo:

- sawazisha	- mpenzi
- shikilia	- maombezi
- wasiliana	- msingalijua
- hatukumsogelea	- mazungumzo
- hawatakukumbuka	- msahaulifu
- majinizano	



4. Bainisha mizizi katika maneno yafuatayo:

- nilimwona
- kimbiliana
- mtu
- amehamishwa

SURA YA NNE: UUNDAJI WA MANENO KATIKA LUGHA YA KISWAHILI

Kwa kawaida vijenzi muhimu vinavyohusika katika kuunda maneno ni viambishi, mizizi na mashina kama vilivyozungumziwa hapo juu. Kwa kuunda maneno, vijenzi hivi huungana kwa namna mbalimbali. Taratibu zinazohusika katika kuunganisha vijenzi hivi ndizo hujulikana kama «uambishaji» na «unyambulishaji».

4.0. Uundaji wa maneno ya kiswahili

Uduni, wastani na udogo.

Unaweza kuunda maneno yaonyeshayo uduni, wastani na ukubwa. Maneno haya, kwa kawaida, huundwa kutoka kwa maneno ya wastani, yaani ya kati kwa kati ama ya kawaida, hata ingawa muundo huu hutegemea uliouanzia.

Kwa mfano unaweza kulichukua neno la kawaida kama vile 'mtu' na ukaliundia ukubwa wake 'jitu' na halafu ukaliundia udogo wake, yaani 'kijitu.' Utaona hapa kwamba ni jambo la kufaa ukitafuta ukubwa wa neno la wastani kwanza kwa sababu hali ya udogo huwa ni ule ule ukubwa ambao umetanguliziwa na "ki-".

Mifano:

<i>Uduni</i>	<i>Wastani</i>	<i>Ukubwa</i>
Kidege	ndege	dege
Kigombe	ng'ombe	gombe
Kijito	mtu	jito
Kifupa	mfupa	fupa
Kijisu	kisu	jisu
Kijikombe	kikombe	kombe

Hata hivyo si maneno yote ya Kiswahili yanayoweza kuuchukua muundo huu.

Yale ambayo kabisa hayawezi kuingia hapa hutumiwa pamoja na maneno 'dogo' ama 'ukubwa' k.v.

'mwiko mdogo' ama 'mwiko mkubwa

Dhana ya dhahania

Dhana ya dhahania ni dhana ambayo ni ya kufikilika yaani maneno ambayo hayashikiki. Kwa mfano:

m-toto: u-toto

m-zee:u-zee

bikira: u-bikira

ki-jana: u-jana

safi: u-safi

baya: u-baya

zuri: u-zuri

rembo: u-rembo

4.1. UAMBISHAJI

Uambishaji ni utaratibu wa kuweka kiambishi kabla, katikati au baada ya mizizi. Ni utaratibu wa kuambatisha viambishi kwenye mzizi. Katika Kiswahili uambishaji unaopatikana ni wa aina mbili kama vile uambishaji wa kabla ya mzizi na uambishaji wa baada ya mzizi. Uambishaji wa katikati ya mzizi katika lugha ya Kiswahili haupo.

Mifano:

- M-tu; ki-tu
- Ma-kabati; m-lango
- Andik-il-a: l → Φ/I-I

- Pelek-a
- Kal-a: $l \rightarrow \Phi / I-I$
- Wa-li-o-tu-pend-ik-il-y-a: $l+y=z, i \rightarrow e/ze-$
- Tu-li-wa-nunul-il-a: $l \rightarrow \Phi / I-I$
- Wa-me-tu-pig-an-ish-a
- M-na-ondok-a

Uambishaji ni uundaji wa maneno kutoka maneno mengine. Uambishaji hufanyika kwa kuongeza viambishi awali au tamati kwenye mizizi au mashina ya awali na kupata maneno mapya.

Katika uambishaji huu, mizizi ya maneno inaweza kuwekewa viambishi kadha wa kadha. Kwa mfano, mizizi ya maneno inaweza kuwekewa viambishi vya umoja, viambishi vya wingi, viambishi vya ukubwa na viambishi vya udogo. Kapinga, M.C. (1983:16).

Kuna aina mbili za uambishaji:

- Kuunda vitenzi (uambishaji wa vitenzi)
- Kuunda nomino (uambishaji wa majina)

4.1.1. Uambishaji wa vitenzi

Ni uundaji wa vitenzi kutoka maneno mengine. Kuna uundaji wa vitenzi kutoka: vitenzi vingine, nomino, vivumishi, vielezi.

1. Vitenzi kutoka vitenzi

Namna hii hufanyika kwa kuongeza viambishi tamati kwenye mizizi ya vitenzi. Viambishi tamati ni mofimu zinazochukua nafasi baina ya mzizi na mwisho wa kitenzi. Mwambatano huu wa mzizi na kiambishi tamati unaitwa **shina la kitenzi**.

Kuna aina 3 za viambishi tamati vinavyotumika katika uambishaji:

- Viambishi tamati vya kawaida
- Viambishi tamati maalumu
- Viambishi tamati vya kimaumbo

❖ **Viambishi tamati vya kawaida**

Ni aina za viambishi tamati vinavyoweza kuambatana na mzizi wowote wa vitenzi.

Kuna viambishi tamati vifuatavyo:

- Kiambishi tamati sababishia (tendea)
- Kiambishi tamati unganisha (tendana)
- Kiambishi tamati sababisha (tendesha)
- Kiambishi tamati sababishwa (tendwa)

a) Kiambishi tamati sababishia (tendea)

Kiambishi tamati sababishia kina umbo **-il-**. Humaanisha kwamba dhana ya kitenzi hukamilishwa kwa ajili ya mtu fulani au katika mahali fulani.

Mifano:

- Kupikia: ku-pik-il-a: l →Φ/I-I
- Kuchezea: ku-chez-il-a: l →Φ/I-I, i →e/ze-
- Kukalia: ku-kal-il-a: l →Φ/I-I
- Kusomea: ku-som-il-a: l →Φ/I-I, i →e/zo-
- Kunywea: ku-nyo-il-a: l →Φ/I-I, o →w/-I

b) Kiambishi tamati unganisha (tendana)

Kiambishi tamati unganisha kina umbo **-an-**. Kinaonyesha kwamba viumbe wawili au zaidi hushirikiana kukamilisha kitendo kila mojawapo akishiriki kwa niaba ya mwingine.

Mifano:

- Wameonana: wa-me-on-an-a
- Wanapigana: wa-na-pig-an-a
- Wameuana: wa-me-ul-an-a: l → Φ/I-I
- Mnapendana: m-na-pend-an-a

c) Kiambishi tamati sababisha (tendesha)

Kiambishi tamati sababisha kina maumbo ya: **-ish-**, **-y-**. Hutumiwa ndani ya kitenzi kwa kusema kuwa kiumbe amesaidiwa na kiumbe mwingine au kutumia kifaa fulani ili kutimiza kitendo.

Mifano:

- Kuchosha: ku-chok-y-a: k+y=sh
- Kuchekesha: ku-chek-ish-a: i → e/ze-
- Kufunza: ku-fund-y-a: d+y=z
- Kulaza: ku-lal-y-a: l+y=z
- Kufundisha: ku-fund-ish-a

Tanbihi: Kiambishi tamati sababisha **-ish-** katika lugha ya Kinyarwanda hutumiwa nyuma ya mzizi ambao huishia na konsonanti, wakati kiambishi tamati sababisha **-sh-** hutumiwa nyuma ya mzizi ambao huishia na irabu.

d) Kiambishi tamati sababishwa (tendwa)

Kiambishi hiki kina maumbo ya: **-w-**, **-il-w-**. Kiambishi tamati sababishwa humaanisha kiumbe kukamilishiwa (kufanyiwa) dhana ya kitenzi badala ya yeye mwenyewe kukamilisha.

Mifano ya kiswahili:

- Kupewa: ku-pa-il-w-a: l → φ/-w, a+i=e
- Kuuzwa: ku-uz-w-a

- Kufungwa:ku-fung-wa
- Kuliwa: ku-li-w-a
- Kutendewa: ku-tend-il-w-a: l →Φ/-w, i →e/ze-

❖ Viambishi tamati maalumu

Ni aina ya viambishi tamati ambavyo vinaambatana na mizizi michache ya vitenzi vya Kiswahili. Vinagawanyika katika makundi manne:

- Kiambishi tamati maalumu pindu
- Kiambishi tamati maalumu tendeka
- Kiambishi tamati maalumu cha hali
- Kiambishi tamati maalumu rudia

i) Kiambishi tamati maalumu pindu

Hujitokeza kwa namna mbili: **-ul-**, **-uk-**. Huongezea mzizi wa kitenzi dhana ambayo ni kinyume na dhana ya kawaida. Maana ya kitenzi ya kawaida inageuka kuwa kinyume.

Mifano:

-ul-

- funga – fungua: fung-ul-a: l →Φ/I-I
- tega – tegua: teg-ul-a: l →Φ/I-I
- chimba – chimbua: chimb-ul-a: l →Φ/I-I
- fumba – fumbua: fumb-ul-a: l →Φ/I-I

-uk-

- fungua – funguka: fung-uk-a
- chimbua – chimbuka: chimb-uk-a



ii) Kiambishi tamati maalumu tendeka: -ik-

Huongezea mzizi wa kitenzi dhana ya kutendeka.

Mifano:

- Vunja - vunjika: vunj-ik-a
- Kula – kulika: ku-li-ik-a: $i \rightarrow \phi / -I$
- Fuga – fugika: fug-ik-a

iii) Kiambishi tamati maalumu cha hali: -am-

Huongezea mzizi wa kitenzi dhana ya hali, yaani kuonyesha hali ya kitu.

Mifano:

- Kunja – kunjama: kunj-am-a
- Panda – pindama: pind-am-a
- Ficha – fichama: fich-am-a

iv) Kiambishi tamati maalumu rudia

Kiambishi tamati rudia kina maumbo ya: **-il-il-**, **-ang-**. Huongezea mzizi wa kitenzi dhana ya marudio.

Mifano:

-il-il-

- piga – pigilia: pig-il-il-a
- fuata – fuatilia: fuat-il-il-a

-ang-

- finya – finyanga: finy-ang-a



❖ Viambishi tamati vya kimaumbo

Ni aina za viambishi tamati ambavyo vinaambatana na mizizi yake ya vitenzi vya Kiswahili maana yake haitambuliki wazi wazi. Kuna aina mbili:

- Kuna ambavyo vinafanana na viambishi maalumu
- Kuna viambishi tamati vya kimaumbo ambavyo havifanani na vya kawaida au maalumu.

a) Viambishi tamati vya kimaumbo vinavyofanana na vya kawaida au maalumu.

Mifano:

- kimbia: kimb-il-a: l → φ/I-I
- tembea: temb-il-a: l → φ/I-I, i → e/ze-
- kutana: kut-an-a
- chelewa: chel-il-w-a: l → φ/-w, i → e/ze-
- achana: ach-an-a
- tambua: tamb-ul-a: l → φ/I-I
- tendeka: tend-ik-a: i → e/ze-

b) Viambishi tamati vya kimaumbo visivyofanana na vingine -al- na -at-

Mifano:

- angalia: ang-al-il-a : l → φ/I-I
- shangaa: shang-al-a: l → φ/I-I
- fumbata: fumb-at-a
- kamata: kam-at-a

Kwa ujumla, tunaweza kusema kwamba uambishaji katika lugha ni uwekaji pamoja wa viambishi na mzizi kwa namna mbalimbali bila kutilia maanani suala la aina ya

maumbo yanayopatikana alimradi tu miunganiko inayotokea ikubalike kisarufi katika lugha.

2. Vitenzi kutoka majina (nomino)

Uambishaji wa vitenzi kutoka majina hufanyika kwa kuongeza viambishi awali na viambishi tamati kwenye mashina ya majina.

Mfano:

NOMINO	VITENZI	UAMBISHAJI
Hesabu	Kuhesabu	Ku-hesab-u
Adhabu	Kuadhibu	Ku-adhib-u
Ahadi	Kuahidi	Ku-ahid-i
Ahadi	Kuahidiana	Ku-ahid-il-an-a
Sala	Kusali	Ku-sal-i
Safari	Kusafiri	Ku-safir-i

3. Vitenzi kutoka vivumishi

Uambishaji wa aina hii unafanyika kwa kuongeza kiambishi awali na viambishi tamati kwenye mashina ya vivumishi.

Mifano:

VIVUMISHI	VITENZI	UAMBISHAJI
Bora	Kuboresha	Ku-bor-ish-a: i → e/zo-
Safi	Kusafisha	Ku-saf-ish-a
Refu	Kurefuka	Ku-ref-uk-a
Chafu	Kuchafuka	Ku-chaf-uk-a

4.1.2. Uambishaji wa majina kutoka vitenzi

Uambishaji huu, unafanyika kwa kuongeza kwenye mizizi au mashina ya vitenzi viambishi awali vya majina na viambishi tamati. Viambishi tamati vinavyotumiwa katika uundaji huu ni hivi vifuatavyo: **-aji, -u, -i, -e, -o, -a**.

i) kiambishi tamati **-aji**

- fuga → mfugaji: m-fug-aji
wafugaji: wa-fug-aji
ufugaji: u-fug-aji
- imba → mwimbaji: mu-imb-aji
waimbaji: wa-imb-aji
uimbaji: u-imb-aji

ii) kiambishi tamati **-i**

Kuna aina mbili za viambishi tamati **-i**:

- Kuna kiambishi tamati **-i** ambacho hakisababishi mabadiliko ya konsonanti ya mwishoni mwa mzizi au shina la kitenzi.
- Kuna kiambishi tamati **-yi** ambacho kinasababisha mabadiliko ya konsonanti ya mwishoni mwa mzizi au shina la kitenzi.

Mifano 1:

- sema: usemi= u-sem-i
- shinda: ushindi= u-shind-i
- omba: ombi= φ-omb-i
- shindana: mshindani= m-shind-an-i
- soma: msomi= m-som-i
- ona: oni/maoni: ma-on-i

Mifano 2:

- linda: mlinzi= m-lind-yi: d+y=z
- pika: mpishi= m-pik-yi: k+y=sh
- lewa: mlevi= m-lew-yi: w+y=v
- loga: mlozi= m-log-yi : g+y=z
- vaa: vazi= ϕ -val-yi : l+y=z
- okoa : mwokozi= mu-ok-ul-yi: l+y=z, u→o/zo-, u→w/-l
- tembea: mtembezi= m-temb-il-yi: l+y=z, i→e/ze-
- tukana : matusi= ma-tuk-yi: k+y=s

iii) Kiambishi tamati **-u**

Kiambishi tamati hiki husababisha mabadiliko ya konsonanti ya mwishoni mwa mzizi au shina la kitenzi.

Mifano:

- tulia: utulivu= u-tul-il-u : l→v/-u
- pungua: upungufu= u-pung-ul-u : l→f/-u
- elewa: uelevu= u-el-il-w-u : l→ ϕ /-w, w→v/-u
- kosea: ukosefu= u-kos-il-u : l→f/-u, i→e/zo-
- haribia: uharibifu= u-harib-il-u : l→f/-u
- potoka: upotofu= u-pot-uk-u : k→f/-u, u→o/zo-
- choka: uchovu= u-chok-u : k→v/-u
- lemaa: ulemavu= u-lem-ul-u : l→v/-u, u→a/ze-
- aminika: uaminifu= u-amin-ik-u : k→f/-u
- changamka: uchangamfu= u-chang-am-uk-u : k→f/-u
- zoea: uzoefu= u-zo-il-u: l→f/-u

iv) Kiambishi tamati -e

- umba : kiumbe= ki-umb-e
- pinda : upinde= u-pind-e
- tuma : mtume= m-tum-e
- shiba : shibe= ϕ -shib-e
- poa : mpole= m-pol-e

v) Kiambishi tamati -o

- tenda : tendo= ϕ -tend-o
- tokea : tokeo= ϕ -tok-il-o
- kopa : mkopo= m-kop-o
- lima : ki-lim-o
- Kufa : kifo= ki-fu-o
- lipuka: malipuko= ma-lip-uk-o
- igiza : maigizo= ma-ig-il-y-o : l+y=z

vi) Kiambishi tamati -a

- Kukosa : kosa= ϕ -kos-a
- Kulima : mlima= m-lim-a

4.1.3. Uambishaji wa majina kutoka vivumishi

Uambishaji huu hufanyika kwa kuongeza viambishi awali vya majina kwenye mashina ya vivumishi. Kiambishi awali kinachotumika sana ni **u-** (ngeli ya 11) na ngeli ya 1 na ya 2 (**m-**, **wa-**) zinaweza kutumika vilevile.

Mifano:

- Zuri : uzuri= u-zuri (mzuri)
- Zembe : uzembe= u-zemb-e (mzembe)

- Baya: ubaya= u-baya
- Dogo: udogo= u-dogo
- Tamu: utamu= u-tamu
- Ekundu: wekundu= u-ekundu: u→w/-I
- Pana: upana= u-pana
- Refu: urefu= u-refu

4.1.4. Uambishaji wa maneno kutoka vielezi

Vielezi ni kategoria ya maneno ambayo huweza kuunda maneno ya aina nyingine.

Kwa mfano:

- Haraka = Harakisha- Harakisho -Uharakishaji
- Tayari = Tayarisha – Tayarisho – Utayari – Utayarishaji – Mtayarishaji - Mtayarishwaji
- Binafsi = Ubinafsi – Binafsisha - Ubinafsishaji
- Karibu = Ukaribu – Karibia – Karibisha - Makaribisho

4.1.5. Uambishaji wa vielezi kutoka majina

Ni utaratibu wa kuunda vielezi kutoka majina.

Mfano:

- Mzungu = kizungu (Mukamusoni amevaa kizungu)
- Mtoto = kitoto (Masabo anatembea kitoto)
- Mtajiri = kitajiri (Juma anazungumza kitajiri)

4.1.6. Uambishaji wa vielezi kutoka vivumishi

Ni utaratibu wa kuunda vivumishi kutoka vielezi.

Mifano:

- Zuri = vizuri (Mkulima analima shamba lake vizuri)
- Ema = vema (Wasichana wanazungumza vyema lugha ya Kifaransa)
- Kali = vikali (Anapotembea ananguruma vikali sana)
- Baya = vibaya (Mwenendo wake unamfanya achukiwe vibaya mno)

Tanbihi:

Kuna wakati ambapo majina huweza kubadili ngeli na kuwa katika ngeli nyingine.

Mfano:

Hali ya kawaida	Hali ya kukuza
Mtu	Jitu
Nyumba	Jumba
Nyoka	Joka
Mwizi	Jizi
Mbwa	Jibwa
Kisu	Jisu
Mfuko	Fuko

- a) Katika hali ya kukuza (kuonyesha ukubwa) tunaweza kuweka majina katika ngeli ya **Li-Ya**.
- b) Katika hali ya kudunisha (kuonyesha udogo) kuna wakati ambapo tunaweza kuweka majina nyingine katika ngeli ya **Ki-Vi**.



Hali ya kawaida	Hali ya kudunisha
Mlima	Kilima
Sanduku	Kisanduku
Mtoto	Kitoto
Tonge	Kitonge
Tumbo	Kitumbo
Vumbi	Kivumbi

Kama inatokea kwamba shina la neno ni silabi moja tu basi tunapachika **-ji-** katikati.

Mifano:

- Mti → kijiti
- Mwiko → kijiko
- Mto → kijito
- Mtu → kijitu
- Nyumba → kijumba
- Jiwe → kijiwe

Pia ikiwa nomino yenyewe huanzia na **-ki-** tunapachika **-ji-** katikati.

Mifano:

- Kichwa → kijichwa
- Kiboko → kijiboko
- Kitabu → kijitabu
- Kiatu → kijiatu



MAZOEZI

1. Yaunde majina sita kutoka kwa vitenzi ambavyo havikutajwa katika sehemu hii.
2. Viunde vitenzi saba kutoka kwa vivumishi ambavyo havikutumika hapa. Vitungie sentensi sahihi vitatu vya kwanza.
3. Toa mifano tano ya majina yaliyoundwa kutoka kwa majina mengine.

SURA YA TANO: UTUNGAJI

5.1. RISALA

5.1.1. Maana ya risala

Risala ni hotuba fupi inayosomwa mbele ya kiongozi kwa niaba ya kundi Fulani la watu hasa hasa wanafunzi, wafanyakazi, washiriki, wanachama, mafundi n.k ili kutoa maelezo ya haja zake mbalimbali na mahitaji yake au kuonyesha msimamo wa kundi hilo kwa kiongozi.

5.1.2. Mambo muhimu Katika utungaji wa risala

- Cheo cha kiongozi anayehusika
- Kundi linalowakilishwa
- Maelezo ya hali halisi ya maswala na msimamo wa kundi linalowakirishwa.
- Mapendeleo na hatua zinazotakiwa kuchukuliwa.
- Shukrani na mwisho

Tanbihi: Kama vilivyosemwa awali risala ni hotuba fupi lakini inachukua mambo muhimu tu na kuyaeleza. Hivyo risala yenyewe huwa ni maelezo ya muhtasari kwa jambo linalohitaji maelezo marefu Katika hotuba.

Utungaji wa risala unahitaji uangalifu sana na lugha ya heshima iliyo wazi kueleweka kwa kiongozi.

MAZOEZI

1. Jifanye wewe ni kiongozi wa darasa hili (kidato cha sita lugha). Tunga risala kuhusu shida za wanafunzi (wa darasa hili) mwishoni mwa mwaka na hatua zinazotakiwa kuchukuliwa.
2. Jifanye wewe ni mwanachama wa chama cha kisasa nchini Rwanda. Tunga risala kuwaelezea viongozi wa chama msimamo wa wanachama wenzako kuhusu mfumo mpya wa ngazi za uongozi bora nchini Rwanda.

SURA YA SITA: UTUNGAJI WA HOTUBA

6.1. Maana ya hotuba

Hotuba ni mazungumzo ya habari Fulani yanayotolewa kwa kundi la watu. Hotuba inaweza kuwa ndefu au fupi kufuatana na urefu wa matayarisho yake. Hotuba inaweza kuwa ya kuhimiza, kualika watu, kutenda jambo fulani, kupasha habari ya furaha au ya simanzi, kulingana na nia ya mzungumzaji.

Hotuba inaweza kuwa mahubiri ya kisiasa au mhadhara kutokana na mahali ilipotolewa (kanisani, kwa wanainchi, kwa ajili ya kundi maalumu)

Hotuba mara nyingi hutolewa kwenye majukwaa ya watu wengi ili kuwahimiza kutekeleza na kuendeleza jambo fulani. Hotuba zina lengo la kuwashawishi, kuarifu na kuwaburudisha watu kulingana na aina ya hotuba inayotarajiwa.

6.2. Sifa za hotuba nzuri

- Hotuba nzuri ina lengo la kuongeza ujuzi wa hadhira au kubadilisha fikra na matendo ya hadhira.
- Hotuba nzuri inafafanua, inachanganua na kueleza mada. Inafanya hadhira ibadilishe majibu yayo kuhusu mada.
- Hotuba nzuri inakuza ujuzi wa hadhira, inafanya msikilizaji ahisi, atende kinyume na alivyohisi na kutenda au achukue mwelekeo fulani.
- Hotuba nzuri huvutia maskio na mioyo ya hadhira.
- Hutumia pia lugha na picha zinazoeleweka kwa hadhira. Lugha ya hotuba inatakiwa iwe yenye heshima na taadhima.
- Hotuba nzuri inapaswa kuwa na mpangilio mzuri.

6.3. Muundo wa hotuba

Hotuba inaundwa na sehemu kubwa tatu ambazo ni pamoja na :

1. Utangulizi
2. Mwili
3. Hitimisho

i) Utangulizi

Mazugumzo Katika utangulizi yanatoa mwanga ama picha ya habari inayokusudiwa na kuzungumziwa. Kwa maana nyingine mazungumzo ya utangulizi huifunua kwa ufupi habari inayokusudiwa kuzungumziwa. Sehemu hii ya utangulizi huwa fupi ili isiweze kuingilia habari inayokusudiwa kuzungumzwa. Utangulizi lazima uwe wa kuisimua ili kuamsha wasikilizaji na kuyateka mawazo yao ili wawe na shauku ya kusikiliza unayotaka kusema.

Kwa mfano:

Kama hotuba inahusu” **kilimo bora**” inaweza kuanza hivi:

- Nani hajaweka mbolea Katika shamba lake?

Kama hotuba inahusu **usafi** unaweza kuanza hivi:

- Nani alitupa takataka hapa? Au wangapi walioga asubuhi ya leo?

Na kama hotuba inahusu **usalama barabarani**, waanza hivi:

- Nani ambaye gari lake halina taa?

Mifano hii ni mwongozo wa jinsi ambavyo utangulizi wa hotuba unatakiwa kutoa mwanga ama picha ya habari inayokusudiwa kuzungumzwa.

ii) Mwili

Sehemu hii ya hotuba ndiyo kiini cha mazungumzo yanayokusudiwa kuzungumzwa. Mawazo ya habari Katika sehemu hii lazima yapangwe kufuatana na uzito ama umuhimu wake. Wazo lililo muhimu lazima lianze kwanza kuzungumzwa kwa

ukamilifu ikiwezekana kwa mifano halafu watiwe na mawazo mengine nayo kwa kikamilifu na kwa mifano ikiwezekana. Hotuba inaweza ikashindwa kuwafishia ujumbe wasikilizaji kama muhutubu hakupanga mawazo yake kwa mtiririko unaoanzia na jambo lito na kuishia jambo dogo. Hotuba inatakikana ibebe maudhui sita mazito na kusafafanua kinaganaga. Hatibu anapasa kujieleza kwa ufasaha wa kuvutia masikio ya mioyo ya wasikilizaji kwa kutumia lugha itakayo gusa hadhira. Ili hadhira ivutike hatubu anaweza kutumia lugha ya picha, mifano yenye kujenga taswira za mawazo na vielelezo, ili wapokeaji wayatafakali yasemwayo. Hatibu anaweza kudhumisha shauku ya kusikilizwa kwa kutumia visa vifupi vinavyochangamsha, Pia hotuba zinakusudiwa kushawishi kama ilivyo Katika mijadala. Katika hali hii hoja zijadiliwe kwa jinsi ambayo inatimiza lengo la hotuba. Lugha ya hotuba inatakikana iwe ya heshima na taadhima.

Hotuba inatakiwa kuwa na mpangilio mzuri wa aya na mawazo yapangwe kwa mfululizo mzuri kimantiki. Hatibu awe akilejelea kwa mwenye kiti au mgeni wa heshima kila mara

Hotuba huandikwa kwa msembo halisi lakini bila matumizi yaalama za usemi halisi mwanzoni na mwishoni mwa hotuba, alama za usemi zinakumiwa kwa kufunga maneno ya kunukuu (dondoo).

iii) Mwisho

Katika sehemu hii ya hotuba mazungumzo yajumlishe mawazo yote yaliyozungumzwa kwa maelezo fasaha. Mazungumzo ni lazima yaifunge hotuba kwa picha inayofanana na ile ya utangulizi ili kumbukumbu ya habari iliyozungumzwa ibaki Katika mawazo ya wasikilizaji. Hitimisho ni sehemu ya mwisho ya hotuba ambayo inatoa kauli ya ushauri kwa azma ya kuhimiza hadhira itimize jambo fulani, Hatibu hufanya mhutajari wa hotuba yake

Hitimisho huvutia hadhira. Katika kuhitimisha hotuba hatibu huwaombea hadhira heri, baraka za mungu matakiyo mema na kumaliza kwa shukrani:

..... Asante.

..... Namshukuru sana kwa kunisikiliza.

Iwapo ni hotuba ya mijadala, hatibu hutamatisha hotuba yake kwa kushawishi wapinzani wake wamuunge mkono, katika kutetea au kupinga mada ya mjadala, ilimradi waafiki msimamo wake.

Tanbihi: Ikumbukwe kuwa kabla ya kuanza kutoa hotuba kuna utaratibu wa kusalimiana na pengine kujulisha majina.

6.4. Aina za hotuba

6.4.1. Hotuba ya kushawishi: ni aina ya hotuba yenye ujumbe na madhumuni ya kuathiri, kuvuta na kushawishi hadhira katika uchaguzi wake kwa kubadili majibu kwa fikra, tendo, hoja au bidhaa.

Sifa za hotuba ya kushawishi

- Inalenga kubadilisha kumbukumbu na matendo fulani ya hadhira,
- Ni hotuba ya kujenga picha mpya katika fikra za hadhira kuongeza nguvu za wasikilizaji na kubadilisha majibu yao kuhusu jambo fulani,
- Hotuba ya aina hii inafanya hadhira kuhisi na kufikiri kwa namna nyingine,
- Hotuba hii inalenga kubadili mienendo kwa uchaguzi kuvutiwa na ustahili.

6.4.2. Hotuba ya kuarifu au kujulisha

Hotuba ya kuarifu ni hotuba yenye madhumuni ya kuongeza ujuzi wa hadhira kuhusu mada, kusaidia hadhira kujifunza mengi kuhusu mada furani, kubadilisha ukweli wa imani ya hadhira kwa njia fulani. Hotuba ya kuarifu inawapa wasikilizaji hamu ya kutaka taarifa, husaidia hadhira kujua taarifa pamoja na kuiweka matendoni.

Sifa za hotuba ya kuarifu

- Kuwasilisha taarifa mpya kwa hadhira,
- Kuongeza ujuzi wa hadhira kuhusu mada,
- Kusawazisha ujuzi hadhira ilionawo kuhusu mada,



6.4.3. Hotuba ya kuburudisha

Hotuba za kuburudisha ni hotuba zenye madhumuni ya kufurahisha na kuburudisha hadhira, ni hotuba za kufanya hadhira iburudike, ichangamke, icheke kwa kutumia mbinu mbalimbali za kuburudisha.

6.4.4. Hotuba za nyakati maalum

Ingawa hotuba zote zina madhumuni ya kuburudisha kuarifu na kushawishi kuna wakati utahitaji hotuba ya wakati maalumu kama wakati wa mazishi, harusi na ndoa, kupata shahada.

Hotuba za aina hii zinasifa za kipekee zinatungwa kwa kufuata njia fulani kulingana na wakati huo maalumu.

Kuna aina nyingine za hotuba kama vile:

1. Urefu wa matayarisho

Kulingana na urefu wa hotuba, aidha matayarisho yake, kuna **hotuba ndefu** na **hotuba fupi**. Zipo pia hotuba zilizotzyarishwa kwa muda mrefu na hotuba za dharura yaani zinazotolewa papo hapo bila kupata muda mrefu wa kuziandaa.

2. Mahali zinapotolewa

Kulingana na mahali zinapotolewa hotuba zipo aina nyingi. Baadhi yake ni:

- i) **Mahubiri:** hizi ni hotuba au mafundisho ya kidini. Zinatolewa kanisani, miskitini au kwa njia ya redio.
- ii) **Hotuba za kisiasa na kiserikali:** mathalani matangazo ya kiserikali na chama, fafanuzi za mazimio au sheria.
- iii) **Mihadhara au masomo ya mwalimu darasani:** hizi ni hotuba au mafundisho ya mwalimu shuleni, hasa anapofundisha kundi kubwa la wanafunzi na hasa anapofundisha wanavyuo wa Chuo Kikuu.

3. Nia ya mzungumzaji

- Hotuba za kuhimiza na kualika watu kutenda jambo fulani,

- Hotuba za kupasha habari ya furaha,
- Hotuba za kushukuru na kukaribisha wageni,
- Hotuba za kupongeza na kutoa hongera,
- Hotuba za kumliwaza na kufariji mwenye huzuni,
- Hotuba za kushtumu na kukaripia

6.5. Ushirikiano na hadhira

Ushirikiano na hadhira ni taratibu ya kuhusisha mada yako, madhumuni, lugha na njia ya mawasiliano kwa kuondoa vizuwizi na wapanzani katika hadhira kwa kuongeza mvuto na uwezo wa kufika lengo hotuba yako.

Ushirikiano na hadhira unazingatia

- Uchaguzi wa mana inayolingana na kuipendeza,
- Kuonyesha madhumuni yako kwa hadhira, kuuonyesha lengo mwafaka,
- Kutumia lugha safi, sanifu, lugha inayolingana na kiwango cha ujuzi wa hadhira,
- Kujibu maswali bila kusitasita kwa njia sahihi na hekima,
- Kushirikiana na hadhira, lakini bila kubadili namna ulivyo au unavyohisi na kufikiri.

6.6. Fundisho muhimu wakati wa kutoa hotuba

Katika utoaji hutuba msemaji anapaswa:

- Kutumia sauti yake vizuri kulingana na wakati na hali vya hotuba; ni lazima sauti ihusishwe na ujumbe; msemaji anaweza kutia mkazo kwa maneno, kwenda pole pole, kutumia ridhimu, kutumia vituo mbali mbali, kupandisha na kupuuza sauti,
- Msemaji anatumia viungo vya mwili kama mikono na macho kwa kuwasilisha ujumbe wake vyema,



- Msemaji anapaswa kuvaa kulingana na hadhira yake na madhumuni ya hotuba.
- Msemaji anapaswa kutumia ishara na linganifu kwa ujumbe.

6.7. Mahali na hali ya hewa

Katika mahali na hali ya hewa hatibu anachunguza kiwango cha wasikilizaji, mazingira, wakati maalumu, mada pamoja na umuhimu wa hali fulani.

1. Kiwango cha wasikilizaji ni idadi ya wasikilizaji wote ambayo inasaidia katika uchaguzi wa mbinu za kuwasilisha ujumbe kama vifaa na matumizi mbalimbali ya ishara.

2. Mazingira hatibu anachunguza mahali ikiwa ni uwanjani, katika chumba, kuwepo na kutokuwepo kwa jukwaa au manufaa, kuwepo na kutokuwepo kwa vielelezo vya kusikika na kuona.

3. Wakati maalum ni kitu kingine ambacho huzingatiwa; huonyesha tofauti katika namna hhtibu anajifahamisha kwa hadhira yake hapa hatibu anapaswa kuwa mchangamfu, mcheshi, mtulivu, mwenye nguvu katika hotuba yake kulingana na mahali na hali na ujumbe unaotarajiwa kuwasilishwa.

4. Muda: muda unazingatia muda wa siku, muda wa kusema na muda wote ambao hatibu atachukua katika kuwasilisha hotuba yake. Hotuba za asubuhi zinawakuta wasikilizaji katika hali nzuri, hotuba za mchana zinawafanya kusinzia. Hadhira haitapendezwa na hotuba ya dakika 30 kusemwa katika dakika tano. Kwa upande mwingine hadhira itapendezwa na hotuba ya saa nzima kuchukuwa dakika arobaini na tano.

5. Umuhimu ni kitu kingine ambacho huchunguzwa katika mahali na hali ya hewa. Katika kiwango hiki maana inayoambatana na hali fulani hurazimisha hatibu kuhusiana na uzito wa hali ya mada. Hali fulani inaweza kuwa na maana lakini nyingine ikaoneka na kuwa dhaifu.

Hotuba za sikukuu zinachukuliwa kama za daraja la juu na rasmi kuliko hotuba zisizo rasmi za mikutano mbalimbali ya jamii. Ndio maana hatibu anapaswa kuchunguza umuhimu wa tukio ili asiye akachukuliwa vibaya na hadhira.

6.8. Kujali hadhira

Ni kutambua kwa mapana na marefu kuhusu hadhira kwa madhumuni ya kuongeza mawasiliano nayo. Utambuzi huu unaweza kufanywa kabla, wakati au baada ya kusema. Ni lazima kujua hadhira ili utayarishie ujumbe wako kwa hadhira hiyo. Hotuba si msemu wa kibinafsi mbele ya watu bali ni ujumbe unaotoka kwa mtu mmoja kwenda kwa watu wengi katika mandari ambapo msemaji na hadhira wanaathiriana mmoja kwa mwingine.

Uchaguzi wa mada na namna ya kuasiliana na hadhira vinaathiriwa sana na aina ya hadhira. Wakati ambapo tunaongea na watu tunatilia maanani tunachosema na namna tunachokisema, namna tunavyoongea na wageni siyo kama tunavyoongea na marafiki, namna tunavyoongea na waheshimiwa siyo kwa watu wa kawaida, namna tunavyoongea na watoto siyo kwa watu wazima sawasawa na hivyo, tunahitaji kutambua sifa za hadhira, kutambua au kufahamu wakati tunapochagua mada kwao, na kwa hivyo tunaamua namna ya kuwasilisha mada hiyo kwa hadhira. Kwa mara ya kwanza unapaswa kuangalia ujuzi wa kawaida wa hadhira na kwa mara ya pili unapaswa kufahamu demografia ya hadhira kama jinsia, umri, makabila, elimu, n.k

i) Ujuzi wa kawaida

Ni maoni ya umma ya wakati huo kuhusu matokeo mbalimbali na mambo mengine yaliyomo katika jamii kama utamaduni, mabadiliko na namna wanavyoelewa ukweli na uongo. Ujuzi wa kawaida unaonyesha namna watu wanavyofikiri ambavyo vyaweza kuathiri mienendo yetu. Kujua hivi wakati fulani vinatokana na kujua matokeo fulani kama kujua kinachoendelea katika jamii na katika ulimwengu wetu. Ujuzi wa kawaida unatusaidia katika uchaguzi wa mada. Ni lazima pia kuchambua saikolojia ya hadhira ambamo kuna fikra, imani, thamani na manufaa ya hadhira husika.

ii) Demografia

Inamaanisha sifa za watu ambozo ni pamoja na jinsia, umri, ukabila, vyeo vya kiuchumi, kazi zao na elimu yao. Ni vizuri kuchunguza jinsia katika hadhira kwa sababu namna msemaji anavyosema vyaweza kuathiri watu wa jinsia moja, ndiyo maana ni vizuri kuchunguza ikiwa mada yako inalingana na jinsia na usawajinsia,



na kurekebisha mada wakati unapohotubia wanaume kwa ujumla, wanawake kwa ujumla au mchanganyiko. Unapaswa kuchunguza vipengele vyote ambavyo vyaweza kuwafanya wanawake au wanaume kutenda kinyume na mada, ni lazima kujua kuwa badhi ya wanawake na wanaume wanahisi kuwa wanawake wanafanyiwa ubaguzi, ndiyo maana ni lazima kujiepusha na ubaguzi wowote wa kijinsia.

iii) Umri

Ni lazima kuuchunguza umri wa wasikilizaji katika uchaguzi wa mada ya hotuba kwa sababu wapendavyo vijana sivyo watu wakongwe hupenda. Maoni ya watu wakuu ni tofauti na maoni ya vijana.

iv) Hali ya kiuchumi

Fikra za watu ambao wanatajirika zinatofautiana na zile za watu duni. Kuna mada zinazoweza kuchaguliwa kwa wakwasi na mada nyingine ambazo zaweza kuchaguliwa kwa watu wa cheo cha chini kiuchumi.

v) Kazi

Wakati unapohotubia wafanyakazi, utahitaji kujua kazi za kila mtu. Uchaguzi wa lugha unayoitumia na mbinu nyingine katika hotuba yako vinaathiriwa sana na kazi za watu hao. Ni lazima kufanya uchaguzi wa maneno ambayo yanatumiwa kwa kazi zao za kila siku.

vi) Elimu

Ni kigezo muhimu cha kutiliwa maanani katika kujali hadhira. Ni vyema kujua ikiwa hadhira yako ni wasomi au la. Katika kujali hadhira ni lazima kuchunguza ukweli wowote hadhira ilio nao na mambo mengine yaweza kukusaidia kuwasilisha ujumbe wako bila vizuizi.

KIELELEZO CHA HOTUBA

Hotuba ya mwalimu mkuu kwa wazazi kuhusu mikakati ya maendeleo shuleni.

Mheshimiwa mgeni rasmi Bwana Eduard Kalisa, Mheshimiwa afisa wa elimu wilayani. Bwana Maike Gakware, walimu wenzangu, wazazi, wengine waalikwa na mabwana. Hamjambo? Nachukua fursa hii kuwakaribisha hapa shuleni. Napenda pia kwa niaba yangu binafsi na kwa niaba ya walimu kumshukuru mgeni rasmi kwa kuja kujumuika nasi leo hii kwa lengo la kubadilishana mawazo ili kuboresha kiwango cha taaluma, nidhamu na maendeleo katika shule hii.

Mgeni wetu wa heshima, kutokana na uwezo mdogo wa serikali Katika juhudi za kujenga na kuhakikisha mazingira mazuri ya utoaji wa elimu, shule zinawajibika kujitegemea kutafuta fedha za kujiendeleza. Wazazi wanalazimika kuchangia garama za mahitaji, hudhuma za kielimu, upatikanaji wa vifaa vya kitaalamu na uimarishaji wa mazingira ya kusomea. Kwa sasa kuna mahitaji ya msingi ambayo yasipokuwepo matarajio ya kuendeleza shule yataendelea kutumbukia nyongo.

Ili kutimiza azma ya kuinua viwango vya elimu, hatuna budi kujenga maktaba. Maktaba yenye vitabu vya kutosha vya rejea itawawezesha wanafunzi kusoma kwa ziada ili wapate kile kisichopatikana darasani. Shule hii vilevile inahitaji maabara ya kisasa iliyo katika hali ya kumruhusu mwanafunzi kusoma kwa vitendo yale mambo ya kisayansi yanayofundishwa kinadhria darasani. Wazazi wana jukumu la kuchangia kununua vifaa vya maabara. Kwa njia hii, taifa hili linategemea kupata watoto wenye maarifa na ujuzi na walioiva kitaaluma tayari kuendelea na elimu ya juu katika nyanja za sayansi.

Mheshimiwa mgeni rasmi, mojawapo ya mambo ya msingi kwa ufanisi wa shule kielimu ni walimu. Kazi ya ualimu ni kazi ya wito inahitaji moyo, juhudi na uvumilivu. Mafanikio yaliyopatikana yanatokana kwa sehemu kubwa na walimu kujitolea kufanya kazi bila kinyongo. Matunda ya juhudi zao tumeyaona. Kwa hilo hatuna budi kuwapongeza kwani chanda chema huvikwa pete. Lakini vile vile, napenda kuwaomba walimu waongeze ari na bidii ilimatokeo bora zaidi yapatikane Katika mitihani. Naomba wazazi muungane nami Katika kuwaenzi walimu hawa. Tuna uhaba mkubwa wa nyumba za walimu. Ni imani yangu na ninadhani ni imani ya wenzangu pia kuwa mazingira mazuri ya kuishi hapa shuleni ni kichocheo cha walimu kuchapa kazi bila

kinyongo. Kuwajengea nyumba ni njia ya pekee ya kuonyesha kuwa yunajali maslahi yao na tunawathamini kwa mchango wao wa kutusomeshea watoto. Hata hivyo, jifya moja haliinjiki chungu. Wazazi wanahitajika kushirikiana bega kwa bega na walimu Katika dhamani kubwa ya ulezi na utoaji wa taaluma kwa watoto. Vikao vya mara kwa mara baina ya wazazi na walimu vinavyolenga kuratibu maendeleo ya wanafunzi vitasaidia sana kuinua viwango vya elimu. Napenda kuwahimiza wazazi kuendeleza kuwapa watoto moyo wa kusoma, kuwaasa, kuwarudi, na hata kuwaadhibu endapo italazima. Kwa kufanya hivyo, vitendo vya utovu wa nidhamu ambavyo ni kikwazo kwa maendeleo mazuri ya watoto kimasomo vitapungua. Samaki hukunjwa angali mbichi.

Mgeni wa heshima, idadi ya wanafunzi wanaojiunga na shule hii inaendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka. Ongezeko hili linapasa kwenda sambamba na upanuzi wa vyumba vya madarasa na mabweni ili kupunguza msongamano. Madarasa tuliyonayo hivi sasa si ya hali ya kuridhisha na mara nyingi kuna usumbufu Katika utoaji na upokeaji wa elimu. Napendekeza kuwa idadi ya madarasa iongezwe. Aidha, kuna baadhi ya wanafunzi wa kutwaa wanaoacha shule kutokana na umbali ambao wanapaswa kusafiri kwenda na kutoka shuleni. Wanafunzi hao wanapofika shuleni huwa wanachoka kiasi cha kuwa wanakosa utulivu wakati wa masomo. Ningependekeza mfuko maalum uanzishwe kwa ajili ya kununua basi ili kuwaondolea adha ya usafiri wanafunzi hawa.

Mheshimiwa mgeni wa heshima, walimu, wazazi, wageni waalikwa, mabibi na mabwana, elimu ni haki ya msingi kwa hawa viongozi na wataalam wa siku za usoni. Tunapasa kujifunga vibwebwe na kuwa na moyo wa dhati na wa kufanikisha maendeleo tunayoazimia kwani hamadi kibindoni ni silaha iliyo mkononi.

Ahsanteni sana kwa kunisikiliza.

MAZOEZI

1. Mwalimu mkuu anakutaka utoe hotuba Katika hafla ya siku ya wazazi kuhusu uadhilifu na nidhamu miongoni mwa vijana. Watakaohudhuria kwenye sherehe hizo ni pamoja na Mkurugenzi, wazazi, walimu na wanafunzi. Tunga hotuba utakayotoa.

2. Toa hotuba kwa madhumuni ya kushutumu mila na desturi za kiafrika ambazo ni pingamizi ya maendeleo
3. Chama cha majadiliano Katika shule yenu kimekuomba ujadili mada isemayo: jamii haina budi kutilia maanani uzazi wa mpango. Andaa hotuba ukitoa mawazo yako ya kukubaliana na mada hiyo
4. Wewe umesoma na umehitimu shahada za juu katika elimu. Umealikwa kuwahutubia wanafunzi katika shule za sekondari uliyosomea. Wewe mwenyewe ukiwa kielelezo cha kupigiwa mfano, waeleze kwa kuwaelekeza yale ambayo wangefanya na kwa sababu gani ili nao wapate kufanikiwa katika masomo yao. Andika hotuba yako.

MAREJEJO

- Abdilatif, A. (1973). *Sauti ya dhiki*. Nairobi, Oxford University Press.
- Bakhressa Salim, K. & Islam K. (1999/1998/1997/1996/1995). *Kiswahili Sanifu: Darasa la saba*, Oxford University Press: Oxford New York.
- F.E.M.K. SENKORO (1988). *Ushairi: Nadharia na tahakiki*: Dar es Salaam University Press, Dar es salaam
- Kearney, P. (1999). *Public speaking in a diverse society*: second Edition: MC Graw-Hill: New York
- Kihore, Y.M., Massamba, D.P.B., Msanjila, Y.P. (2008/2007/2003). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu (SAMAKISA): Sekondari na Vyu*, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Dar es Salaam.
- MASSAMBA, D.P.B, KIHORE, Y .M, Hokororo, J.I (2001/1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA): Sekondari na Vyu*, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Dar es Salaam
- Mbunda, M. (1993). *Misingi ya uhakiki wa Fasihi*, English Press Limited: Nairobi.
- Mbunda, M. (1999). *Uhakiki wa Fasihi*, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Dar es Salaam
- Ndalu, A. (1997). *Mwangaza wa Kiswahili*, E.A.E.P Limited: Nairobi.
- Nelson .P, Scott. T& Judy P. (2007). *Public speaking: a guide for the engaged communicator*, M C Graw – Hill: New York
- Ngure, A. (2007/2006/2005/2004/2003). *Fasihi simulizi kwa shule zasekondari*, Phoenix Publishers: Nairobi.
- Polycarp. S.W (2000). *Uandishi wa Insha*, Acacia Stantex Publishers.
- SENKORO, F.E.M.K. (1988). *Ushairi: nadharia na tahakiki*. Dar es Salaam, Dare es Salaam University Press.

- SHAABAN, R. (1952). *Adili na Nduguze*. London: Macmillan and Co Ltd.
- TUKI. (2003). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Dar es Salaam
- TUKI. (2004/2002/1993/1981). *Fasihi Simulizi : Methali*: Chuo Kikuu cha Dar es Salaam: Dar es Salaam.
- Wizara ya Mafunzo ya Msingi na Sekondari. (1987). *Kitabu cha Kiswahili IV-VC: Kitabu cha Mwanafunzi*, Regie de l’Imprimerie Scolaire: Kigali.
- Ndayambaje, L. (2012). *Kanuni za kimofofonolojia katika nomino na vitenzi vya lugha za kiswahili na Kinyarwanda*. KIE, Kigali.

